**13 FEBRUARI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 13 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

**MHE. MARY F. MASANJA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu apokee salamu kutoka kwa wananchi wa Kinondoni, ukamwambie Mheshimiwa Rais kwamba tunaridhika na tunafurahi kuona kwamba ametuondolea shida za Kinondoni. Hatudaiwi sekondari, hatudaiwi elimu, hatudaiwi afya, ametuletea shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya mradi wa Daraja la Jangwani na vilevile pale Kigogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu mimi Mheshimiwa Waziri Mkuu linahusu barabara za ndani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wote tunajua barabara za ndani ni kiungo muhimu sana kwa uchumi wa watu na uchumi wa Taifa hili, zimekuwa na gharama kubwa, Mheshimiwa Rais na Bunge hili limekuwa likizungumzia juu ya umuhimu wa utunzaji wa barabara zile ambazo barabara moja sasa hivi inafikia kwa

kilometa moja shilingi bilioni 1.3, lakini ukarabati na utunzaji wake ni wa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafika wakati mashimo hata yakiwa madogo yanaachwa mpaka yanakuwa makubwa kiasi kwamba utengenezaji wake unasubiri utaratibu wa manunuzi ya mkandarasi, huku mashimo yanaongezeka. Hata ikitokea kalvati likivunjika linasubiri mkandarasi binafsi aje kutengeneza. Sasa suala hili linasababisha Serikali iendelee kupata hasara katika utunzaji wa barabara.

Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba mfumo ulioko sasa hivi umefeli, haufanyi kazi? Je, Serikali iko tayari sasa kufikiria kurudisha mfumo uliokuwepo zamani ambapo halmashauri zinatumia karakana zake, mitambo yake midogo kama ilivyo kwenye nchi nyingine kama *South Africa* ambapo mashimo yakitokea vikosi kazi haraka sana huenda kutengeneza na vinatengeneza kwa ukamilifu kiasi kwamba barabara zile zinakuwa na uhai mrefu wa kuweza kuishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, twende kwenye swali.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni hilo nimemuuliza, je, Serikali haioni kwamba inahitaji kubadilisha mfumo wa kutumia wakandarasi binafsi kutengeneza barabara zile, badala yake Serikali irudishe mfumo uliokuwepo awali wa kutumia vikosi kazi vya manispaa au hata *TARURA* yenyewe wakapewa kazi hizo kuweza kuzifanya badala ya kutegemea mkandarasi binafsi? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee salamu za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya Kinondoni, lakini pia na Taifa zima, salamu hizo zitafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukarabati, ujenzi mpya wa barabara nchini tuna uratibu vizuri na tumeufanyia tathmini mara kadhaa. Awali mfumo wa ujenzi wa barabara za vijijini zilikuwa zinakarabatiwa na halmashauri zenyewe, tukagundua kwamba hizi halmashauri zina uwezo tofauti, kuna halmashauri ndogo ambazo hazina uwezo kabisa, kuna halmashauri zenye mapato ya kati, lakini na halmashauri zile zenye uwezo kama Jiji la Dar es Salaam, Kinondoni na maeneo mengine nayo pia yana idara ya ujenzi iliyokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakati wote mlipokuwa mnaomba baadhi ya barabara zenu kwenye halmashauri zihamishiwe *TANROADS*. *TANROADS* ni taasisi ambayo tuliiunda kwa kushughulikia barabara kuu na ikaonekana kwamba *TANROADS* ni wakala ambao unafanya vizuri zaidi. Kutokana na maombi ya mara kwa mara tukaendelea kufanya tathmini ya ukarabati wa barabara za kwenye wilaya, lakini pia na vijijini, ndipo Serikali ilipoamua kuunda wakala mwingine wanaoshughulikia barabara za vijijini ambaye ni *TARURA* na ndiyo inayosimamia ujenzi wa barabara za kwenye miji na vijijini, na inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi ni pale ambapo umesisitiza kwamba ni vizuri kutumia mamlaka yenyewe ikarabati barabara badala ya wakandarasi binafsi. Sasa hili suala linategemea na yule mwombaji aliyeonesha kama ana uwezo, lakini akafanya vibaya. Sasa ambacho tutakifanya kutokana na ushauri wako na ombi lako, tunaendelea kufanya tathmini ya utendaji wa *TARURA*, lakini hadi sasa *TARURA* imeendelea kufanya vizuri kwa sababu wameendelea kukarabati, kutengeneza na kujenga barabara, iwe hawajengi wenyewe lakini wanawapa wakandarasi binafsi, wanawasimamia kazi hizo na tunaona mafanikio yanayofanywa na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kipindi hiki ambako mvua nyingi zimenyesha nchini na barabara nyingi zimeharibika,

*TARURA* wanaendelea kufanya kazi na sisi tunaongeza bajeti ili kuongeza uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, tutaendelea kuchukua ushauri wako na kuangalia mwenendo wa utendaji wa *TARURA,* lakini hasa wakandarasi binafsi. Tutaitaka *TARURA* isimamie wakandarasi hawa wanapopewa kazi wawe na uwezo wa kujenga barabara za kudumu kwa mujibu wa viwango vilivyopo ili hizi barabara ziweze kutumika kwa muda mrefu. Tutaendelea kuwapa fedha za matengenezo ya muda mfupi mfupi kwa ajili ya kuziba mashimo pale ambapo panatokea shimo badala ya kukaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, tukiwa tunaendelea kufuatilia mwenendo wa utendaji wa *TARURA* na maoni yenu, sasa niiagize *TARURA* kujikita katika kuhakikisha kwamba wanapotaka kujenga barabara na wanatoa kandarasi, basi mkandarasi huyo awe na uwezo wa kujenga kwa viwango vinavyokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia panapotokea uharibifu watumie ile fedha ambayo tunawapa ya matengenezo ya muda mfupi ili kuhakikisha kwamba uharibifu huo unazibwa mara moja na barabara ziendelee kutumika. Huo ndiyo mpango ambao tunao ndani ya Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza ninaipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inaratibu zoezi la utoaji wa mikopo ya 10% ya mapato yote ya halmashauri ambapo akina mama wanapewa asilimia nne, asilimia nne - vijana na asilimia mbili wanapewa watu wenye ulemavu. Hivi karibuni yamefanyika maboresho ya kanuni na kuruhusu kundi la vijana umri wake kuongezwa kutoka miaka 35 mpaka 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kundi la akina baba limeachwa nyuma, Serikali haioni ni wakati sahihi kuruhusu kundi la akina baba na wao linufaike na mikopo hii, kwa sababu kumekuwa na malalamiko makubwa ya akina baba kukosa fursa hii na wao ndiyo wakuu wa kaya, wao ndiyo wakuu wa familia hizi.

Je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kufanya marekebisho ya kikanuni ili kundi la wanaume (akina baba) na wao wanufaike kwa mikopo hii bila kigezo cha umri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fursa za mikopo kwenye maeneo mbalimbali zilifanyiwa tathmini, tukagundua kwamba yapo makundi hayana fursa nzuri, yana fursa ndogo sana kupata mikopo hii. Makundi haya ni yale ambayo baadaye tulianzisha mikopo maalumu ile kupitia halmashauri zetu nao ni walemavu, wanawake na vijana. Hili kundi tuliamua kuanzisha mfuko maalumu kwenye halmashauri zetu ili wapate nafasi ya wazi kupata mikopo kwenye haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la wanaume kupata nafasi. Hao ndio walikuwa wanapata nafasi ya wazi ya kunufaika na hata baada ya kubadilisha umri, bado ninaona wana nafasi kubwa. Wakati huo vijana wakiwa wanafikia umri wa miaka 35, wanaume ambao ni vijana wanapata nafasi ya kukopa wakiwa vijana, lakini baada ya miaka 35 kwa wakati huo walikuwa pia na fursa za kwenda kwenye taasisi za kifedha na ndiyo fursa ambayo tulifanya tathmini tukagundua kwamba wengi wanaopata mikopo kwenye taasisi mbalimbali za kifedha ni wanaume kuliko akina mama baada ya kufanya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata baada ya kuwa tumebadilisha kigezo cha kijana kutoka miaka 35 mpaka 45, bado kijana huyu huyu sasa tumemuongezea muda na bado

akizidi muda wa miaka 45 anakuwa mtu mzima, vilevile anaweza kupata mikopo.

Kwa hiyo, utakuta kundi hili pia bado lina nafasi ya kupata mikopo kwenye taasisi yoyote ya fedha, lakini pia wana nafasi ya kupata mikopo kwenye halmashauri. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba kundi hili lina fursa ile ya awali ya kuingia kwenye taasisi baada ya miaka 45, chini ya miaka 45 anapata kwenye taasisi na vilevile kwenye mikopo ya halmashauri. Kwa hiyo, fursa hii tumeigawa hivyo, tunajua kabisa haya makundi yote yanaweza kupata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini Serikali imefanya, tumeshazungumza na taasisi zote za fedha ambazo zinajishughulisha na utoaji wa mikopo, kufungua dirisha la mikopo kwa wajasiriamali wote na kuhakikisha kwamba kila anayefika pale anapata fursa sawa na mwingine ili kuboresha, kuwafanya Watanzania kubuni miradi na kuweza kupata mikopo ili waweze kujiongezea uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kufatilia hilo, tunaendelea kufanya tathmini, pale ambako tutagundua bado kuna kundi ambalo halipati fursa tutaendelea kuweka utaratibu kupitia mifuko tuliyonayo hata pia ndani ya Serikali. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha utoaji mikopo kwa makundi yote, ili yeyote kutoka kwenye makundi hayo aweze kupata fursa ya kupata mitaji na kuendesha shughuli za kiuchumi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sekta ya afya ni muhimu kwa Watanzania na kwa kuwa tunatambua kuna jitihada zinazoendelea za kuhakikisha kwamba sekta hii inaboreshwa,

ikiwemo kudhibiti magonjwa mbalimbali yayoambukiza na yasiyoambakiza mfano malaria na mengineyo. Kutokana na mazingira yetu mengi katika maeneo mbalimbali, kuna madimbwi mengi yamejaa maji, lakini na mrundikano mwingi wa uchafu katika maeneo mbalimbali unaosababisha mazalia mengi ya mbu.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mazalia haya yanamalizwa na mapambano dhidi ya malaria yanaendelea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Paresso, Mbunge kutoka Mkoa wa Arusha, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazalia ya mbu na kusababisha malaria, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wanajua kwamba Serikali yetu ina miradi maalumu ya uthibiti wa magonjwa ya malaria. Serikali inaendesha kampeni kwenye maeneo yetu yote mpaka vijijini ya usafi na usafi huu pia unagusa maeneo yote yenye mazalia ya mbu ili kuzuia kabisa na ikiwezekana kuondoa tatizo la malaria hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na utoaji wa *net* kwa matumizi ya watoto, mama na mtoto kwenye maeneo hayo kwa lengo la kujikinga na malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kampeni hii ya kufanya usafi, pia ikilenga kuondoa maeneo yote yenye mazalia ya mbu ambao wanasababisha malaria, inaenda sambamba na hamasa ya Serikali kwa wawekezaji kujenga viwanda vya kutengeneza dawa mbalimbali zinazosaidia kutibu ugonjwa wenyewe wa malaria, lakini pia kuua hata hayo mazalia ya vijidudu. Kwa sasa hivi wote mnajua kwamba pale Kibaha, Mkoani Pwani tuna kiwanda kikubwa sana kinachotengeneza dawa za kunyunyuzia maeneo haya yenye mazalia ya mbu ili kuua vijidudu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa nimefanya ziara pia kwenye eneo lile na kutoa wito kwa halmashauri zetu za wilaya

pamoja na kampeni ya usafi bado wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti zao ili wakanunue zile dawa pale Kibaha, waweze kunyunyiza kwenye maeneo yote ambayo yana mazalia ya mbu ili kuua kabisa hawa mbu. Tukiwa tunaendelea na kampeni hii, tutaendelea kuimarisha bajeti zetu kwenye halmashauri kununua hizo dawa, lakini pia ujenzi wa viwanda na uwekezaji. Tumeendelea kukaribisha wawekezaji wote wanaoweza kujenga viwanda vya kutengeneza dawa mbalimbali, mbali ya malaria lakini na dawa nyingine kwa lengo la kujaribu kupunguza kabisa kiwango cha magonjwa ili kuweza kulifanya Taifa hili kuendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa nakamilisha kutoa maelezo ya jibu hili niwahakikishie Watanzania kwamba kampeni yetu ambayo inaendelea kwa sasa nchini kote, itaendelea kuimarishwa mpaka ngazi ya vijiji. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, lakini pia Wakurugenzi kwenye halmashauri zao chini ya Maafisa Waganga wa Wilaya kuhakikisha kwamba wanafanya tathmini kwenye maeneo yote na kubaini maeneo yenye tatizo la ugonjwa wa malaria, chanzo cha ugonjwa huo na kuanza kufanya kampeni ya usafi angalau kila wiki na kampeni hii ambayo pia tunaendelea nayo kwenye maeneo ya wazi, kwenye masoko, shule, vituo vya mabasi itasaidia sana kupunguza kiwango cha uzalishaji wa wadudu ambao wanasabisha ugonjwa wa malaria, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini zaidi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza, Serikali ina mpango gani wa kuzipandisha hadhi Halmashari za Serikali za

Mitaa ambazo zimeshapitia hatua zote za wilaya, mkoa ili zipandishwe hadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa sasa upo uhitaji mkubwa wa baadhi ya maeneo ya kiutawala kutaka kupandishwa hadhi. Ninatambua pia Mheshimiwa Mbunge amekuwa akija mara kadhaa kuiomba Serikali kuupandisha hadhi ya Mji wa Moshi. Tunatambua zipo halmashauri kadhaa zimeshapitia hatua zote za kufikia vigezo vya kupata hadhi ya maeneo mapya ya utawala. Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa nyakati na kwa mara ya mwisho tulitoa maelekezo kwamba kwa sasa tutasimama kidogo kutoa maeneo mapya ya utawala baada ya kuwa tuna maeneo mapya ambayo sasa tunajenga miundombinu kuhakikisha kwamba rasilimali fedha na watu zinakamilika na maeneo haya kujiimarisha katika utoaji huduma kwa wananchi wa maeneo hayo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi tutakapojiridhisha kwamba utoaji huduma kwenye maeneo haya miundombinu imekamika, rasilimali watu zinatosha, rasilimali fedha pale za kujiendesha ni nzuri tutaendelea kutoa vibali kwa maeneo mapya ili maeneo yale yote yenye uhitaji wa mamlaka mpya iweze kupata mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa hiyo ninaamini Mji wa Moshi tayari umeshaleta taarifa, halmashauri wanaendelea kuchakata na kuona ukamilishaji wa miundombinu kwenye maeneo mapya ukoje na baadaye tutapata taarifa na Mheshimiwa Tarimo akiwa ni mmoja wa watu ambao wamehitaji sana mabadiliko kwenye mji wake basi Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI italishughulikia jambo hilo kulingana na wakati na kukamilika kwa mahitaji hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Rorya hayupo, Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, awali ya yote niipongeze Serikali kwa kuanzisha *East Africa Commercial and Logistics Centre* pale Ubungo ili kuwawezesha Watanzania waliokuwa wakihangaika kwenda China na mitaji yao midogo kuweza kujipatia bidhaa zao hapa nchini.

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuwalinda, kukuza na kujenga ushindani wa wawekezaji wazawa ikiwemo kutoa *preferences* kwa wawekezaji wa ndani na kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji wao na kuondoa vikwazo vinavyoweza kukwamisha uwekezaji na uzalishaji nchini ili zile bidhaa wanazoweza kuzalisha wao wazalishe badala ya kutegemea zile zinazoletwa na Wachina nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikuyapata vizuri maelezo ya awali ya swali lake yaliyojenga msingi wa swali zima, kwa hiyo, naomba arudie tena.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulenge uliza swali vizuri, fupi lieleweke.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kulinda na kukuza uwekezaji wa wawekezaji wazawa ikiwemo kutoa *preferences* kwa wawekezaji wa ndani na kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji wao ili zile bidhaa ambazo zinaweza kuzalisha nchini zizalishwe kuliko kutegemea kuletewa na Wachina?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa hamasa kwa wawekezaji wa ndani ili waweze kuwekeza na waweze kuzalisha bidhaa badala ya kutegemea bidhaa kutoka nje kama ambavyo Mheshimiwa *engineer* ameeleza kutoka China.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja tumetengeneza mazingira nafuu ya uwekezaji wa Mtanzania kwa kupunguza kiwango cha kuwa mwekezaji, tumepunguza kutoka dola 100,000 kuja mpaka dola 50,000. Hii inamfanya sasa mwekezaji wa ndani kuweza pia kutafuta mtaji. Akishapata dola 50,000 anaingia kwenye orodha ya wawekezaji na akishaingia kwenye orodha ya wawekezaji mazingira yanamwezesha Mtanzania kuweza kuwekeza moja anapata mazingira rahisi ya kupata ardhi, mwenyeji anamiliki ardhi, lakini wageni wanapata hati tu ya kuwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili; tumeona namna ambavyo bidhaa hizi zinavyoweza kuwekezwa na kufanyiwa biashara, hivyo tumetengeneza mazingira ya kumwezesha mfanyabiashara huyu au mwekezaji huyu kuendesha biashara yake katika mazingira rahisi. Tumeweka fursa na tumetengeneza mazingira ambayo yatamfanya afanye biashara vizuri, tumepunguza kodi, tumehakikisha kuwa hatua zile za kupata ardhi zinarahisishwa zaidi, lakini pia uendeshaji wa biashara anayoizalisha kama kuna biashara inazalishwa ndani ya nchi na kuna biashara aina hiyo hiyo inatoka nje ya nchi, ile inayotoka nje ya nchi tumeiongezea kodi ili kuipa nafasi hii kuingia kwenye masoko na kuweza kupata masoko yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira haya tumeendelea kuwahamasisha kwa Watanzania, lakini pia tumeweka masharti ya wawekezaji wa nje wanapokuja kuwekeza Tanzania lazima waambatane na Mtanzania kuwa mwekezaji mwenza ili Watanzania wapate nafasi ya kuwa wawekezaji wakubwa hapa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mazingira haya yote tumeendelea kufanya maboresho ya uwekezaji ndani ya nchi na kuhakikisha kuwa kila mwekezaji ambaye ni Mtanzania anafuata mazingira hayo ili kumwezesha kuwekeza kwa urahisi na kwa

gharama nafuu na masoko yake tunayo ndani ya nchi, lakini na nchi jirani na tumeendelea kujenga mahusiano na nchi jirani kwa kuja kufanya biashara ili wawekezaji wetu waweze kuwekeza vizuri na kupata faida kwenye uwekezaji wao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa nchini kwetu sekta ya michezo imekuwa ikikua kwa kasi sana na hili limedhihirishwa kutokana na kiwango cha soka nchini ambacho kimekua. Hata ukiangalia ligi yetu kwa sasa katika viwango vya Afrika tupo ndani ya ligi bora tano. Hili huwezi kulitengenisha na jitihada mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kukuza sekta ya michezo. Tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa jemedari namba moja katika kuhakikisha sekta ya michezo inakua nchini kwa kujenga miundombinu ya michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ya Awamu ya Sita imetengeneza mazingira mazuri ambayo yamevutia wawekezaji na wadau mbalimbali kushiriki katika sekta hii. Swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, ni ipi mikakati madhubuti ya Serikali ambayo itachukuliwa katika kuhakikisha halmashauri zetu kupitia mapato ya ndani wanajenga viwanja mbalimbali vya michezo vinavyokidhi vigezo vya kitaifa katika kukuza sekta hii ya michezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngassa, Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ukweli kwamba kiwango cha michezo nchini kimepanda na ninataka nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan ambaye yeye mwenyewe amekuwa nambari moja kuhamasisha Watanzania kushikiri katika michezo mbalimbali. Tumeendelea kufanya maboresho ya maeneo ya kufanyia mazoezi ikiwemo na viwanja na zipo halmashauri kadhaa ambazo zimeendelea kutenga bajeti zao kwa ajili ya kujenga viwanja na huku Serikali Kuu pia tukijenga viwanja vyenye viwango vya kimataifa kwa lengo la kuwafanya Watanzania wanapofanya mazoezi wafanye mazoezi kwenye viwanja vyenye viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua mfano wa mpira wa miguu huu umetuletea heshima nchi yetu. Kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba mpira wa miguu leo Tanzania ndio wenye ligi bora Barani Afrika. Sasa tumeona timu yetu ya Taifa, ligi yetu imepanda viwango mpaka nafasi ya nne Barani Afrika. Nimeona pia hata kwenye *ITV* kila siku inaeleza na kidunia ninadhani tupo wa 57, tunaona kwenye *TV* Azam wanatangaza mafanikio hayo kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya nayatokana pia na ujenzi wa viwanja kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye halmashari ambazo Mheshimiwa Mbunge amesema wanatengeneza kwa fedha zao kama vile Bukoba pale Kaitaba wamejenga uwanja mzuri, Nyamagana Jiji la Mwanza wamejenga uwanja mzuri. Pia tumeona kule Wilayani Ruangwa napo wamejenga uwanja mzuri, Kinondoni *(KMC)* wamejenga uwanja mzuri na sasa hivi Chunya napo wanajenga uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo zipo jitihada za kila halmashauri kujenga viwanja vyenye viwango vya kimataifa na ndivyo vinapandisha hadhi ya kiwango cha soka nchini. Hata kwa vilabu kimoja kimoja tumeona na ninyi ni mashahidi, timu zetu zile kongwe mbili Simba ni ya saba kwenye ngazi ya *CAF* na Yanga ni ya 13, Simba ya saba kwenye *CAF* na Yanga ya 13. Vyote hivi vipo zaidi ndani ya 20 bora, vinatuletea heshima kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya michezo nchini kwa michezo yote ili

kuhakikisha Watanzania wanapata kushiriki kwenye viwanja vilivyo bora, maeneo yenye miundombinu iliyo bora kwa lengo la kuwawezesha kufanya mazoezi kwenye viwanja hivyo. Tutaendelea kuimarisha ufundi katika michezo hiyo ili pia viwango viendelee kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa halmashauri na mikoa kuhakikisha kwamba taasisi zetu zote, maeneo yetu yote ya umma vijijini, wilayani na mikoani tunakuwa na viwanja bora vya kuwawezesha wananchi kushiriki kwenye michezo yao. Pale ambapo tuna viwanja tutahakikisha kwamba tunaviimarisha na kuviongezea uwezo wa viwanja hivyo kuweza kupokea washiriki wengi wa michezo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha kuwa ujenzi wa viwanja unaendelea na kwa ngazi ya Taifa mnajua kwamba sasa hivi tunajenga uwanja mkubwa Arusha, lakini pia tutakarabati uwanja wa Benjamin Mkapa, uwanja wa Uhuru na kule Zanzibar viwanja vya Gombani na Amani vinaimarishwa. Malengo ni kutaka kukaribisha heshima tuliyopewa ya kuweza kuwa wenyeji wa mashindano ya *CHAN* mwezi wa nane mwaka huu, na tunao uwezo huo. Pia mashindano ya *AFCON* mwaka 2027, uwezo huo tunao. Hiyo ndiyo faraja ya Watanzania kuona kwamba mashirikisho mbalimbali ya michezo duniani yanaiona Tanzania kuwa ni sehemu sahihi ya kuendesha michezo hiyo kwa ngazi ya Afrika na ya dunia pia. Huo ndiyo mkakati wetu wa Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana muda wetu umekwisha tumepangiwa dakika 30. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa majibu mazuri inaonesha unavyobobea na hasa majibu yako ya mwisho mwisho. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE.**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya kawaida, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mushashu.

Na. 215

**Waajiri Waliojiunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Nchini**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, asilimia ngani ya waajiri nchini wamejiunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)* na unawanufaishaje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Desemba 2024, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)* umesajili 93.39% ya waajiri wote kutoka katika mikoa yote Tanzania Bara waliotambuliwa na mfuko. Manufaa ya *WCF* kwa waajiri ni kuwa mwajiri anapojisajili na mfuko anaondokana na wajibu wa kuwapatia wafanyakazi wake huduma za matibabu au kuwalipa fidia pale wanapopata madhila na wanapoumia au kupata ajali, magonjwa ama kifo wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Jukumu hilo linabebwa na mfuko kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwenye majibu yake ya msingi amezungumzia juu ya fidia, ningependa atueleze kinagaubaga, huo Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unatoa mafao gani hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa *WCF* ni mfuko ambao unatoa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kufariki kabisa wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kazi, lakini kwa kuwa mfuko huu unachangiwa na mwajiri tu, je, yule mwajiri ambaye anashindwa kujisajili kwenye *WCF* na hivyo kuwafanya wafanyakazi wake wakakosa mafao haya anachukuliwa hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mushashu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ni mfuko maalumu ulionzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi wanapopata madhila yanayotokana na kazi kwenye maeneo yao na hivyo inapotokea aidha mfanyakazi ameugua na ugonjwa huo umesababishwa na eneo lake la kazi ama amepata ajali itakayoathiri afya yake au viungo vyake mfuko unachukua jukumu moja kwa moja la kuweza kufanya huduma zote za matibabu, lakini pia kutoa gharama za utengamao kuweza kuhakikisha anakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea kifo hivyo hivyo mfuko unachukua jukumu hilo kwa niaba ya mwajiri ambaye tayari atakuwa amesajiliwa na kwamba alikuwa analipa zile tozo ambazo zimeelekezwa na sheria. Hii ni pamoja na changamoto nyingine zozote ambazo anazipata na magonjwa kama igonomia

yanayotokana na kazi. Kwa hiyo mfuko unabeba jukumu hilo na unamsaidia mwajiri kuweza ku-*deal* na mambo ya uzalishaji zaidi na uwekezaji kuliko kushughulika na mfanyakazi mmoja mmoja ambapo mfuko unabeba jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake zipo nyingi kwa mujibu wa sheria, lakini kwa sababu ya muda nieleze kwa ufupi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili waajiri wanachukuliwa hatua gani ikiwa hawajajisajili. Utaratibu wa usajili ni jukumu kwanza la mwajiri ndiye anayepaswa kujisajili. Pia mfuko tunachukua jukumu hilo la kuweza kuhakikisha tunawatafuta. Mpaka sasa tumeshaenda maeneo ya kazi zaidi ya 37,726 ambayo haya ni maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti yake hapa, jinsi *WCF* inavyofanya kazi kuna tofauti na taasisi nyingine zinazosajili maeneo ya kazi. Mathalani tukichukulia benki moja ya *NMB* au *CRDB; CRDB* ina *branches* 90 na katika hizi *branches* 90 kwa mwingine angeweza kusajili kama ni maeneo ya kazi 90 au waajiri 90, lakini kwa *WCF* huyo ni mwajiri mmoja. Tunafanya kazi hiyo na tunaendelea kukaribia kufikia *target*, tupo zaidi ya 93% kati ya waajiri 40,000 ambao tunatarajia kuweza kuwapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuchukua hatua kwa wale ambao hawataona umuhimu wa kujisajili na sisi kama mfuko bado tunaendelea kuchukua jukumu la kutoa elimu na kuwatembelea kwenye maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Tarimo.

Na. 216

**Kuanza kwa Mradi wa *TACTIC TIRE II***

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa *TACTIC Tire II* utaanza na ni lini unatarajiwa kukamilika kwenye manispaa zinazohusika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa Mradi wa *TACTIC* katika kundi la pili ambao unajumuisha miji 15 ikiwemo Manispaa ya Moshi tayari umekamilika na nyaraka za zabuni kuwapata wakandarasi na wasimamizi ziliandaliwa na kutangazwa kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Umma *(NeST)* mapema wiki hii. Aidha, utekelezaji wa ujenzi unatarajiwa kuanza ifikapo Mei, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha miji katika Mikoa na Wilaya zake kwa ajili ya kujenga miundombinu muhimu ili kupendezesha miji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na nikiri nimeshaliona tangazo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa sababu tulishawahi kuleta hapa maombi ya kuombea wakandarasi wazawa waweze kupewa hii miradi ya Benki ya Dunia na Serikali iliridhia, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia kwamba wakandarasi wazawa watapewa kazi kwenye miradi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa mfano, kwa sababu kwenye barabara kunakuwa na barabara nyingi, Serikali iko tayari kuweka wakandarasi zaidi ya mmoja ili kazi iweze kukamilika mapema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba Serikali iliweka mpango wa

kuwahusisha kwa karibu wakandarasi wazawa katika kutekeleza miradi hii ya *TACTIC* na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge mpango wa Serikali ni kuendelea kuwapa kipaumbele wazawa, wale ambao watakidhi vigezo na kuwa na ushindani kulingana na taratibu za manunuzi ya Serikali. Kwa hiyo, wale ambao watakuwa na sifa hizo na watakuwa na vigezo na watashinda zabuni hizo, watapata miradi hiyo. Pia nitumie nafasi hii kuendelea kuwahamasisha wakandarasi wa ndani kutumia fursa hizi mara zinapotangazwa ili waweze kupata miradi hiyo na kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili; barabara ambazo ziko kwenye Mradi wa *TACTIC* ziko za urefu tofauti tofauti, lakini Serikali imeweka utaratibu wa kupata makandarasi kuzijenga barabara hizo. Hata hivyo, tunapokea wazo lake, tutalifanyia tathmini na kuona ikiwa barabara ni ndefu sana na inahitaji muda mfupi zaidi kutekeleza tutaona namna ya kuboresha ili utekelezaji wake uweze kukamilika kwa wakati, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mradi wa *World Bank* ambao unatekelezwa Dar es Salaam, Mradi wa *DMDP* wakandarasi wameshapatikana, je, wakandarasi hawa wataanza ujenzi lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu Dar es Salaam *(DMDP)* uko kwa awamu au makundi tofauti. Kuna kundi la kwanza, kundi la pili, lakini kwa kundi la pili ni kweli makandarsi wameshapatikana na tunatarajia wakati wowote kuanzia sasa watasaini mikataba kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo katika maeneo mbalimbali ambayo yamekwishatangazwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alfred. Hayupo?

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mheshimiwa Waziri, Halmashauri ya *Korogwe TC* pia ina mradi wa *TACTIC*. Wananchi wamekwisha pisha ujenzi wa mradi huo, je, unawaahidi kwamba lini wakandarasi wataonekana kwenye Halmashauri ya Korogwe Mji wakianza kazi ya kutengeneza barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Halmashauri ya Korogwe Mji iko kwenye mpango wa utekelezaji wa Miradi ya Uboreshaji wa Miji 45 *(TACTIC)*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Korogwe Mji kwamba Serikali iko kwenye hatua mbalimbali za ununuzi na mara hatua hizo zitakapokamilika makandarasi watakwenda kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kutekeleza miradi yote iliyomo kwenye *package* ya Korogwe Mji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali inakopa pesa kutoka taasisi mbalimbali za kimataifa za pesa kujenga barabara na vitu vingine, lakini taasisi hizi tunazokopa pesa zinakuja na masharti ya kutuwekea ma-*contractors* wanaowataka wao ambao siyo wazawa wa kutoka kwetu. Athari yake tunalipa deni kwa dola, tunalipa wakandarasi wa nje kwa dola. Naomba mjaribu ku-*revisit* masharti ya hii mikataba ili kutoa fursa zaidi ya pesa zibaki ndani, lakini vilevile wakandarasi wa ndani wapate fursa ya kupata hizi kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Fakharia.

Na. 217

**Kumalizika kwa Mradi wa *TASAF***

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza: -

Je, wananchi watarajie nini baada ya kumalizika kwa Mradi wa *TASAF?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo kwenye maandalizi ya kuendelea na Kipindi cha Tatu cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambacho utekelezaji wake utakuwa wa miaka mitano kuanzia mwaka 2026 hadi mwaka 2030 katika maeneo yote ya Tanzania. Lengo la Kipindi cha Tatu cha Mpango ni kuendelea kupambana na umaskini wa kaya za walengwa zenye hali duni ikiwa ni pamoja na makundi maalumu ya watoto na wazee. Mpango unalenga kuzijengea kaya hizi ujuzi wa ujasiriamali ili waweze kuwa na misingi ya kujitegemea. Mpango huu utaendelea kutumia dhana ya ushirikishwaji jamii ili kufikia malengo ya kupambana na umaskini, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shomar.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza sina budi kuishukuru Serikali kwa maelezo yao mazuri ambayo yanaweza kuwafanikisha wale wote walengwa wa *TASAF,* lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya walengwa ambao walikuwa kwenye *TASAF II* na ambao bado hawakufanikiwa kimaisha na wametolewa; je, kwenye hii *TASAF III* watakuwa na nafasi ya kuingizwa ili waweze kutengeneza maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina mpango mzuri katika *TASAF III* lakini pale pale waangalie baadhi ya washirika wetu wa maendeleo wamebadilisha sera zao za nje za misaada kwa nchi. Ninataka kujua, je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua imejipanga vipi ili iweze kufanikisha Mpango wa *TASAF III? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Fakharia kwa namna anavyofuatilia programu ya *TASAF*. Kuhusu suala la walengwa waliotolewa na bado hali zao ziko duni, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo. Kati ya walengwa waliotambuliwa 1,300,916 tayari waliohitimu wapo 400,000 na kati ya hao 400,000 nao tumewafanyia tathmini na kati yao 100,000 walionekana wana hali duni. Serikali haikuwaacha, imewapa mkono wa kwaheri ambao unaitwa *Lived Productive Branch* ya shilingi 350,000 na kuwapa elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini katika hao 400,000 ambao wame-*graduate* bado wana fursa nyingine ya awamu itakayokuja mwaka 2026 mpaka 2030 watapewa kipaumbele kulingana na hali zao zitakavyofanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu programu hii tutakayoanza mwaka 2026 mpaka 2030 awamu hii ya miaka mitano, Serikali inatambua mazingira tunayoenda na dunia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari tumeshakaa na wadau hawa wanaoweka fedha kwa ajili ya mfuko huu wa *TASAF* na tayari wadau wapatao 14 wakiongozwa na *World Bank* wako tayari na hivyo tutakapomaliza programu hii ya awamu ya pili kwa mwezi Septemba, tutakapoanza mwaka 2026 tayari tuna fedha za kuanza na wadau wameonesha *commitment*. Kwa hiyo, nikuondoe shaka programu hii itatekelezeka na hakuna jambo lolote litakalofanya ikwame, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ally Makoa.

Na. 218

**Kurudisha Bei ya Shilingi 27,000 Kuunganisha Umeme**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha bei ya shilingi 27,000 kuunganisha umeme kwa wananchi walioshindwa kulipia shilingi 320,000?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kuunganisha umeme zinafuata mwongozo uliowekwa na Serikali ambapo kwa maeneo ya vijijini, gharama ni shilingi 27,000 na nje ya hapo ni shilingi 320,960. Katika kuhakikisha tunapunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi, Serikali inatekeleza miradi ya kusogeza huduma ya umeme karibu na wananchi ikiwemo Miradi ya *Peri-Urban* kwa maeneo ya miji na miradi ya kupeleka umeme vitongojini kwa maeneo ya vijijini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na pamoja na hayo ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika jimbo ikiwemo kuwapelekea wananchi wetu umeme. Pia ninawapongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika jimbo langu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mitaa minne ambayo haijapata umeme. Sasa kuna mitaa mitatu ya Mongoroma, Chandimu na Hachwi hawajapata umeme kabisa. Nini mpango wa Serikali wa kufanya haraka na hawa pia wapate umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, iko Mitaa ya Tampori, Kwa Mtwara pamoja na Chemchem wamepata Mradi wa *REA* lakini *TANESCO* wamekosa nguvu ya kufikisha umeme mkubwa kwenye haya maeneo na wameshindwa nguvu kidogo tu.

Je, Serikali iko tayari siku mbili, tatu hizi ikawapelekea japo nguzo 200 ili *TANESCO* waweze kufikisha ule umeme, *REA* wanasambaza wananchi waendelee kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nishukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ilikuwa mitaa sita katika Jimbo la Kondoa Mjini ambayo ilikuwa na changamoto ya umeme na kupitia mradi wetu wa kupeleka umeme vijijini, mitaa mitatu ilipata mradi na mitaa mitatu ya Mongoroma, Chandimu na Hachwi bado haijapata mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, nia ya Serikali ni kuhakikisha maeneo haya yanapata umeme na kwa yale maeneo ya Tampori, Chemchem na Kwa Mtwara ambayo yanahitaji nguzo takribani 188, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nimeshamwelekeza meneja pamoja na makao makuu watafute angalau nguzo 100 ili tuweze kuanza katika mitaa hii mitatu. Ile mitaa mingine mitatu tunafanya mikakati kuhakikisha kwamba tunapeleka umeme mkubwa na wananchi wanaendelea kupata umeme wa uhakika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Mji wa Iguguno haujawahi kuwa mji, lakini mpaka sasa wanapelekewa umeme kwa shilingi 320,000. Lini Serikali itatoa tamko ili wananchi wa Iguguno waache kuteseka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, namna ambayo maeneo yanatozwa kwa kadiri ya mwongozo ambao tunao, tumeweka maeneo haya kwa maana ya miji pamoja na vijiji miji pamoja na maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, kwa yale maeneo ambayo ni vijiji miji na maeneo, lakini ambayo ni miji gharama yake ni hiyo shilingi 320,960 na yale maeneo

ambayo yamekuwa *categorized* kama vijiji gharama yake ni shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo analolisema Mheshimiwa Mbunge, tutaenda kufanya mapitio tuonea kama vile vigezo ambavyo vimewekwa havikidhi eneo hilo kuwa-*charged* shilingi 320,960 na baada ya hapo tutakuja na majibu ya mwisho, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote Mkoa wa Mbeya, baadhi ya vitongoji havijafikiwa na umeme kwenye Wilaya ya Rungwe, Kyela, Busokelo, Mbarali, Mbeya Jiji, Mbeya Vijijini na Chunya. Je, ni lini Serikali itampeleka mkandarasi ili aweze kuanza kupeleka umeme kwenye hivyo vitongoji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Mbeya mkandarasi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 alikuwa amechelewa, lakini nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi yupo katika hatua za mwisho za kupatikana na hivi karibuni atapatikana na tutaanza kazi ya kupeleka umeme kwenye hivi vitongoji 15 vya kila jimbo. Vilevile tunao mradi mkubwa kwa mwaka huu wa fedha kupeleka umeme kwenye vitongoji takribani 8,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, majimbo haya yote ambayo ameyataja na yenyewe yatanufaika na mradi huu ambao hivi karibuni tutautangaza, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Sophia Hebron.

Na. 219

**Wawekezaji wa Viwanda Vidogovidogo vya Zao la Ndizi**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatafuta wawekezaji wa viwanda vidogovidogo vya kuongeza thamani katika zao la ndizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, mkakati wa Serikali wa kutafuta wawekezaji wa viwanda vidogo ni kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI) kwa kuwajengea uwezo Watanzania ili waanzishe viwanda vidogo. Sambamba na hilo, pia Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vikubwa vya kuchakata mazao ili kuyaongezea thamani kwa wingi zaidi ikiwemo zao la ndizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Tanzania *(SIDO)* imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo katika maeneo yao kulingana na fursa zinazopatikana huko ili waweze kufanya uwekezaji wa viwanda vidogo vya kuchakata mazao mbalimbali ikiwemo zao la ndizi kwa kuwezesha teknolojia za usindikaji wa kaukau za ndizi, mvinyo wa ndizi, pombe kali na unga wa ndizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Caribbean zinaishi kwa kutegemea zao la ndizi katika soko la kimataifa. Hamuoni sasa kuna haja ya Serikali yetu kuhakikisha zao hili linauzwa kimataifa kwa sababu soko bado lipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, umezungumzia suala la *SIDO* kuweza kusaidia wananchi wa ngazi za chini, lakini *SIDO* imeishia katika Mikoa na Wilayani hazipo. Mheshimiwa Waziri, unaonaje mkashusha fedha na ofisi katika wilaya ili kusaidia wananchi hao waweze kutengeneza hizo *crispy* na hayo mambo mengine uliyoyaeleza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa ufuatiliaji wa kuweka viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo kutoka kule Tukuyu, lakini zaidi nachukua mawazo yake na ndiyo kazi ya Serikali tunayofanya kwamba moja; tungependa kama tunavyofanya kwenye mazao mengine kuuza ndizi kwa maana ya mazao ya kilimo kama ilivyo kwenye masoko ya kimataifa na hili linafanyika na tunaendelea kutafuta masoko zaidi kama ambavyo umesema mfano wa nchi za Caribbean wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni hili la pili, ambalo aliuliza swali, tunataka mazao ya kilimo yaongezwe thamani. Mheshimiwa Rais ameshafanya kazi kubwa sana ya kuongeza bajeti kwenye sekta ya kilimo, kwa hiyo, uzalishaji wa mazao ya kilimo umeongezeka. Kwa hiyo, tunadhani tukiweza kuyachakata, moja tutapunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, lakini pili kuongeza thamani kutakuwa na tija kwa wakulima lakini na mnyororo mzima wa thamani wa wafanyabiashara katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, moja; hili alilolisema ndiyo lengo la Serikali, tunataka *SIDO* iende kwenye ngazi za halmashauri ili waweze kukaa kule na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Niwakumbushe *SIDO* kutekeleza maagizo hayo ambayo Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo alisema kwamba sasa waanze kufungua ofisi kwenye ngazi ya halmashauri ili wawahudumie kirahisi zaidi wafanyabiashara katika ngazi hiyo na hilo tunaweza kulifanya. Katika mwaka wa fedha unaokuja tunaongeza bajeti kwa ajili ya *SIDO* waweze kufanya kazi vizuri, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, ameshakuelewa.

Waheshimiwa tunakwenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Florence.

Na. 220

**Uchimbaji wa Visima vya Maji kwenye Taasisi za Umma – Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itachimba visima virefu vya maji kwenye taasisi za umma hususan mashuleni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inapatikana katika maeneo yote ikijumuisha taasisi za umma zikiwemo shule na vituo vya kutolea huduma za afya. Serikali huzingatia uwepo wa taasisi hizo wakati wa usanifu wa miradi ya maji na hivyo kuhakikisha zinapata huduma hiyo muhimu wakati wa utekelezaji wa miradi. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia miradi

mbalimbali iliyotekelezwa imefikisha huduma ya majisafi na salama katika taasisi za umma 31,130 ambapo kati ya hizo, shule za msingi na sekondari ni 25,820 wakati vituo vya kutolea huduma za afya ni 5,310.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufikisha huduma ya maji kwa taasisi zote za umma nchini kupitia miradi inayoendelea na inayotarajia kujengwa ikiwemo kuchimba visima virefu kadiri itakavyoonekana inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza niipongeze Serikali kwa kuleta miradi ya maji katika Jimbo la Muhambwe. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kumtua mwanamke ndoo kichwani Jimbo la Muhambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, je, Serikali haioni kwamba iko haja sasa ya kuwa na programu maalumu ya kupeleka maji katika taasisi hizi za elimu na afya katika vijiji vyetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni mwaka mmoja sasa mitambo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika Jimbo la Muhambwe imechimba kisima katika Kijiji cha Lusohoko ambacho kinatoa maji zaidi ya lita milioni moja kwa saa na nikushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika katika kijiji kile.

Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuleta mradi katika kijiji kile ili wananchi waweze kupata maji tofauti na sasa ambavyo maji yanapotea tu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Muhambwe. Nilifika

katika eneo hilo na eneo hilo linatoa maji ya kutosha na visima ambavyo vimeshachimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, eneo la Lusohoko tayari Serikali imeshatangaza *tender* ya kumpata mkandarasi ambaye atakwenda kujenga mtandao wa maji ili uwafikie wananchi. Hiyo ni kwa ajili ya awamu ya kwanza, lakini kwa awamu ya pili tuna wataalamu pale ambao wameanza kufanya usanifu mradi mkubwa wa kutoka katika visima vilevile ili kwenda kusaidia vijiji 11 vikiwepo vijiji vya Bitale na Mji wa Kibondo wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba baada ya kukamilisha kwa huu mradi, basi utaweza kusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo hilo wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba Serikali inaendelea? Kama nilivyojibu swali la msingi, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba tunazingatia katika usanifu wetu. Taasisi za umma, vituo vya afya, shule, sekondari na hata taasisi za kidini, tunaendelea kushirikiana nao na sisi tutaendelea kufanya vikao vyetu na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na programu ya pamoja tunapokwenda kutekeleza ili tusije kuwa na mwingiliano na kuwa na *(duplicate of effort)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini kwamba tukifanya hivyo tutakuwa tumetatua changamoto hiyo. Napokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo amesema, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Serikali ilichimba kisima katika eneo la Mtandika, Wilaya ya Kilolo, je, lini itatoa pesa za usambazaji katika eneo la Kichangani, Kituo cha Afya Ruaha Mbuyuni pamoja na eneo ambalo Mzee Julius anaishi na kujenga tenki la Ikula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati amekuwa akifuatilia sana kuhusu eneo hili. Pia tunatambua kwamba kulikuwa na uhitaji wa fedha, napenda kutumia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tumeshapeleka fedha na kazi inaendelea. Kitua cha Afya cha Ruaha Mbuyuni pamoja na Kichangani watapata maji safi na salama, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kuchimba visima kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini kupitia mitambo aliyoitoa Mheshimiwa Rais, tuna zaidi ya visima kumi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Serikali ipo tayari kutoa fedha kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya visima hivi ili viwasaidie wananchi kupata huduma ya maji kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumeliona nchi nzima, programu ya visima 900 na mpaka kufikia Desemba, takribani visima 920 vilikuwa vimechimbwa kati ya visima 864 ambavyo tulikuwa tumepanga kuvichimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa kwamba wananchi wanahitaji kupata maji. Sasa tulichoamua ni kwamba kabla hatujatengeneza miundombinu au ile *point source* ya wananchi kupata maji, basi tuna uwezo wa kuunganisha maji

kwenye mtandao na wananchi wakaanza kupata maji wakati tukiwa tunaendelea kuzijenga zile *point source*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunalipokea na kwa msisitizo mkubwa tutalifanyia kazi ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama kwa wakati, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa katika miji 28 iliyopata miradi mikubwa ya maji na Makambako tupo, je, Serikali mpaka sasa imefikia asilimia ngapi kwenye mradi mkubwa wa Makambako?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Mji wa Makambako ni katika Mradi wa Miji 28 ambao unasimamia kutoka Njombe, Makambako na kuelekea jimbo moja ambalo liko upande wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili tulikuwa na mkandarasi ambaye kidogo kulikuwa na changamoto na baadaye akatafuta *sub-contractor* ambaye kidogo uwezo wake haukuwa unajitosheleza, tukatoa maelekezo ya kuhakikisha kwamba anambadilisha yule *sub-contractor* ili kazi iende kwa wakati. Mpaka sasa utekelezaji wa mradi huo unakwenda vizuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumeweka jicho pale ili kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati kulingana na mkataba ambao tulisaini na mkandarasi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

Na. 221

**Ulinzi wa Vyanzo vya Maji Nchini**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuvilinda na kuvihifadhi vyanzo vya maji nchini kwa kuzihusisha sekta za misitu, kilimo na mifugo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea na programu maalumu ya uhifadhi wa vyanzo vya maji iliyoanza mwaka 2021 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2035. Utekelezaji wa programu hiyo unashirikisha sekta zinazohusiana na maji pamoja na taasisi zake ambapo utekelezaji wake unafanyika kupitia Timu ya Kisekta ya Kitaifa iliyoundwa kwa kujumuisha sekta za Maji, Kilimo, Mifugo, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia programu hiyo kazi mbalimbali za uhifadhi wa vyanzo vya maji zinatekelezwa ikiwemo kutambua vyanzo vya maji, kuweka mipaka na kuvitangaza vyanzo hivyo kwenye Gazeti la Serikali, kupanda miti rafiki kwa maji katika vyanzo vya maji na kufanya kilimo na ufugaji rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa jumla ya vyanzo 3,285 vimetambuliwa ambapo kati ya hivyo 327 vimewekewa mipaka na vyanzo 68 vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Aidha, jumla ya miti rafiki 5,381,548 imepandwa katika vyanzo maji mbalimbali nchini. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua kwamba takwimu zinatuonesha kuwa nchini kwa mwaka tunapoteza karibu hekta 400,000 za misitu kutokana na uharibifu wa misitu na kwa kuwa uharibifu huu unachangia pia uharibifu wa vyanzo vya maji, je, Serikali ina mkakati gani wa kuzishirikisha taasisi au sekta za misitu, maliasili pamoja na TAMISEMI ili kuwa na mkakati wa pamoja wa kuhifadhi vyanzo vya maji nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili, kadiri ninavyofahamu ni kwamba Serikali imeweka fedha nyingi sana katika Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo ni matumaini makubwa sana kwa wananchi wa Tanzania ili kupata umeme ambao ni endelevu. *(Makofi)*

Je, kwa vile uharibifu wa misitu unachangia utiririkaji wa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuna mkakati gani wa kuzishirikisha taasisi za Maliasili, wenzetu wa Misitu na TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji unakuwa endelevu na uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere unakuwa endelevu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza na kama nilivyojibu katika jibu la msingi, ni kwamba kwanza kabisa mwaka 2022 Serikali kupitia tamko la Mawaziri wa Kisekta ambapo walikaa pamoja na kukubaliana kuweka mpango ambao utahakikisha kwamba tunakuwa na timu ya kitaifa. Hii timu ya kitaifa, ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na ushirikishwaji wa sekta ambazo zinaguswa na huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhakikisha kwamba mabwawa na miradi ya kimkakati ambayo inahitaji maji likiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere, basi maji yaweze kuwa endelevu kwa kufanya shughuli na kutengeneza mikakati ambayo itawezesha shughuli hizo ziwezeshe maji kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu hiyo bado iko kazini na inafanya kazi vizuri kabisa, bado hatujapata changamoto yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, Wizara ya Maji iliandaa mpango wa utekelezaji wa utunzaji wa vyanzo vya maji. Mpango huo unahusisha upandaji wa miti rafiki, lakini pia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ambazo hazitakuwa na madhara yoyote katika kuathiri vyanzo vyetu vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa rasilimali za maji ni lazima zilindwe ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama, mamlaka zetu za maji, wakala wetu wa maji, waweze kuwa na vyanzo vya uhakika na endelevu ambavyo havitoingiliwa na shughuli za kibinadamu ambazo zitasababisha vyanzo hivyo kupoteza upatikanaji wa maji. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dkt. Thea.

Na. 222

**Kukipatia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA)* Tawi la Tunduru Eneo la Kiwanda**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kukipatia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA)* Tawi la Tunduru eneo la kiwanda cha kubangua korosho kilichotelekezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kulifanya eneo la kiwanda cha kubangua korosho kilichopo Tunduru katika Mkoa wa Ruvuma kama Tawi la *SUA* ni la muhimu na Serikali imepokea. Aidha, Serikali itakaa pamoja (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na mmiliki wa kiwanda ambaye ni Wizara ya Viwanda na Biashara) ili kufanya mazungumzo na tathmini kabla ya maamuzi ya *SUA* kulichukua eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri yanayoleta matumaini. Nina mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mpaka sasa ni programu gani zinaendelea pale *SUA*?

Swali la pili, ni lini Waziri sasa ataamua kupeleka Kamati ya Elimu, Tunduru ili ikaone kazi zinazofanyika pale? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jambo lake la kwanza ambalo linazungumzia suala la programu gani, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokwishakueleza kwenye majibu ya swali la msingi, eneo hili la Tunduru kwa hivi sasa linatumika na Chuo chetu cha *SUA* kwa lengo la kutoa yale mafunzo ya vitendo kwa kozi za sayansi ya misitu na usimamizi wa wanyamapori kwa wale wanafunzi wa shahada ya kwanza ambao wanasoma kwa kipindi cha miaka mitatu pale chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba dhamira ya Dkt. Thea ni kulifanya eneo hili kuwa *campus* ya Chuo Kikuu cha *SUA*. Nimuondoe hofu, kwa hivi sasa lile eneo ni dogo, lina ukubwa wa ekari tisa na hivi sasa tuko kwenye mazungumzo

Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili kutuongezea eneo la angalau ekari 300 ili tuweze kufungua *campus* kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anazungumzia kuhusu Kamati yetu ya Bunge, kwamba ni lini inaweza kwenda?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tutakaa na Mwenyekiti wa Kamati na sisi kama Wizara tuweze kupanga ratiba vizuri ili ikiwezekana kabla ya Bunge la mwezi wa nne, tuweze kutembelea eneo hili la Tunduru ili na ninyi wenyewe mkajionee maendeleo yaliyofanywa na Chuo chetu cha *SUA*. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Dkt. Alfred James.

Na. 223

**Uhitaji wa Gari la Zimamoto – *Korogwe TC***

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini Jeshi la Zimamoto *Korogwe TC* litapatiwa gari jipya la zimamoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe lipo gari moja la zimamoto na uokoaji aina ya Isuzu lenye ujazo wa lita 5000 za maji linalotumika kwa shughuli za maokozi. Kwa sasa Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza mradi wa ununuzi wa vifaa na magari ya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni 100 kutoka kwa Kampuni ya *NAFFCO FZCO* iliyopo Dubai. Mradi huo utawezesha kupatikana kwa vitendea kazi mbalimbali ikiwemo

magari 150 ya kuzima moto na uokoaji yatakayosambazwa nchi nzima ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Korogwe, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred.

**MHE. DKT ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Serikali imejibu, hata hivyo, nataka kutoa msisitizo kwamba gari lililopo mara nyingi linaharibika sana na Mji wa Korogwe ni mji unaokuwa kwa kasi, majanga ya moto yanatokea mara nyingi na tunashindwa kuya-*control*.

Je, Serikali inatuhakikishia ni lini magari hayo yatapatikana ili Mji wa Korogwe upate gari jipya na zuri ili tuachane na hili la zamani? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, mradi huu tayari tumeshaagiza magari na tumeyalipia. Kwa hiyo, Mbunge awe na subira, magari yatafika na Mji wa Korogwe utapata gari kwa ajili ya zimamoto na uokoaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, katika Jimbo la Tarime Vijijini, tarehe 8 kuamkia tarehe 9 walitekwa watu watatu akiwepo Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Itiro. Mpaka leo asubuhi hakuna taarifa yoyote ambayo imetolewa na *RPC*, *OCD* wala *DC*, badala yake wanasema hawajui hao watu wako wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo limekuwa linazua taharuki, watu wamekuwa wakipigiwa simu za vitisho na maswali yao wanauliza ya kisiasa sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, swali lako? Uliza swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sasa Wizara ya Mambo ya Ndani, itoe kauli juu ya jambo hilo la utekaji na hali tete iliyopo kule Itiro, ili wananchi wengi waendelee kuishi kwa amani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unazo taarifa za matukio?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa, saa saba nitalifanyia kazi na tutaongea na Mheshimiwa Mbunge tujue tunafanyaje…

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, kaa naye ulifanyie kazi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea na maswali yetu yamekwisha. Sasa ni kipindi cha wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliokaa katika Jukwaa la Spika; tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Tausi Kida - Katibu Mkuu; Ndugu Gilead Teri - Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC);* Ndugu Charles Itembe - Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji kwa Mauzo Nje *(EPZA),* Ndugu James Maziku - Mkurugenzi Huduma kwa Wawekezaji; na wageni wengine 11 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambao ni watendaji na maafisa kutoka Wizara hiyo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde - Waziri wa Madini, kutoka Beijing China, wakiongozwa na Ndugu Theobalt Maina, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 10 wa Mheshimiwa Omary Kipanga - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM kutoka Mafia, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylivester Mabula ambao ni watoto wake kutoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ambaye ni Ndugu Hafsa Hamad mtoto wake kutoka Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mchoteka, Tunduru Kusini, Mkoa wa Ruvuma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambaye ni rafiki yake Ndugu Rashid Mbegu kutoka Arumeru Magharibi, Mkoa wa Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Wakurugenzi wa *Current Group* kutoka Musoma Mjini Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 122 wa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Wenyeviti wa CCM wa Matawi ya Jimbo la Mkalama kutoka Mkoa wa Singida, karibuni wageni, Mbunge wenu anafanya kazi vizuri sana hapa ndani. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ambao ni wanafunzi 20 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari *One World* ya Wilaya  ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wafanyakazi wa *Sky International Tv* kutoka Mkoa wa Songwe na walimu wa Shule ya Msingi ya Iyula Malaika ya Ntyuka, Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Peter Getere, mpiga kura, mke na mtoto wake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda kutoka Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndugu Kiria Laizer, Mwenyekiti wa CCM Wilaya na Ndugu Baraka Laizer, Mwenyekiti wa Halmashauri, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ambao ni Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Mkoa wa Singida - Ndugu Timoth Kingu na kijana wake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni walimu na makada wa CCM kutoka Mkoa wa Mwanza. Pia yupo mgeni mwingine Ndugu Ngwasi Zakari ambaye ni mdogo wake, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*). *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Wahadhiri wawili wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) kutoka jijini Dodoma, karibuni.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 95(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, pamoja na mambo mengine iliitaka Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezezaji ili kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kama nyenzo muhimu ya kukuza uchumi. Kwa kuzingatia maelekezo haya, katika Mpango *wa* Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(*2021/2022 – 2025/2026*)*, wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, uliweka lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kama msingi muhimu katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipoingia madarakani, pamoja na mambo mengine ilidhamiria kukuza uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara kama sehemu ya mikakati muhimu ya kuchochea ukuaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi kubwa zimeendelea kufanyika katika kutekeleza maelekezo ya Ilani, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais katika kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kutokana na juhudi hizi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mafaniko mengi yamepatikana. Kwa mfano, idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)* iliongezeka kutoka miradi 256 mwaka 2021 hadi kufikia miradi 901 mwaka 2024. Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji imeutangaza mwaka 2024 kama mwaka bora zaidi katika sekta ya uwekezaji nchini kutokana na ukweli kwamba ndiyo mwaka ambao *TIC* ilisajili miradi mingi zaidi ya uwekezaji (miradi 901) tangu Tanzania ianzishe kituo hiki na kuanza kurekodi miradi ya uwekezaji mwaka 1996. Hii inavunja rekodi ya miradi 885 iliyosajiliwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze chimbuko la muswada huu. Katika kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, mwaka 2023 Serikali ilifanya tathmini ya utendaji kazi wa mashirika na taasisi za umma nchini. Pamoja na mambo mengine, matokeo ya tathmini hii yalionesha kuwa majukumu ya baadhi ya taasisi hizo yanashabihiana na kuingiliana. Hali hii imekuwa ikisababisha mwingiliano wa kiutendaji na kuongeza gharama za uendeshaji na kufanya biashara na hivyo kuathiri ufanisi uliokusudiwa. Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hii, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunganisha na/au kufuta baadhi ya mashirika na taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Mamlaka ya Kukuza Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi *(EPZA)* ni baadhi ya mashirika ya umma ambayo majukumu yake yalibainika kuingiliana na kushabihiana na hivyo kuamuliwa kuunganishwa na kuwa taasisi moja. Hivyo basi, chimbuko la muswada huu ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)* na Mamlaka ya *EPZ (EPZA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malengo ya muswada, Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi una malengo ya kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji Tanzania; kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji; kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu; ulinzi, uvutiaji; uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini; kuweka utaratibu wa kuanzisha, kuendeleza na kusimamia maeneo

maalumu ya kiuchumi; kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya 2022, kufuta Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya 2002 na kufuta Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielezee maudhui ya muswada; muswada huu umegawanyika katika sehemu tisa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria inayopendekezwa kutungwa, maelezo kuhusu matumizi ya sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya muswada inaweka mfumo wa kitaasisi wa uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini. Sehemu hii inaanzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ambayo itakuwa chombo kikuu cha Serikali cha kuratibu uhamasishaji, uwezeshaji, usimamizi na uendelezaji wa uwekezaji nchini. Sehemu hii pia inaanzisha Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji itakayokuwa na jukumu la msingi la kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri uidhinishaji wa vivutio vya ziada kwa wawekezaji wa kimkakati, kuhakikisha kuwa kuna mazingira mazuri kwa uwekezaji katika sekta binafsi na miradi ya uwekezaji inaendelezwa na kudumishwa, kusimamia miradi mikubwa yenye matokeo makubwa kitaifa kulingana na ukubwa, mtaji, manufaa ya kiteknolojia na ajira, na kuidhinisha uanzishwaji na usimamizi wa maeneo ya uwekezaji wa kimkakati. Aidha, sehemu hii inaweka masharti na majukuku ya bodi, pamoja na masharti ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka na watumishi wengine wa mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uwekezaji. Katika sehemu hii, masharti yanawekwa kwa ajili ya kuzitaka taasisi za Serikali kushirikiana na mamlaka katika kutoa huduma mbalimbali kwa

wawekezaji kupitia Kituo cha Huduma Mahali Pamoja. Vilevile sehemu hii inaweka masharti kuhusu mfumo unganishi wa kielektroniki. Mfumo huu unalenga kuunganisha mamlaka muhimu za Serikali zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uwekezaji. Hatua hii itatoa fursa kwa wawekezaji kupata huduma kwa urahisi bila kulazimika kushughulikia vibali au leseni katika taasisi mbalimbali. Aidha, sehemu hii inaweka masharti kuhusu usajili wa wawekezaji wa ndani na wa kigeni na utoaji wa cheti na leseni ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pia imebainisha vigezo kwa mwekezaji kupewa hadhi ya kuwa mwekezaji wa kimkakati kwa kuzingatia kiwango cha chini cha mtaji kwa mwekezaji wa ndani na mwekezaji wa kigeni. Sehemu hii pia inaweka vigezo kwa mwekezaji anayetaka kubadili au kuacha kuendeleza uwekezaji alioufanya. Aidha, sehemu hii inabainisha masharti ya kupata vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyotolewa chini ya sheria mbalimbali kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika sheria hizo. Vilevile ili kutoa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani sehemu hii inabainisha kuwa Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha, anaweza kubainisha maeneo mahsusi ambayo wawekezaji wa ndani wanaweza kupewa vivutio kwa kuzingatia sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi inayofaa kwa ajili ya uwekezaji, muswada unapendekeza kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa Benki ya Ardhi. Kwa mujibu wa masharti yanayopendekezwa, Benki ya Ardhi itakuwa ni kanzidata itakayohifadhi taarifa kuhusu ardhi inayopatikana sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya uwekezaji. Mbali na ardhi itakayotengwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji, Benki ya Ardhi itajumuisha pia ardhi inayomilikiwa na watu binafsi ambao wangependa kukodisha ardhi yao kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya muswada inaainisha masharti kuhusu uanzishaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi. Maeneo yatakayoanzishwa yanaweza kuwa kongani za viwanda, maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya

nje, maeneo ya biashara huru, maeneo ya bandari huru, maeneo ya kilimo, kongani za utalii, kongani za sayansi na teknolojia, na maeneo mengine kadiri mamlaka itakavyobainisha. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu taratibu za kiforodha katika maeneo maalumu ya kiuchumi, uingizaji na utoaji wa huduma na bidhaa katika maeneo maalumu ya kiuchumi, usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi, na masuala ya utoaji huduma katika maeneo maalumu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya muswada inaainisha haki na wajibu wa Serikali na wawekezaji. Muswada unapendekeza kuipa Serikali haki na wajibu wa kusimamia shughuli za uwekezaji ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya sera na sheria za nchi, ikijumuisha maafisa wa mamlaka kuweza kuingia katika eneo ambalo shughuli za uwekezaji zinafanyika kwa madhumuni ya ufuatiliaji. Wajibu unaopendekezwa kwa mwekezaji katika sehemu hii ni pamoja na kutii sheria za nchi, kuendesha shughuli za uwekezaji kwa namna inayolinda walaji, mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka na taasisi nyingine za Serikali pale zitakapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii inaainisha pia haki mbalimbali alizonazo mwekezaji katika kipindi cha kutekeleza mradi wa uwekezaji ambao amewekeza. Haki hizo zinajumuisha kuhamisha nje ya nchi faida, mapato na gawio kupitia benki yoyote baada ya kulipa madeni ya kodi, ada au tozo za Serikali na malipo mengine yaliyowekwa na sheria. Aidha, sheria inaweka kinga ya kutotaifishwa kwa miradi ya uwekezaji bila fidia stahiki kwa mujibu wa sheria na kupata mikopo katika benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa ndani ya nchi kwa ajili ya kufadhili miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu wawekezaji wa kigeni kutobaguliwa katika shughuli na fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Pamoja na masharti hayo, Serikali haitazuiliwa kuchukua hatua zozote za ziada kwa ajili ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita ya muswada inaainisha masharti kuhusu ushughulikiwaji wa malalamiko na utatuzi wa migogoro. Katika sehemu hii, inapendekezwa kuwa mwekezaji anaweza kuwasilisha kwa mamlaka malalamiko kuhusu mwenendo au kitendo cha taasisi yoyote ya Serikali ambacho hakuridhishwa nacho na mamlaka itakuwa na wajibu wa kufanya jitihada za kushughulikia malalamiko hayo ili kutoathiri shughuli za uwekezaji. Sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wowote uliotolewa na mamlaka na inaainisha pia utaratibu wa utatuzi wa migogoro baina ya wawekezaji na mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba ya muswada inaainisha masharti ya fedha; masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya mapato ya mamlaka na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu, uandaaji wa bajeti na taarifa ya mwaka. Kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Serikali, mamlaka itaandaa hesabu na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane ya muswada inaainisha masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayohusiana na masuala ya uwekezaji na adhabu zake; utunzaji wa rejesta ya uwekezaji; matumizi ya sheria nyingine; pamoja na mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria inayopendekezwa. Aidha, sehemu hii pia inapendekeza kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022; Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya mwaka 2002; na Sheria ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2006, pamoja na kutambua masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na sheria zinazopendekezwa kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa ya muswada inajumuisha marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuendana na masharti yanayopendekezwa katika sheria itakayotungwa. Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni pamoja na Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia wa Kigeni, Sura ya 436; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa,

Sura ya 147; na Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapomalizia ninaomba kusisitiza mambo matatu ambayo kwa kiasi kikubwa ni mapya katika muswada huu.

Mosi, ni kuanzishwa kwa mamlaka mpya itakayochukua nafasi ya *TIC* na *EPZA* ambayo ipo katika Ibara ya 4 ya muswada unaopendekezwa. Mamlaka hii itaitwa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania *(Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority – TISEZA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, muswada huu unapendekeza kuwepo kwa fursa na vivutio mahususi kwa wawekezaji wa ndani pekee ipo Ibara ya 22.

Tatu, muswada unapendekeza kuanzishwa kwa Benki ya Ardhi, kifungu cha 23. Kupitia Benki hii, mbali na ardhi itakayotengwa na mamlaka inayoanzishwa, watu na kampuni binafsi zitaruhusiwa kusajili ardhi zao na kuunganishwa na wawekezaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe hotuba yangu hii kwanza kwa kukushukuru sana wewe kwa kunipa fursa ya kuwasilisha muswada huu katika Mkutano huu wa Kumi na Nane na katika Kikao hiki cha Kumi na Tatu cha Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Augustino Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, kwa ushirikiano waliotupatia katika kipindi chote cha kushughulikia muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwashukuru sana Watendaji wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji wakiongozwa

na Katibu Mkuu Dkt. Tausi Kida na Wakuu wa Taasisi za *TIC* na *EPZA* kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kuandaa muswada huu. Vilevile ninamshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao amekuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee ninamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri katika Ofisi yake nikishughulikia sekta hizi za mipango na uwekezaji fursa ambayo amenipa nafasi ya kuanzisha muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI, WAKATI WA KUSOMWA KWA MARA YA PILI KWA "MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI WA MWAKA 2024" BUNGENI, DODOMA, TAREHE 13 FEBRUARI 2025.**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa kuzingatia Kanuni ya 95(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Februari 2023), ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maelezo kuhusu *Muswada wa* ***Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi*** wa Mwaka 2024.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Kama unavyofahamu, Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, pamoja na mambo mengine, iliitaka Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezezaji ili kuvutia wawekezaji kutoka ndani ya nje ya nchi kama nyenzo muhimu ya kukuza uchumi. Kwa kuzingatia maelekezo haya, katika ***Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26)***, wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, uliweka lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na

uwekezaji kama msingi muhimu katika ***kuchochea uchumi shindani na shirikishi.*** Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa **na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** ilipoingia madarakani, pamoja na mambo mengine, ilidhamiria kukuza uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara kama sehemu ya mikakati muhimu ya kuchochea ukuaji wa uchumi nchini.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi kubwa zimeendelea kufanyika katika kutekeleza maelekezo ya Ilani, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, na maelekezo ya Mheshimiwa Rais katika kuendelea kuimarisha mazingiraya biashara na uwekezaji nchini. Kutokana na juhudi hizi, katika kipindi cha miaka minne iliyopita mafaniko mengi yamepatikana. Kwa mfano, idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) iliongeza kutoka miradi 256 mwaka 2021 hadi kufikia miradi 901 mwaka 2024. Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji imeutangaza Mwaka 2024 kama ***mwaka bora zaidi katika sekta ya uwekezaji Tanzania*** kutokana na ukweli kwamba ndio mwaka ambao TIC ilisajili miradi mingi zaidi ya uwekezaji (miradi 901) tangu Tanzania ianzishe kituo hiki na kuanza kurekodi miradi ya uwekezaji mwaka 1996.

Hii inavunja rekodi ya miradi 885 iliyosajiliwa mwaka 2013.

## CHIMBUKO LA MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, mwaka 2023 Serikali ilifanya tathmini ya utendaji kazi wa mashirika na taasisi za umma nchini. Pamoja na mambo mengine, matokeo ya tathmini hii yalionesha kuwa majukumu ya baadhi ya taasisi hizo yanashabihiana na kuingiliana. Hali hii imekuwa ikisababisha mwingiliano wa kiutendaji na kuongeza gharama za uendeshaji na kufanya biashara, na hivyo kuathiri ufanisi uliokusudiwa. Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hii, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunganisha na/au kufuta baadhi ya mashirika na taasisi za umma.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Centre – TIC) na Mamlaka ya Kukuza Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi (Export Processing Zones Authority – EPZA) ni baadhi ya mashirika ya umma ambayo majukumu yake yalibainika kuingiliana na kushabihiana na hivyo kuamuliwa kuunganishwa na kuwa taasisi moja. Hivyo basi, chimbuko la Muswada huu ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya EPZ (EPZA).

## MALENGO YA MUSWADA

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi una malengo ya kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji Tanzania, kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji, kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini, kuweka utaratibu wa uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi, kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania, 2022, kufuta Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, 2002 na kufuta Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji, 2006.

## MAUDHUI YA MUSWADA

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa kama ifuatavyo:

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa kutungwa, maelezo kuhusu matumizi ya Sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka mfumo wa kitaasisi wa uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini. Sehemu hii inaanzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ambayo itakuwa

chombo kikuu cha Serikali cha kuratibu uhamasishaji, uwezeshaji, usimamizi na uendelezaji wa uwekezaji nchini. Sehemu hii pia inaanzisha Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji itakayokuwa na jukumu la msingi la kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri uidhinishaji wa vivutio vya ziada kwa wawekezaji wa kimkakati, kuhakikisha kuwa kuna mazingira mazuri kwa uwekezaji katika sekta binafsi na miradi ya uwekezaji inaendelezwa na kudumishwa, kusimamia miradi mikubwa yenye matokeo makubwa kitaifa kulingana na ukubwa, mtaji, manufaa ya kiteknolojia na ajira, na kuidhinisha uanzishwaji na usimamizi wa maeneo ya uwekezaji wa kimkakati. Aidha, Sehemu hii inaweka masharti na majukuku Bodi, pamoja na masharti ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka na watumishi wengine wa Mamlaka.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uwekezaji. Katika Sehemu hii, masharti yanawekwa kwa ajili ya kuzitaka taasisi za Serikali kushirikiana na Mamlaka katika kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji kupitia Kituo cha Huduma Mahala Pamoja. Vilevile, Sehemu hii inaweka masharti kuhusu mfumo unganishi wa kielektroniki. Mfumo huu unalenga kuunganisha mamlaka muhimu za Serikali zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uwekezaji. Hatua hii itatoa fursa kwa wawekezaji kupata huduma kwa urahisi bila kulazimika kushughulikia vibali au leseni katika taasisi mbalimbali. Aidha, Sehemu hii inaweka masharti kuhusu usajili wa wawekezaji wa ndani na wa kigeni na utoaji wa cheti na leseni ya uwekezaji.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu hii imebainisha vigezo kwa mwekezaji kupewa hadhi ya kuwa mwekezaji wa kimkakati kwa kuzingatia kiwango cha chini cha mtaji kwa mwekezaji wa ndani na mwekezaji wa kigeni. Sehemu hii pia inaweka vigezo kwa mwekezaji anayetaka kubadili au kuacha kuendeleza uwekezaji alioufanya. Aidha, Sehemu hii inabainisha masharti ya kupata vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyotolewa chini ya sheria mbalimbali kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika sheria hizo. Vilevile, ili kutoa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani, sehemu hii inabainisha kuwa Waziri, kwa kushauriana na

Waziri mwenye dhamana ya fedha, anaweza kubainisha maeneo mahsusi ambayo wawekezaji wa ndani wanaweza kupewa vivutio kwa kuzingatia sheria husika.

12. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi inayofaa kwa ajili ya uwekezaji, Muswada unapendekeza kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa benki ya ardhi. Kwa mujibu wa masharti yanayopendekezwa, benki ya ardhi itakuwa ni kanzi data itakayohifadhi taarifa kuhusu ardhi inayopatikana sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya uwekezaji. Mbali na ardhi itakayotengwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji, benki ya ardhi itajumuisha pia ardhi inayomilikiwa na watu binafsi ambao wangependa kukodisha ardhi yao kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nne ya Muswada inaainisha masharti kuhusu uanzishaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi. Maeneo yatakayoanzishwa yanaweza kuwa kongani za viwanda, maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje, maeneo ya biashara huru, maeneo ya bandari huru, maeneo ya kilimo, kongani za utalii, kongani za sayansi na teknolojia, na maeneo mengine kadri Mamlaka itakavyobainisha. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu taratibu za kiforodha katika maeneo maalumu ya kiuchumi, uingizaji na utoaji wa huduma na bidhaa katika maeneo maalumu ya kiuchumi, usimamizi wa maeneo maalumu la kiuchumi, na masuala ya utoaji huduma katika maeneo maalumu ya kiuchumi.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha haki na wajibu wa Serikali na wawekezaji. Muswada unapendekeza kuipa Serikali haki na wajibu wa kusimamia shughuli za uwekezaji ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya sera na sheria za nchi, ikijumuisha maafisa wa Mamlaka kuweza kuingia katika eneo ambako shughuli za uwekezaji zinafanyika kwa madhumuni ya ufuatiliaji. Wajibu unaopendekezwa kwa mwekezaji katika sehemu hii ni pamoja na kutii sheria za nchi, kuendesha shughuli za uwekezaji kwa namna inayolinda walaji, mazingira na kutoa taarifa kwa Mamlaka na taasisi nyingine za Serikali pale zitakapohitajika.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu hii inaainisha pia haki mbalimbali alizonazo mwekezaji katika kipindi cha kutekeleza mradi wa uwekezaji. Haki hizo zinajumuisha kuhamisha nje ya nchi faida, mapato na gawio kupitia benki yoyote baada ya kulipa madeni ya kodi, ada au tozo za Serikali na malipo mengine yaliyowekwa na Sheria. Aidha Sheria inaweka kinga ya kutotaifishwa kwa miradi ya uwekezaji bila fidia stahiki kwa mujibu wa sheria na kupata mikopo katika benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa ndani ya nchi kwa ajili ya kufadhili miradi ya uwekezaji. Sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu wawekezaji wa kigeni kutobaguliwa katika shughuli na fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Pamoja na masharti hayo, Serikali haitazuiliwa kuchukua hatua zozote za ziada kwa ajili ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Sita ya Muswada inaainisha masharti kuhusu ushughulikiaji wa malalamiko na utatuzi wa migogoro. Katika Sehemu hii, inapendekezwa kuwa mwekezaji anaweza kuwasilisha kwa Mamlaka malalamiko kuhusu mwenendo au kitendo cha taasisi yoyote ya Serikali ambacho hakuridhishwa nacho na Mamlaka itakuwa na wajibu wa kufanya jitihada za kushughulikia malalamiko hayo ili kutoathiri shughuli za uwekezaji. Sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wowote uliotolewa na Mamlaka na inaainisha pia utaratibu wa utatuzi wa migogoro baina ya wawekezaji na Mamlaka au Serikali.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Saba ya Muswada inaainisha masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya mapato ya Mamlaka na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu, uandaaji wa bajeti na taarifa ya mwaka. Kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Serikali, Mamlaka itaandaa hesabu na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nane ya Muswada inaainisha masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayohusiana na masuala ya uwekezaji na adhabu zake, utunzaji wa rejesta ya uwekezaji, matumizi ya sheria nyingine

pamoja na mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria inayopendekezwa. Aidha, Sehemu hii pia inapendekeza kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022, Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya mwaka 2002 na Sheria ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2006, pamoja na kutambua masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na Sheria zinazopendekezwa kufutwa.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tisa ya Muswada inajumuisha marekebisho ya Sheria mbalimbali ili kuendana na masharti yanayopendekezwa katika Sheria itakayotungwa. Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia wa Kigeni, Sura ya 436, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 na Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapomalizia ninaomba kusisitiza mambo matatu ambayo kwa kiasi kikubwa ni mapya katika Muswada huu. Mosi, ni kuanzishwa kwa mamlaka mpya itakayochukua nafasi ya TIC na EPZA (ibara ya 4). Mamlaka hii itaitwa ***Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority – TISEZA).*** Pili, Muswada huu unapendekeza kuwepo kwa fursa na vivutio mahususi kwa wawekezaji wa ndani pekee (ibara ya 22). Tatu, Muswada unapendekeza kuanzishwa kwa Benki ya Ardhi (Kifungu cha 23). Kupitia benki hii, mbali na ardhi itakayotengwa na Mamlaka inayoanzishwa, watu na makampuni binafsi yataruhusiwa kusajili ardhi zao na kuunganishwa na wawekezaji mbalimbali.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Muswada huu katika Mkutano huu wa Kumi na Nane (katika Kikao cha Kumi na Tatu) wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Augustino Vuma Hole (Mbunge wa Kasulu Vijijini), na Makamu Mwenyekiti

wa Kamati, Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mbunge wa Viti Maalumu), kwa ushirikiano waliotupatia katika kipindi chote cha kushughulikia Muswada huu.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.),**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI.**
**Alhamisi, 13 Februari 2025.**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono ahsante. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati. Mwenyekiti au mwakilishi wake?

**MHE. VUMA A. HOLLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya kiuchumi wa mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 8 Novemba, 2024 kwa mujibu wa kifungu cha 97(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Baada ya hatua hiyo, uliletwa kwenye Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo

inahusu masharti ya muswada uliosomwa mara ya kwanza kupelekwa kwenye Kamati na inataka Kamati iliyopelekewa muswada kuanza kujadili mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia misingi ya Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayoitaka Kamati iliyopelekewa muswada kuanza kujadili mapema iwezekanavyo, Kamati ilianza kushughulikia muswada huu katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 15 hadi 24 Januari, 2025 na tarehe 7 na 10 Februari, 2025. Kamati ilitekeleza jukumu lake kiukamilifu kwa lengo la kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali ipasavyo katika kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mpangilio uliofafanuliwa katika Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, juu ya uandishi wa taarifa za Bunge. Aidha, taarifa hii imelenga kulijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi muswada huu, matokeo ya uchambuzi ambayo yanajumuisha maoni na ushauri kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu njia na mbinu zilizotumika, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti na ustahiki ninaomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia zilizotumika kuufanyia kazi muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya taarifa hii. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo: -

(a) Kufanya mapitio ya maudhui ya muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa katika uendelezaji na uimarishaji wa uwekezaji Tanzania kwa lengo la kutathmini kufaa au kutokufaa kwa sheria inayopendekezwa;

(b) Kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Alexander Kitila Mkumbo, Mbunge, siku ya tarehe 7 Februari, 2025;

(c) Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* uliofanyika tarehe 15 Januari, 2024, lengo likiwa ni kupata mawazo ya jamii tunayoiwakilisha hapa Bungeni. Pia kutimiza masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru kwa dhati wadau waliofanikiwa kuwasilisha maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yametoa picha na kusaidia kujua matarajio ya wananchi na kuongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya muswada huu. Kuchambua maoni ya wadau na baadae kufanya majumuisho na Serikali, ambavyo vilifanyika tarehe 10 Februari, 2025.

Katika majumuisho haya, Waziri pamoja na timu yake walifanya majadiliano na Kamati juu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Ibara mbalimbali za muswada kwa lengo la kupata ufafanuzi katika Ibara hizo na mwisho kupata msimamo wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mbinu zilizotumika; ili kuweza kulisaidia Bunge lako Tukufu kutunga sheria yenye manufaa na inayozingatia maslahi ya sekta hii, kwa lengo la kuuelewa muswada huu, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo: -

(a) Kubaini mambo mapya kabisa yanayoletwa na muswada huu katika kuendeleza uwekezaji nchini;

(b) Kuangalia uzoefu wa nchi nyingine ambazo zinatumia utaratibu unaopendekezwa katika muswada huu katika uendelezaji na uimarishaji wa uwekezaji; na

(c) Kuoanisha nia na mambo yanayopendekezwa kutungwa kwa sheria hii pamoja na sera za nchi na ahadi iliyotolewa kwa wananchi katika Ilani ya Chama kilichopo madarakani ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa ambazo zimetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi matarajio ya wananchi katika utungaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa muswada; muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa zenye jumla ya Ibara 68 ambapo unapendekeza kutungwa kwa Sheria Mpya ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2024. Lengo la sheria inayopendekezwa kutungwa ni kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu wa shughuli za uwekezaji nchini na uwezeshaji wa uwekezaji kwa wawekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi na maeneo mengine yanayotamkwa na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, taarifa hii inabainisha uchambuzi katika sehemu kuu tisa; sehemu hizo ni Masharti ya Utangulizi, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania, Uwezeshaji wa Uwekezaji, Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Haki na Wajibu, Utatuzi wa Migogoro, Masharti ya Fedha na Masharti mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilipata ufafanuzi kuhusu Maudhui ya Muswada wa Sheria na Uchambuzi wa Ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vya sheria inayotungwa. Mtiririko huo unaweza kulisaidia Bunge kufanya uamuzi unaotokana na tatizo au ombwe la sheria inayopendekezwa, unaotatua au kuziba ombwe ipasavyo na unaozingatia misingi ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya muswada huu na kubaini kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kutungwa inalenga kuweka mfumo wa

kitaasisi wa uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini na kuimarisha masharti ya uwekezaji nchini, kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZA)*. Vilevile sheria inayopendekezwa inalenga kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya miongozo; Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji Tanzania inatoa miongozo na mwelekeo juu ya jinsi ya kuhamasisha na kuimarisha uwekezaji katika sekta binafsi ili iweze kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Sera inasisitiza kuhusu umuhimu wa sekta binafsi kuimarishwa na kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuweka vivutio ili iweze kuwa *engine* ya ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji wa kimkakati na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatarajiwa kuwa sheria hii itakuwa nyenzo ya kutekeleza sera kwa kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa sehemu salama, yenye kuvutia na endelevu kwa uwekezaji wa ndani na wa kimataifa. Sheria inayotungwa inalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji, kukuza ushirikiano wa sekta binafsi na umma, kuimarisha ushiriki wa wawekezaji wa ndani, kuweka misingi ya vivutio mbalimbali vikiwemo vya kikodi, kukuza maeneo maalumu ya kiuchumi, kuweka misingi ya maendeleo endelevu kwa kufanya uwekezaji unaozingatia hifadhi ya mazingira na kuwekeza katika miradi inayoongeza thamani kwa jamii na kulinda rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ilani ya chama kinachoongoza Serikali, kwa kurejea ilani ya chama kinachoongoza Serikali kwa sasa ambacho ni Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kamati ilichambua muswada huu kwa muktadha wa kuangaalia ahadi walizopewa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kuhusiana na mipango ya Serikali juu ya kuimarisha uwekezaji katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya wananchi yanazingatiwa katika muswada huu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba chama

kinachoiongoza Serikali kwa sasa kiliwaahidi wananchi kuweka mazingira wezeshi katika sekta binafsi kukua na kustawi pamoja na kuvutia wawekezaji, kujenga na kukuza uchumi shindani, hususani kupitia sekta za viwanda na huduma za kiuchumi. Kuimarisha miundombinu ya kimkakati ili kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija na kutenga maeneo maalumu ya akiba ya ardhi na uwekezaji ili kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa sheria hii kunadhamiria kuweka masharti bora ya uendelezaji wa uwekezaji, mazingira bora ya uwekezaji, mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini. Kuweka utaratibu wa uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi, hivyo basi, madhumuni ya sheria hii yameendana na ahadi waliyopewa wananchi, kama inavyotolewa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, katika Ibara ya 9(B)(i), (ii), (iii) na (vii).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzoefu wa nchi nyingine; Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za nchi saba ambazo zinatumia mfumo huu katika kukuza na kuendeleza uwekezaji katika sekta binafsi kwa nchi hizo ili kuweza kujifunza kutoka kwao na kupata uelewa zaidi juu ya muswada unaopendekezwa. Miongoni mwa nchi zilizoonekana kutumia mfumo huu na kufanya vyema katika muktadha huo ni pamoja na Rwanda, Kenya, Ghana, Singapore, Mauritius, Afrika Kusini na Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyingine kuhusiana na muswada huu, Kamati ililenga kujifunza mambo makuu manne kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni hoja ya uanzishaji wa mamlaka zenye majukumu ya kuimarisha, kuratibu na kusimamia uwekezaji katika sekta binafsi na malengo yake. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa nchi hizi zilianzisha mamlaka ya aina hii kwa lengo la kuunganisha taasisi mbalimbali zinazoshughulikia maendeleo ya kiuchumi na uwekezaji ili kupunguza urasimu na kurahisisha huduma kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili ni vivutio vya uwekezaji hususani msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni. Uchambuzi wa Kamati umebaini vivutio mbalimbali vinavyotolewa na nchi ilizofuatilia uzoefu wake na ilijikita katika gharama za uwekezaji na vivutio vya kikodi ambapo gharama ya uwekezaji kwa nchi zilizochambuliwa ni kuanzia dola 500,000 mpaka dola milioni 50. Msamaha wa kodi ya mapato kuanzia miaka mitano mpaka miaka kumi na msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inayopendekezwa ni muhimu kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutungwa kwa sheria hii kutawezesha: -

(a) Kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji Tanzania;

(b) Kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji;

(c) Kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini; na

(d) Kuweka utaratibu wa uanzishaji uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu ni vema Serikali ikapitia vivutio vilivyowekwa na nchi nyingine kwa lengo la kuiwezesha kuweka vivutio shindani vitakavyoleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu ibara za muswada; uchambuzi huu unahusu maeneo ambayo Kamati iliona haja ya kufanya marekebisho, kwa ajili ya kuboresha muswada. Wakati wa kufanya uchambuzi Kamati ilibaini mambo mbalimbali, baadhi ya mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni sehemu ya kwanza ya muswada; sehemu hii ina jumla ya ibara tatu; inapendekeza jina la sheria inayokusudiwa kutungwa, aina za wawekezaji, shughuli

ambazo sheria hii inazishughulikia pamoja na mipaka (wigo) yake na fasili za misamiati mbalimbali iliyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitoa maoni ya kufanya marekebisho katika Ibara ya 1 kwa kurekebisha Jina Refu la Muswada. Kamati ilipendekeza Jina Refu la Muswada lisomeke, "Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji wa Uwekezaji na Mazingira Bora kwa Wawekezaji Tanzania, Uendelezaji na Usimamizi wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania, 2022, Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, 2002, Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji, 2006 na Masuala Yanayohusiana na hayo."

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo yamekubaliwa na Serikali. Serikali inakubaliana na mapendekezo ya kufanya maboresho ya kiuandishi kwenye jina refu la muswada. Hata hivyo, Serikali ilipendekeza maudhui kuhusu mfumo wa kitaasisi, kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini yaendelee kubaki ili kulifanya jina refu liendelee kuakisi mfumo wa kitaasisi unaoonzishwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na kufanya marekebisho kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu sehemu ya pili ya muswada; sehemu hii inajumuisha ibara nane, ambazo zinaanzia Ibara ya 4 hadi ya 11 ambazo zinahusu uwekezaji na maeneo maalumu ya kiuchumi Tanzania. Katika sehemu hii Kamati ilifanya marekebisho katika Ibara ya 7(3) na kuongeza aya mpya, hii kuhusu jukumu la kuidhinisha uanzishwaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kimkakati ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, Serikali ilipendekeza ibara hii ifanyiwe maboresho kuipa Kamati jukumu la kuidhinisha uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya uwekezaji wa kimkakati. Muafaka ulifikiwa na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya tatu ya muswada. sehemu hii ina jumla ya ibara 13 na inaanzia Ibara ya 12 mpaka ya 24 ambayo kiujumla inafafanua kuhusu "Uwezeshaji wa Uwekezaji." Sehemu hii inahusisha kuanzisha kituo cha huduma mahala pamoja ambapo taasisi zote za Serikali zitashirikiana kikamilifu na mamlaka katika utekelezaji wa majukumu ya kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi katika ibara hizi na kuja na mapendekezo ya kuboresha Ibara ya 18 inayohusu kubadili au kuacha uwekezaji. Kamati ilishauri kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka kosa na adhabu kwa kiwango cha chini na juu kwa mwekezaji ambaye atakiuka kuitaarifu mamlaka kuwa amebadili au kuacha uwekezaji. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na marekebisho yamefanyika kama inavyoonekana katika Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya nne ya muswada; sehemu hii inaanzia Ibara ya 6, kuanzia Ibara ya 25 hadi Ibara ya 30 na inaweka masharti kuhusu Maeneo Maalumu ya Kiuchumi. Katika uchambuzi wa ibara hizi, Kamati iliomba kupata ufafanuzi wa Ibara ya 27 inayohusu masuala ya forodha katika eneo maalumu la kiuchumi na ni ipi mipaka ya utendaji kazi kati ya Mamlaka ya Forodha na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ili ifahamike mipaka ya utendaji kazi kati ya mamlaka hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa ufafanuzi kuwa baada ya eneo kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi, liko chini ya mamlaka. Hata hivyo, kwa madhumuni ya forodha kuhusu masuala ya usimamizi wa kodi, eneo hilo litadhibitiwa na Mamlaka ya Forodha. Kamishna Mkuu wa *TRA* ataweka utaratibu wa usimamizi wa kodi katika eneo husika kama ilivyo sasa. Baada ya majadiliano, Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya tano ya muswada; sehemu hii inahusu haki...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye maoni na mapendekezo.

**MHE. VUMA A. HOLLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati; kutokana na uchambuzi wa madhumuni, maudhui na masharti mbalimbali katika muswada huu, Kamati ina maoni ya jumla na mapendekezo mahsusi ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa sheria hii kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni ya jumla; Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maamuzi ya kuunganisha baadhi ya taasisi zake ambazo majukumu yake, kwa namna moja au nyingine, yanafanana. Uamuzi huu utakwenda kuongeza ufanisi na kuipunguzia mzigo wa ruzuku. Serikali ilitangaza kuunganisha jumla ya taasisi na mashirika 19, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee na mchakato wa kuunganisha mashirika hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi, tija na kupunguza mzigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na mapendekezo mahususi; pamoja na uchambuzi na marekebisho ya ibara mbalimbali za muswada huu, Kamati inaisisitiza Serikali katika mambo muhimu yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuweka vivutio vya kiushindani. Sheria inaelekeza kuandaliwa kwa orodha ya vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji na kuvitangaza. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inazingatia kuwa vivutio vinavyotolewa vinakidhi hali ya ushindani ili sheria inayotungwa iweze kuwa yenye ufanisi na tija hususani katika kuvutia mtaji kutoka nje ya nchi *(FDI)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uwezeshaji wazawa; Ibara ya 22 ya sheria inayotungwa inaeleza kuwa Waziri kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha anaweza kubainisha maeneo mahususi ambayo wawekezaji wa ndani wanaweza kupewa vivutio kwa kuzingatia sheria husika. Kamati inashauri kwamba Serikali iandae namna bora itakayowawezesha

wawekezaji wazawa kushiriki kikamilifu katika uwekezaji ili kukuza mitaji yao na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kuhusu Benki ya Ardhi; sheria imeainisha kuwa Benki ya Ardhi itakayokuwa chini ya mamlaka itahusisha ardhi za watu binafsi na kuwa ardhi ya mtu binafsi itakayoingizwa katika Benki ya Ardhi inaendelea kubaki kuwa mali ya mtu husika hadi atakapopatikana mwekezaji ambaye ndiye atawajibika kulipa fidia kwa mmiliki. Kamati inaishauri mamlaka isimamie mchakato mzima wa utoaji wa ardhi ya mtu binafsi kwenda kwa mwekezaji na utaratibu mzima wa ulipaji fidia, ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya ardhi hiyo, ili mmiliki aweze kupata fidia stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni Kuhusu watoa huduma katika maeneo maalumu ya kiuchumi; sheria inatoa wajibu kwa watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi kuomba kibali kwa mamlaka. Kamati inashauri, Serikali izingatie kuwa kanuni zitakazotungwa kuhusu utaratibu wa kuomba kibali cha kutoa huduma ndani ya eneo maalumu la kiuchumi zibainishe makosa na adhabu kwa viwango vya chini na juu ili kuongeza utii wa sheria kwa watakokiuka masharti ya kuwa na leseni ya kutoa huduma katika maeneo maalumu la kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwa fursa aliyonipa kuwasilisha maoni haya. Napenda kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Alexander Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge na watendaji wote wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa uchambuzi wa muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Kwa heshima na taadhima naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza jukumu la kuchambua muswada huu kwa ukamilifu mpaka leo hii ninapoisoma taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa mwaka 2024, pamoja marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UWEKZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI WA MWAKA 2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya kiuchumi wa Mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza tarehe 08 Novemba, 2024 kwa mujibu wa Kifungu cha 97 (1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Baada ya hatua hiyo, uliletwa kwenye Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo

inahusu masharti ya Muswada uliosomwa Mara ya Kwanza kupelekwa kwenye Kamati na inataka Kamati iliyopelekewa Muswada kuanza kujadili mapema iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia misingi ya Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayoitaka kamati iliyopelekewa Muswada kuanza kujadili mapema iwezekanavyo, Kamati ilianza kushughulikia Muswada huu katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 06 hadi 24 Januari, 2025 na tarehe 07 na 10 Februari, 2025. Kamati ilitekeleza jukumu lake kiukamilifu kwa lengo la kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali ipasavyo ipasavyo katika kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imeandaliwa kwa kuzingatia muongozo wa mpangilio uliofafanuliwa katika Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, juu ya uandishi wa taarifa. Aidha, taarifa hii imelenga kulijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu, matokeo ya uchambuzi ambayo yanajumuisha maoni na ushauri kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi.

**1.2 Njia na Mbinu zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (reliability) na ustahiki (validity), naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu.

**1.2.1 Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, njia zilizotumika kufanyia kazi Muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya Taarifa hii. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo: -

(a) Kufanya mapitio ya Maudhui ya Muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa katika Uendelezaji na Uimarishaji wa Uwekezaji Tanzania kwa lengo la kutathmini kufaa au kutokufaa kwa Sheria inayopendekezwa;

(b) Kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Alexander Kitila Mkumbo (Mb) siku ya tarehe 7 Februari, 2025;

(c) Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau (Public Hearing) uliofanyika tarehe 15 Januari, 2024, lengo likiwa ni kupata mawazo ya jamii tunayoiwakilisha hapa Bungeni lakini pia kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inamshukuru kwa dhati wadau waliofanikiwa kuwasilisha maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yametoa picha na kusaidia kujua matarajio ya wananchi na kuongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

(a) Kuchambua maoni ya wadau, na baadae kufanya majumuisho na Serikali ambavyo vilifanyika tarehe 10 Februari, 2025. Katika majumuisho haya, Waziri pamoja na timu yake ilifanya majadiliano na Kamati juu ya mapendekezo ya marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada kwa lengo la kupata ufafanuzi katika Ibara hizo na mwisho kupata msimamo wa pamoja.

**1.2.2 Mbinu zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kulisaidia Bunge lako tukufu kutunga Sheria yenye manufaa na inayozingatia maslahi ya sekta hii, kwa lengo la kuuelewa Muswada huu Kamati ilitumia mbinu zifuatazo:-

(a) Kubaini mambo mapya kabisa yanayoletwa na
(b) muswada huu katika kuendeleza uwekezaji nchini;
(c) Kuangalia uzoefu wa Nchi nyingine ambazo zinatumia utaratibu unaopendekezwa katika muswada huu katika uendelezaji na uimarishaji wa uwekezaji; na
(d) Kuoanisha nia, mambo yanayopendekezwa kutungwa kwa Sheria hii pamoja na Sera za nchi na ahadi iliyotolewa kwa

wananchi katika Ilani ya Chama Kilichopo madarakani ya Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa, ambazo zimetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi matarajio ya wananchi katika utungaji wa Sheria inayopendekezwa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa (9) zenye jumla ya Ibara Sitini na Nane (68), ambapo unapendekeza kutungwa kwa Sheria Mpya ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2024 kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa Kitaasisi kwa ajili ya uratibu wa shughuli za uwekezaji nchini na uwezeshaji wa uwekezaji kwa wawekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi na maeneo mengine yaliyotamkwa na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika sehemu kuu Tisa. Sehemu hizo ni: Masharti ya Utangulizi, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania, Uwezeshaji wa Uwekezaji, Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Haki na Wajibu, Utatuzi wa Migogoro, Masharti ya fedha na Masharti mengineyo. Aidha, Kamati ilipata ufafanuzi kuhusu maudhui ya Muswada wa Sheria na Uchambuzi wa Ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vya Sheria inayotungwa. Mtiririko huo unaweza kulisaidia Bunge kufanya uamuzi unaotokana na tatizo au ombwe la sheria inayopendekezwa, unaotatua au kuziba ombwe ipasavyo na unaozingatia misingi ya utungaji wa sheria.

### 2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada (thematic review)

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya kupembua maudhui ya Muswada huu ni kubaini uthabiti wa utungaji wa Sheria inayopendekezwa ili kulishauri Bunge ipasavyo. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu na kubaini kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kutungwa inalenga kuweka Mfumo wa kitaasisi wa uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini na kuimarisha masharti ya uwekezaji nchini, kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya nje ya nchi. Vile vile, Sheria inayopendekezwa inalenga kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wawekezaji.

### 2.3 Mapitio ya Miongozo

#### 2.3.1 Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya kuhamasisha Uwekezaji Tanzania inatoa miongozo na mwelekeo juu ya jinsi ya kuhamasisha na kuimarisha uwekezaji katika sekta binafsi ili iweze kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Sera inasisitiza kuhusu umuhimu wa sekta binafsi kuimarishwa kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuweka vivutio ili iweze kuwa injini ya ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji wa kimkakati na endelevu. Inatarajiwa kuwa Sheria hii itakuwa nyenzo ya kutekeleza sera kwa kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa sehemu salama, yenye kuvutia, na endelevu kwa uwekezaji wa ndani na wa kimataifa. Sheria inalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji, kukuza ushirikiano wa sekta binafsi na umma, kuimarisha ushiriki wa wawekezaji wa ndani, kuweka misingi ya vivutio mbalimbali vikiwemo vya kikodi, kukuza maeneo maalumu ya kiuchumi na kuweka misingi ya maendeleo endelevu kwa kufanya uwekezaji unaozingatia hifadhi ya mazingira na kuwekeza katika miradi inayoongeza thamani kwa jamii na kulinda rasilimali za taifa.

### 2.3.2 Ilani ya Chama kinachoongoza Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa kurejea Ilani ya chama kinachoongoza Serikali kwa sasa ambacho ni Chama cha Mapinduzi (CCM), Kamati ilichambua Muswada huu kwa muktadha wa kuangaalia ahadi walizopewa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kuhusiana na Mipango ya Serikali kuhusu kuimarisha Uwekezaji katika sekta binafsi. Lengo la kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya Wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Kamati ilibaini kwamba, Chama kinachoongoza Serikali kwa sasa kiliwaahidi wananchi kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kustawi pamoja na kuvutia wawekezaji, kujenga na kukuza uchumi shindani hususan kupitia sekta za viwanda na huduma za kiuchumi, kuimarisha miundombinu ya kimkakati ili kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija na kutenga maeneo maalum ya akiba ya ardhi na uwekezaji ili kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani.

**Mheshimiwa Spika**, Kutungwa kwa Sheria hii kunadhamiria kuweka masharti bora ya uendelezaji wa uwekezaji, mazingira bora kwa wawekezaji, mfumo wa kitaasisi kwaajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini, na kuweka utaratibu wa uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi. Hivyo basi, madhumuni ya Sheria hii yameendana na ahadi waliyopewa wananchi kama inavyotolewa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 katika Ibara ya 9(B) (i), (ii), (iii) na (vii).

### 2.4 Uzoefu wa Nchi zingine

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za nchi saba (7) ambazo zinatumia mfumo huu katika kukuza na kuendeleza Uwekezaji katika sekta binafsi kwa nchi hizo ili kuweza kujifunza kutoka kwao na kupata uelewa zaidi juu ya muswada unaopendekezwa. Miongoni mwa nchi zilizoonekana kutumia mfumo huu na kufanya vyema katika muktadha huo ni pamoja na Rwanda, Kenya, Ghana, Singapore, Mauritius, Afrika Kusini na Ethiopia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyingine kuhusiana na muswada huu, Kamati ililenga kujifunza mambo makuu manne kama ifuatavyo: -

i) Uanzishaji wa Mamlaka zenye majukumu ya Kuimarisha,
ii) Kuratibu na Kusimamia Uwekezaji (katika sekta binafsi);
iii) Malengo ya uanzishwaji wa Mamlaka hizo
iv) Vivutio vya uwekezaji hususani Msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni kwa miaka 10 ya mwanzo; na
v) Jinsi Mamlaka inavyoendeshwa na kutekeleza majukumu yake.

### 2.4.1 Nchi ya Rwanda

**Mheshimiwa Spika,** nchi ya Rwanda ilianzisha Mamlaka ya Rwanda Development Board (RDB) mwaka 2008 kupitia Sheria ya RDB, kwa lengo la kuunganisha taasisi mbalimbali zinazoshughulikia maendeleo ya kiuchumi na uwekezaji. Lengo kuu lilikuwa kupunguza urasimu na kurahisisha huduma kwa wawekezaji. Mamlaka hiyo inaratibiwa na Serikali ya Rwanda kupitia Ofisi ya Rais. Mamlaka hiyo huongozwa na Bodi chini ya Mwenyekiti wa Bodi ambaye huteuliwa na Rais wa nchi hiyo. Pia huwa na Mtendaji Mkuu ambaye hujulikana kama Mkurugenzi Mtendaji ambaye huteuliwa pia na Rais na huwajibika moja kwa moja kwa bodi. Bodi hujumuisha wawakilishi kutoka sekta ya umma na binafsi, ikiwemo mawaziri wa wizara muhimu kama Biashara na Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka hii hutekeleza kazi zake kwa kuunganisha shughuli zote zinazohusiana na uwekezaji, biashara, na maendeleo ya kiuchumi. Hutoa huduma za "one-stop-center" kwa wawekezaji, ikiwa ni pamoja na usajili wa biashara, utoaji wa vibali, na uratibu wa miradi ya uwekezaji.  Vilevile, Wawekezaji wenye miradi mikubwa (zaidi ya USD 50 milioni) wanaweza kufurahia msamaha wa kodi kwa muda wa miaka 7. Na msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kipindi cha miaka 5 kwa uingizaji wa mitambo, vifaa vya uzalishaji, na malighafi ya viwanda una msamaha wa VAT, ili kupunguza gharama za uwekezaji.

### 2.4.2 Nchi ya Kenya

**Mheshimiwa Spika**, Kenya ilianzisha mamlaka ya Kenya Investment Authority (KenInvest) mwaka 2004 kupitia Sheria ya Uwekezaji ya Kenya, kwa lengo la kuvutia na kuwezesha uwekezaji wa ndani na wa kigeni, na kurahisisha taratibu za uwekezaji. Mamlaka hii huongozwa na Bodi chini ya Mwenyekiti wa Bodi ambaye huteuliwa na Rais, pia shughuli za kiutendaji za kila siku husimamiwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye huteuliwa na Waziri wa Biashara. Kwa ujumla, Bodi ya Wakurugenzi husimamia sera na maamuzi ya kimkakati na wajumbe wa bodi hii hujumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na binafsi. Mamlaka hii Kenya huratibu uwekezaji wa ndani na wa kigeni kwa kutoa mwongozo kwa wawekezaji, kusaidia upatikanaji wa vibali, na kuendeleza miradi ya maendeleo ya kiuchumi..

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Uwekezaji ya Kenya (KenInvest) imeweka Kiwango cha uwekezaji kuanzia USD mill 10 hadi USD Mill 50 kulingana na aina ya uwekezaji. Vivutio vya kikodi vinavyotolewa kwa maeneo maalumu ya kiuwekezaji ni Msamaha kamili wa kodi ya mapato kwa miaka 10 ya kwanza, na Miaka 25 inayofuata Kodi ya mapato hupunguzwa hadi kiwango cha asilimia 25. Aidha inatoa Msamaha wa kodi ya zuio (withholding tax) kwenye gawio, riba, na ada ya huduma kwa miaka 10 ya kwanza. Kwa miradi ya kimakati wawekezaji hupata msamaha wa kodi ya mapato kwa kipindi kinachoanzia miaka 5 hadi 10, kulingana na athari za mradi kwa uchumi, ajira, na miundombinu.

### 2.4.3 Nchi ya Ghana

**Mheshimiwa Spika**, Ghana ilianzisha mamlaka ya Ghana Investment Promotion Centre (GIPC) mwaka 1994 chini ya Sheria ya Uwekezaji ya Ghana ili kusimamia, kuvutia na kuwezesha uwekezaji wa ndani na wa kigeni nchini humo. Mamlaka hiyo huongozwa na Bodi ya Wakurugenzi ikiwa na wawakilishi kutoka sekta za umma na binafsi, na mwenyekiti huteuliwa na Rais. Vilevile, shughuli za kiutendaji husimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye pia huteuliwa na Rais wa nchi hiyo, kwa

kushauriana na Waziri wa Biashara na Viwanda. Mamlaka hii huwa na majukumu ya kusimamia uwekezaji katika nchi hiyo kwa kuvutia na kuwezesha uwekezaji wa ndani na wa kigeni, kutoa usaidizi wa kitaalamu kwa wawekezaji, ikiwemo maelezo kuhusu sera za uwekezaji na mwongozo wa kupata vibali.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji ya Ghana (Ghana Investment Promotion Centre - GIPC) inahitaji Kiwango cha chini cha uwekezaji kwa miradi ya kimkakati kawaida ni **USD 50 milioni** au zaidi, kulingana na athari za mradi kwa uchumi wa Ghana, kwa miradi ya kawaida Kiwango cha chini ni **USD** 500,000**.** Mamlaka hutoa vivutio vya msamaha wa kikodi kwa kutegemea sekta, eneo la uwekezaji, na aina ya mradi. Hapa kuna muhtasari wa msamaha wa kikodi unaotolewa. Mfano maeneo ya miji msamaha wa kodi unaweza kuwepo au kutokuwepo kabisa, kwa maeneo nje ya miji Kodi ya mapato hupunguzwa au kusamehewa kabisa kwa kipindi cha kati ya 5 hadi 10 miaka, kulingana na eneo la uwekezaji. Wawekezaji wanaruhusiwa kuagiza mitambo, vifaa vya uzalishaji, na malighafi kwa ajili ya miradi yao bila kulipa ushuru wa forodha. Kwa maeneo maalumu ya kiuchumi Msamaha wa kodi ya mapato kwa miaka 10 ya kwanza. Baada ya miaka 10, kodi ya mapato inapunguzwa hadi kiwango cha **15%** badala ya 25%.

### 2.4.4 Nchi ya Singapore

**Mheshimiwa Spika,** Singapore ilianzisha shirika la Economic Development Board (EDB – Singapore) mwaka 1961 kupitia Sheria ya EDB, kwa lengo la kukuza uchumi wa Singapore kupitia uwekezaji wa kimkakati. Shirika hili huongozwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo hujumuisha wataalamu kutoka sekta za biashara, viwanda, na teknolojia chini ya Mwenyekiti wa Bodi ambaye huteuliwa na Waziri wa Biashara na Viwanda wa nchi hiyo. Vilevile, utekelezaji wa mikakati ya uwekezaji huongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu ambaye huteuliwa na Bodi.

**Mheshimiwa Spika**, shirika hili la serikali hushirikiana na wawekezaji binafsi kukuza uchumi wa Singapore kwa kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati katika sekta mbalimbali kama teknolojia, fedha, na

utengenezaji. Vilevile, EDB – Singapore hushirikiana na sekta binafsi katika utafiti na maendeleo.

**2.5 Umuhimu wa Sheria Inayopendekezwa**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria inayopendekezwa ni muhimu kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutungwa kwa Sheria hii kutawezesha: -

(i) Kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji Tanzania;
(ii) Kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji;
(iii) Kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini; na
(iv) Kuweka utaratibu wa uanzishaji uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi.

**2.6 Uchambuzi Kuhusu Ibara za Muswada**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu unahusu maeneo ambayo Kamati imeona haja ya kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha Muswada. Wakati wa kufanya uchambuzi, Kamati ilibaini mambo mbalimbali. Baadhi ya mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

**2.6.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ina jumla ya Ibara tatu (3), ambayo inapendekeza jina la Sheria inayokusudiwa kutungwa, aina za wawekezaji na shughuli ambazo Sheria hii inazishughulikia pamoja na mipaka (wigo) yake na fasili za misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa maoni ya kufanya marekebisho katika Ibara ya 1 kwa kurekebisha Jina refu la Muswada, Kamati milipendekeza jina refu la Muswada lisomeke "Sheria ya kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji na mazingira bora kwa wawekezaji Tanzania, uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi, kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania, 2022, Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, 2002,

Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji, 2006 na masuala yanayohusiana na hayo".

Mapendekezo hayo yamekubaliwa na Serikali, Serikali inakubaliana na mapendekezo ya kufanya maboresho ya kiuandishi kwenye jina refu la Muswada. Hata hivyo, Serikali ilipendekeza maudhui kuhusu "mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini" yaendelee kubaki ili kulifanya jina refu liendelee kuakisi mfumo wa kitaasisi unaonzishwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na kufanya marekebisho kama inavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho la Serikali.

**2.6.2 Sehemu ya Pili ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ina jumla ya Ibara nane (8) ambayo inaanzia Ibara ya 4 hadi ya 11, ambayo inahusu "Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania" ambayo kwa ujumla inafafanua juu ya uanzishaji Mamlaka, malengo na majukumu ya Mamlaka, uanzishaji wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji, uundwaji wa bodi ya Mamlaka na majukumu ya bodi hiyo, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka na upatikanaji na usimamizi wa watumishi wa Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika**, katika sehemu hii Kamati ilitoa maoni katika **Ibara ya 4** kwa kupendekeza Serikali kufanya marekebisho kwa kuweka sharti la namna gani Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambae ndio mwenye haki ya kusimamia mashauri yote ya serikali ataingia kusimamia mashauri ya Mamlaka wakati wowote. Lengo la marekebisho haya ni kuweza kuendana na matakwa ya Kifungu 6A cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali.

kwamba kati ya wajumbe wanne (4) watakaoteuliwa na Waziri wajumbe wasiopungua wawili watoke katika Sekta binafsi. Lengo la maboresho haya ni kupata mchanganyiko mzuri katika bodi ya mamlaka ambao utaboresha utendaji kwa kuleta uzoefu kutoka katika sekta binafsi. Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho. Hata hivyo, baada ya majadiliano Serikali ilipendekeza kifungu hiki

kibaki kama kilivyo kwenye muswada kwa kuwa Masharti ya Kifungu 6A cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali ambacho kimetoa fursa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia shauri lolote lililofunguliwa dhidi ya Serikali yanajitosheleza. Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya marekebisho katika Ibara ya 7(3) kwa kuongeza aya mpya (e) kuhusu jukumu la kuidhinisha uanzishwaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi ya kimkakati. Baada ya majadilioano Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati, hata hivyo Serikali ilipendekeza ibara hii iifanyiwe maboresho kuipa Kamati jukumu la kuidhinisha uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya uwekezaji wa kimkakati. Muafaka ulifikiwa na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Serikali.

**2.6.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ina jumla ya Ibara 13 na inaanzia Ibara ya 12 hadi ya 24, ambayo kiujumla inafafanua kuhusu "Uwezeshaji wa Uwekezaji". Sehemu hii inahusisha kuanzisha Kituo cha Huduma Mahala Pamoja ambapo taasisi zote za Serikali zitashirikiana kikamilifu na Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu ya kituo hiki, huduma zinazotolewa nje ya Kituo cha Huduma Mahala pamoja, mfumo unganishi wa kielektroniki kwa ajili ya uwezeshaji wa uwekezaji, sharti la usajili kwa wawekezaji wote wanaokusudia kufanya uwekezaji wowote Tanzania. Sehemu hii imefafanua pia kuhusu utaratibu utakaofuatwa endapo mwekezaji atataka kubadili au kuacha Uwekezaji, vivutio vya uwekezaji ambavyo wawekezaji wanaweza kupata nchini Tanzania, inafafanua mwekezaji wa kimkakati na fursa maalumu za mwekezaji wa ndani, kuanzishwa kwa benki ya ardhi na wajibu wa Mamlaka kusimamia ardhi ya uwekezaji. Kamati ilifanya uchambuzi katika ibara hizi na kuja na mapendekezo yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza katika **Ibara ya 12** (Kituo cha Huduma Mahala Pamoja) iboreshwe kwa kubainishe muda wa kufanyia kazi maombi ya mwekezaji ambapo inapendekezwa kuwa muda wa kufanyia kazi maombi hayo uwe

ni siku saba (7). Lengo la mapendekezo haya ni kuwekwa takwa la muda wa kufanyia kazi maombi ya mwekezaji. Baada ya majadiliano ya kina kuhusu Ibara hii Serikali ilipendekeza kuwa masharti ya ibara hii yabaki kama yalivyo kwa kuwa afisa anayehudumia wawekezaji katika Kituo cha Huduma Mahala Pamoja anasimamiwa na sheria na taratibu zinazosimamia majukumu yake. Hata hivyo, Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali zinazohudumia wawekezaji kwenye Kituo cha Huduma Mahala pamoja itaandaa miongozo ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi na kwa wakati. Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 inayohusu kubadili au kuacha uwekezaji, Kamati inashauri kifungu hiki kikaboreshwe kwa kuweka kosa na adhabu kwa kiwango cha chini na juu kwa mwekezaji ambaye atakiuka kuitaarifu Mamlaka kuwa amebadili au kuacha uwekezaji. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na marekebisho yamefanyika kama inavyoonekana katika jedwali la Marekebisho.

**Ibara ya 23** inahusu Benki ya Ardhi, Kamati ilitaka ufafanuzi juu ya kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki. Je kuna fidia itakayolipwa kwa maeneo ya watu binafsi yatakayo ingizwa katika benki ya ardhi?. Serikali ilifafanua kwamba Ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi itakayowekwa katika benki ya ardhi inaendelea kubaki kuwa mali ya mtu husika hadi hapo atakapopatikana mwekezaji ambaye ndiye atawajibika kulipa fidia kwa mmiliki. Kamati ilikubaliaana na ufafanuzi wa Serikali kwa kutoa angalizo kwamba Mamlaka isimamie mchakato mzima mpaka kukamilika kwa ulipaji wa fidia.

### 2.6.4 Sehemu ya Nne ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inaanzia Sehemu hii ina ibara 6 kuanzia Ibara ya 25 hadi ibara ya 30 na inaweka masharti kuhusu "Maeneo Maalumu ya Kiuchumi". Sehemu hii inaanzisha maeneo maalumu ya kiuchumi katika sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuvutia uwekezaji ili kuongeza tija katika uwekezaji, ushindani, ukuaji wa uchumi, uhamasishaji wa mauzo ya nje na uzalishaji wa ajira kwa Watanzania.

**Vilevile,** sehemu hii inaweka utaratibu wa kutambua ardhi inayofaa kwa madhumuni ya kuanzisha maeneo maalumu ya kiuchumi, masharti ya masuala ya forodha katika eneo maalumu la kiuchumi, utaratibu wa uingizaji na utoaji wa huduma na bidhaa katika maeneo maalumu ya kiuchumi, katazo kwa mwekezaji kutoruhusiwa kufanya uwekezaji au biashara katika eneo maalumu la kiuchumi isipokuwa kwa leseni iliyotolewa na Mamlaka na wajibu wa kuomba kibali kwa Mamlaka kwa mtu anayekusudia kutoa huduma ndani ya eneo maalumu la kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Uchambuzi wa Ibara hizi, Kamati iliomba kupata ufafanuzi wa **Ibara ya 27** inayohusu Masuala ya forodha katika eneo maalumu la kiuchumi, ni ipi mipaka ya utendaji kazi kati ya mamlaka ya forodha na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ili ifahamike mipaka ya utendaji kazi kati ya mamlaka hizi mbili.

Serikali ilitoa ufafanuzi kuwa, baada ya eneo kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi liko chini ya Mamlaka, hata hivyo kwa madhumuni ya forodha, kuhusu masuala ya usimamizi wa kodi, eneo hilo litadhibitiwa na mamlaka ya forodha. Kamishna Mkuu wa TRA ataweka utaratibu wa usimamizi wa kodi katika eneo husika kama ilivyo sasa. Baada ya majadiliano, Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Serikali

**Ibara ya 30** inafafanua wajibu wa watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi**,** Kamati inapendekeza kuwa kanuni zitakazotungwa kuhusu utaratibu wa kuomba kibali cha kutoa huduma ndani ya eneo maalumu la kiuchumi zibainishe makosa na adhabu kwa viwango vya chini na juu. Lengo la kutoa pendekezo hili ni kuongeza utii wa sheria kwa watakaokiuka masharti ya kuwa na leseni ya kutoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi. Baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Serikali.

### 2.6.5 Sehemu ya Tano ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu Haki na Wajibu wa Serikali kwa Mwekezaji na ina jumla ya ibara 7 kuanzia ibara ya 31 hadi Ibara ya 37. Kiujumla sehemu hii inafafanua juu ya haki kwa Serikali ya kusimamia shughuli zote za uwekezaji ili kuhakikisha zinaendana na misingi na malengo ya Sheria, wajibu wa mwekezaji, dhamana ya uhamishaji wa mitaji, faida na gawio, kinga dhidi ya utaifishaji au utwaaji wa mali za mwekezaji, fursa sawa kwa mwekezaji wa kigeni, ukomo wa kuajiri wafanyakazi wa kigeni na upatikanaji wa mikopo kwa mwekezaji wa kigeni kutoka benki na taasisi za fedha za ndani. Kamati imeridhishwa na Ibara hizi kwani zinalenga kuleta uwazi na uwajibikaji kwa pande zote mbili yani Serikali na Mwekezaji kwa lengo la kuleta tija iliyokusudiwa.

### 2.6.6 Sehemu ya Sita

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii ina ibara 3 kuanzia ibara ya 38 hadi Ibara ya 40 na imelenga kufafanua namna ya kushughulikia Malalamiko na Utatuzi wa Migogoro, utaratibu wa kukata rufaa kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka na utatuzi wa migogoro pale ambapo mgogoro utatokea baina ya mwekezaji na Mamlaka au Serikali. Kamati imeridhishwa na Ibara hizi kwa angalizo kwamba, Serikali/Mamlaka isimamie kikamilifu masharti ya kifungu cha 120A na 120B cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113 kinacho weka masharti kwamba fedha/mkopo utakaopatikana kwa dhamana ya ardhi ya uwekezaji iliyotolewa na mamlaka ziwekezwe Tanzania.

### 2.6.7 Sehemu ya Saba

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ina jumla ya Ibara 4 kunzia Ibara ya 41 hadi ya 44 na inafafanua kuhusu "Masharti ya Fedha" ambapo inaelezea kuhusu vyanzo vya fedha vya mamlaka, masharti ya uandaaji wa bajeti ya mamlaka, masharti kwa Mamlaka kuandaa taarifa ya mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha. Kamati imeridhishwa na

ufafanuzi wa Ibara hizi kwani zinalenga kuleta uwazi na uwajibikaji kwa Mamlaka.

### 2.6.8 Sehemu ya Nane

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii ina jumla ya Ibara sita (6) kunzia Ibara ya 45 hadi ya 50 na inatoa ufafanuzi kuhusu "Masharti ya Jumla" ambapo inapendekeza makosa na adhabu kwa mtumishi wa Mamlaka au mtu mwingine ambaye wakati wa kutekeleza Sheria hii atapata nyaraka au taarifa yoyote chini ya Sheria hii na kuwasilisha nyaraka au taarifa hiyo kwa mtu mwingine ambaye hajaidhinishwa kwa sheria yoyote au na Bodi.

Vilevile, inafafanua kuhusu kinga kwa Mjumbe wa Bodi, Mkurugenzi Mkuu au afisa wa Mamlaka kutofunguliwa shauri, madai au kuwajibishwa, matumizi ya sheria nyingine, mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022, Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya mwaka 2002 na Sheria ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2006 pamoja na kutambua masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na Sheria zinazopendekezwa kufutwa.
Uchambuzi wa Kamati kwa Ibara hizi, Kamati ilitoa mapendekezo ya kufanya maboresho katika ibara ya 45 kuwa uwekwe ukomo wa chini wa adhabu. Ambapo kwa mujibu wa muswada uliowasilishwa umewekwa ukomo wa juu pekee ambao ni kiasi kisichozidi shilingi Milioni tano au kifungo kisichozidi mwaka mmoja na au vyote, Serikali iliridhia pendekezo la Kamati na kuahidi kuliweka katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali ambapo ilipendekezwa kuweka ukomo wa chini wa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja.

### 2.6.9 Sehemu ya Tisa

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, ambayo ina ina jumla ya Ibara 18 kuanzia Ibara ya 51 hadi 68. Kamati iliridhishwa na ufafanuzi wa Ibara hizi kwasababu unalenga kuondoa ukinzani wa Sheria nyingine za nchi katika kutekeleza matakwa ya Sheria inayokusudiwa kutungwa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 Maoni na Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa madhumuni, maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati ina maoni ya jumla na mapendekezo mahsusi ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa Sheria hii kama ifuatavyo:

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maamuzi ya kuunganisha baadhi ya taasisi zake ambazo majukumu yake kwa namna moja ama nyingine yanafanana. Uamuzi huu utakwenda kuongeza ufanisi na kuipunguzia mzigo wa Ruzuku. Serikali ilitangaza kuunganisha jumla ya taasisi na mashirika 19, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee na mchakato wa kuunganisha mashirika hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija na kupunguza mzigo kwa Serikali.

### 3.2 Maoni na Mapendekezo Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi na marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada huu, Kamati inaisisitiza Serikali katika mambo muhimu yafuatayo;

#### 3.2.1 Kuweka Vivutio vya kiushindani

**Mheshimiwa Spika,** Sheria inaaeleza kuandaliwa kwa orodha ya vivutio vinavyotolewa kwa wakekezaji na kuvitangaza, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe ninazingatia kuwa vivutio vinavyotolewa vinakidhi hali ya ushindani ili sheria inayotungwa iweze kuwa yenye ufanisi na tija hususani katika kuvutia mtaji kutoka nje ya nchi (FDI).

#### 3.2.2 Uwezeshaji kwa Wazawa

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 22 ya sheria inayopendekezwa kutungwa inaeleza kuwa Waziri kwa kushauria na waziri mwenye

dhamana ya fedha anaweza kubainisha maeneo mahususi ambayo wawekezaji wa ndani wanaweza kupewa vivuti kwa kuzingatia sheria husika, Kamati inashauri kwamba, serikali iandae namna bora itakayowawezesha wawekezaji wazawa kushiriki kikamilifu katika uwekezaji ili kukuza mitaji yao na uchumi wa nchi.

**3.2.3 Benki ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, sheria imeainisha kuwa Benki ya Ardhi itakayokuwa chini ya Mamlaka itahusisha ardhi za watu binafsi na kuwa ardhi ya mtu binafsi itakayoingizwa katika benki ya ardhi inaendelea kubaki kuwa mali ya mtu husika hadi hapo atakapopatikana mwekezaji ambaye ndiye atawajibika kulipa fidia kwa mmiliki. Kamati inashauri Mamlaka isimamie mchakato mzima wa utoaji wa ardhi ya mtu binafsi Kwenda kwa mwekezaji na utaratibu mzima wa ulipaji fidia ikiwa ni pamoja na kufanya uthaminishaji wa ardhi hiyo ili mmiliki aweze kupata fidia stahiki.

**3.2.4 Watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria inatoa wajibu kwa watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumu kuomba kibali kwa Mamlaka, Kamati inashauri kuwa Serikali izingatie kuwa kanuni zitakazotungwa kuhusu utaratibu wa kuomba kibali cha kutoa huduma ndani ya eneo maalumu la kiuchumi zibainishe makosa na adhabu kwa viwango vya chini na juu ili Kuongeza utii wa sheria kwa watakokiuka masharti ya kuwa na leseni ya kutoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi.

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mheshimiwa Prof. Alexander Kitila Mkumbo (Mb) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Mipango na

Uwekezaji kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa uchambuzi wa muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma pamoja na Mheshimiwa Mary Fransis Masanja (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Augustine Vumma Hole, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Fransis Msanja, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb
5. Mhe. Aida Joseph Kenani, Mb
6. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb
7. Mhe. Angelah Jasmin Kairuki, Mb
8. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb
9. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb
10. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
11. Mhe. Charles Muguta Kajege,  Mb
12. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb
13. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb
14. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
15. Mhe. Fratey Gregory Massay Mb
16. Mhe. George Natany Malima, Mb
17. Mhe. Haji Amour Haji, Mb
18. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb
19. Mhe. Matha Nehemia Gwau, Mb
20. Mhe. Nicholaus Ngassa, Mb
21. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb
22. Mhe. Santiel Erick Kirumba, Mb
23. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Baraka Idelphonce Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza jukumu la kuchambua muswada huu kwa ukamilifu mpaka leo hii ninaposoma taarifa hii.

**4.1 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024** pamoja marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Augustine Holle Vuma, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**
13 FEBRUARI, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza suala la kuchangia. Tunaanza na Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Kaijage wajiandae.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Samahani, ni Mheshimiwa Kajege.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenipa kibali cha kusimama mbele yako katika Bunge hili. Kipekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kupitishwa kuwa mgombea katika kiti cha Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza kwa sababu kazi za Mheshimiwa Rais zinajionesha waziwazi na Awamu hii ya Sita kazi imefanyika kwa kiwango cha juu. Sambamba na hilo, ninampongeza Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza ambapo uchaguzi utakapofika tunaenda kuweka mambo waa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakipongeza Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia misingi bora na utawala bora hususani katika kutuongoza sisi wanachama wa chama hicho. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba muswada huu unafika Bungeni. Pia kwa yale ambayo sisi Wanakamati tumeyapendekeza wameweza kuyapokea na kuyazingatia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia siwezi kumsahau Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Vuma, kwa kazi nzuri anayoifanya kuiongoza Kamati yetu na hatimaye tumeweza kuleta maoni kuhusu muswada huu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Kituo cha Uwekezaji kilikuwa kinawafanya wawekezaji wanaotafuta fursa mbalimbali za uwekezaji katika nchi yetu kukutana na changamoto nyingi sana za uwekezaji, hususani tulikuwa na *TIC* pamoja na *EPZA*. Vituo hivi vilikuwa vinaingiliana sana kiutendaji na kimajukumu. Kuanzishwa kwa mamlaka ya uwekezaji ambayo itakuwa inafanya kazi kama taasisi kutawarahisishia wawekezaji wanaotafuta fursa za kuwekeza hapa nchini kupata huduma bora katika kituo kimoja ambacho kitakuwa ni mamlaka ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili litawasaidia wawekezaji kupata taratibu zilizo bora. Pia wawekezaji wanaotafuta fursa za kuwekeza hapa nchini wataweza kufika katika kituo hicho na kusaidika kikamilifu kuliko ilivyokuwa hapo awali ambapo mwekezaji anapokuwa anatafuta namna ya kuweka anaenda

sekta hii na hii mwisho wa siku anaweza kumaliza mwaka mzima anatafuta fursa ya uwekezaji na asiipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa mamlaka hii ita-*coordinate* shughuli zote za uwekezaji, itawasaidia hawa wawekezaji kuhamasika au kuhamasishwa kuweza kuwekeza hapa nchini. Kwa kuwa mamlaka hii pia itaratibu shughuli zote, itawalinda wawekezaji na itaweza kuhamasisha uwekezaji hapa nchini. Kumbe sasa kila mwekezaji wa ndani au wa nje ya nchi atakapokuwa anahitaji kuwekeza kutakuwa na eneo moja ambalo ataweza kufika na eneo hilo litasaidia sasa ku-*coordinate* shughuli zote za uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kutakuwa na mfumo bora wa kielektroniki ambao utasaidia kuunganisha taasisi zote za kiserikali na Wizara zote kuhakikisha kwamba uwekezaji wenye tija katika maeneo ya kisekta utaunganishwa katika mamlaka hii. Tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhamasisha wawekezaji kuja hapa nchini na hata wawekezaji wa ndani. Pia tunampongeza mama kwa kuwa amekuwa kinara wa uwekezaji na mambo ya kidiplomasia. Hali hii imesababisha kuleta muswada huu Bungeni ili uweze kupitishwa na kuweza kuwasaidia wawekezaji waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuiomba Serikali kwenye suala la utoaji wa ardhi. Kwanza kabisa ardhi tuliyonayo ni hii hii, wananchi wanazidi kuongezeka na pia tunaenda kuanzisha mamlaka hii ambapo kutakuwa na benki ya ardhi. Ninaiomba Serikali tuwe na tahadhari katika eneo hili, suala la utoaji wa ardhi kuwe na *process* nzuri ya kuwafanya wazawa waweze kulipwa fidia kwa wakati. Pia ardhi hii ambayo inaenda kutwaliwa itwaliwe kwa utaratibu na kwa kuzingatia misingi bora ya sheria za ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na mfumo mzuri kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Nipo zaidi kwenye wawekezaji wa ndani. Wawekezaji wa ndani waandaliwe mazingira bora, tusije tukafanya ushindani kati ya wawekezaji wa nje na wa ndani.

Pia kuwe na mfumo mzuri wa kuwawezesha hawa wawekezaji wa ndani wapate mikopo kwa haraka. Kwa mfano, mwekezaji anapotaka kufanya uwekezaji katika nchi yake, wazawa hawa wanufaike na uwekezaji wao ikiwepo kupata mikopo kwa wakati. Kwa mfano mwekezaji anataka kuwekeza kitu fulani, basi asizungushwe kwa mwaka mzima anatafuta huo mkopo ilihali mwekezaji anayetoka nje ya nchi anapopata fursa ya kuja kuwekeza inakuwa ndani ya mwezi mmoja anakuwa ameshapata hiyo nafasi. Kwa hiyo, ninaiomba sana tuweke mazingira bora kwa wawekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Charles Kajege ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kuchangia kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa uhai na kuweza kunisimamisha hapa kwa ajili ya kuweza kuchangia mchango wangu huu unaojielekeza kwenye muswada wetu huu mpya wa Sheria ya Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali yangu ya kawaida, ninawapongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuweza kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kuwa wagombea wa Chama Cha Mapinduzi kwa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri Kitila ambaye ni Waziri wa Uwekezaji kwa jitihada zake kubwa anazozifanya katika kuhakikisha kwamba uwekezaji wa nchi yetu unakuwa bora na wenye tija kwa nchi yetu. Pia

ninampongeza Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Augustine Vuma, kwa kuweza kuwasilisha ripoti yetu hii ya Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu kwa namna alivyoeleza taarifa yake. Kwa kweli ninampongeza kwa taarifa yake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa Uwekezaji wa Maeneo Maalumu haukuja tu hivi bure, umekuja kwa malengo maalumu ili kuchochea uchumi wa nchi yetu kadiri ambavyo tunakusudia kwenda. Kama nchi yetu ya Tanzania kuwafanya wawekezaji wetu wa ndani pamoja na wawekezaji wa nje kuweza kuimarisha uwekezaji wao na kuifanya nchi yetu kuwa na uwekezaji ulio bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuangalia taarifa hii tulipoletewa muswada ule, tulikuja na njia tofauti za kuweza kuangalia maoni na mapendekezo juu ya muswada huu. Kitu cha kwanza tulijaribu kuangalia hali ya sera zetu pamoja na sheria za nchi yetu zinatuelekeza juu ya namna bora ya kuendana na muswada huu wa uwekezaji katika maeneo maalumu. Njia ambazo tulizitumia ni moja kati ya njia bora ile ya uwasilishaji kwa watu kuja kuleta maoni yao kwa ajili ya kutoa maoni yaliyo bora katika muswada wetu huu. Pia tuliangalia suala la sera yetu pamoja na Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ilivyotuelekeza kuhakikisha kwamba tunakuwa na uwekezaji ulio bora na ulio katika hali njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote tunayaangalia kwa kuangalia tija na ufanisi kwa mamlaka hii ili kuboresha uwekezaji kutokana na takwa la Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyotuelekeza na namna alivyoielekeza taasisi yetu hii ya uwekezaji kwamba ni lazima tuwe na uwekezaji ulio bora na huru kwa faida ya wananchi wetu na wawekezaji wanaokuja katika nchi yetu. Vilevile kwa kuangalia mwongozo wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambao umetuelekeza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia uzoefu wa nchi tofauti ndiyo uliotupa mwongozo katika kuangalia suala hili. Uzoefu umetuelekeza katika nchi tofauti, nchi ambazo tuliziangalia katika kuangalia muswada huu na kuangalia

uwekezaji ulio bora tuliweza kuangalia nchi za Rwanda, Kenya, Singapore, *South Africa* pamoja na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, muswada wetu huu tuliujadili kwa namna kubwa sana kuhakikisha kwamba utakuwa ni muswada bora kwa kuangalia maeneo yaliyo mazuri hasa kwa upande wa ardhi. Kwa wale watakaoweza kuwekeza katika ile ardhi maana yake kuwe na ardhi itakayotwaliwa kama ni ya binafsi iweze kutumika katika hali ya ubora. Vilevile kwa wale wenye ardhi binafsi kwa hiari yao waweze kuipeleka katika mamlaka kwa makubaliano maalum ili kusudi uwekezaji uweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yetu kwa upande wa Kamati tungependa kuishauri Serikali iangalie baadhi ya taasisi ambazo zinafanana majukumu kama ilivyo *EPZ* pamoja na hiyo taasisi ambayo tumeiunganisha na yenyewe iweze kufanya muunganiko kama huu ili kuwe na vitu ambavyo haviwezi kuwa *duplication* ya vitu viwili kwa taasisi mbili pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaunga mkono hoja na mapendekezo ya taarifa yetu hii kwa namna ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Augustine Vuma. Ninaomba kuunga mkono hoja, pia ushauri na mapendekezo yaliyopendekezwa na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika muswada huu.

Kwanza, ninapenda niipongeze Serikali kwa kuleta muswada huu mbele yetu. Sheria hii ni nzuri sana endapo itasimamiwa na kutekelezwa kikamilifu hasa na watumishi ambao wanahusika katika mamlaka yetu. Nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashauri watumishi ambao tutakuwa nao katika mamlaka hii wawe *very pro-active*, yaani wawe mbele ya wakati muda wote kuweza kutambua vivutio na kujua namna ambavyo tutapata wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine inabidi watumishi wa mamlaka hii wapate nafasi ya kwenda kujifunza katika mamlaka za nchi zingine. Mwenzangu ametaja nchi kama Singapore, Rwanda, *South Africa* na nyingine. Hii itasaidia sana watumishi wetu wa mamlaka husika waweze kuwa mbele ya wakati na kujua namna ya ku-*deal* na *investors* ambao wanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo ninaliona ni lugha. Tukiangalia wawekezaji wengi wanatoka katika nchi nyingine nyingi kama China, Ujerumani, Spain na nchi nyingine. Wakija Wachina mara nyingi unakuta kwamba ni vigumu sana kuongea kiingereza, kama watumishi wetu wa mamlaka hawatakuwa wanaweza kuongea hizi lugha kwa ufasaha, Kichina, Kijerumani, Ki-spanish itakuwa ni tatizo sana kuweza kuwasaisdia hawa wawekezaji ambao wanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali pamoja na mambo mengine, ihakikishe kwamba watumishi wa mamlaka yetu hii wawe ambao wanaweza kuongea lugha nyingi za kigeni ikiwa ni pamoja na Mandarin, Kijerumani, Ki-spanish na lugha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linajitokeza mara kwa mara ni hatuna ubora katika *customer service* yetu. Mgeni anapokuja ile *introduction approach* yetu inakuwa siyo *friendly,* kwa hiyo, tunapoteza sana masoko na hasa *potential investors* kutokana na kwamba *customer service* yetu ni mbovu sana.

Kwa hiyo, ninashauri wahusika wahakikishe kwamba watumishi wa mamlaka hii wanakuwa *trained* kujua namna ya ku-*handle potential investors* ambao wanakuja katika nchi yetu, vinginevyo tutakuwa tunawapoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine limekuwa ni urefu wa kuchakata maombi ya wawekezaji. Ukiangalia nchi za jirani kama Rwanda kwa mfano, tunaelezwa kwamba mchakato wa kuanzia kutuma maombi na kufanikiwa kupata kibali cha leseni inachukua *less than one-month,* lakini hapa kwetu inaweza ikachukua hata miaka mitano. Sasa huyo mwekezaji hawezi kukubali kuendelea kusubiri hapa miaka mitano wakati ile fursa ya uwekezaji wake inaendelea kupotea. Kwa hiyo, ni lazima hawa wafanyakazi wa mamlaka yetu kuhakikisha wanakuwa ni *business friendly* na wanajua namna ya kuchakata maombi yetu ikiwa ni leseni na vibali vingine ambavyo vinahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni *brochures* zile za vivutio vyetu, yaani yale maeneo ya kuwekewa vitega uchumi. Mengi yatakuwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza lakini kama nilivyosema kuna watu wengi ambao watakuja kutoka katika mataifa mengine. Kwa mfano, China, Ujerumani, Spain, Ureno, Brazil na kwingine, kwa hiyo hata hizi *brochure* inabidi ziwe katika lugha ambayo inaeleweka kwa *potential investors* ambao wanakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho ninataka niishauri Serikali, ili tuendelee inabidi na sisi tubadilike. Mara nyingi tunasifia kwamba wazungu wameendelea, lakini kwa nini na sisi tusiendelee? Wengi wetu humu tumesoma Ulaya na Marekani lakini kwa nini tukirudi hapa hatubadiliki? Mimi ninaomba hebu tuangalie ni kitu gani ambacho sisi pamoja na kusoma Ulaya, Marekani na wapi kwa nini tukija hapa hatufanyi kama wanavyofanya wenzetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya na mtoa hoja ajiandae. Kwa maandishi?

Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii tena ili niweze kuhitimisha hoja hii kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu ukiacha Kamati, umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge watatu ambao ni Mheshimiwa Mary Francis Masanja ambaye kimsingi ameunga mkono, ametupa tahadhari kuhusu benki ya ardhi hususani masuala ya fidia na mimi ninakubaliana naye kwamba ni mambo ya msingi. Mambo mawili tumezingatia kwenye muswada; moja ni kwamba sheria zetu za ardhi zinazohusu utaifishaji wa ardhi zitazingatiwa. Kwa hiyo, mtu kama ardhi yake imechukuliwa na benki hii litazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu ni kwamba ardhi hii kwa maana ya benki ya ardhi, haitakuwa tu kwa Serikali, mtu binafsi au taasisi binafsi popote ilipo inaweza ikawasilisha ardhi yake na ikatambuliwa kama sehemu ya benki ya ardhi na atakuwa anamiliki yeye mwenyewe, kwa hiyo, ataunganishwa na wawekezaji. Hivyo si lazima anyang'anywe ardhi, anaweza akabaki nayo, lakini itatambuliwa kwamba ni ardhi ambayo ipo katika benki ya ardhi na ataunganishwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Mheshimiwa Masanja ametoa tahadhari kuhusu wawekezaji wa ndani kupewa mazingira mahsusi. Muswada huu umetambua hilo katika maeneo mawili; kwanza, kwenye upande wa wawekezaji wa kimkakati; wawekezaji wa ndani wamepewa mtaji ulio mdogo ambao ni dola milioni 20 wakati wawekezaji wa nje ni dola milioni 50. Kwa hiyo limewekwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeweka kifungu maalumu, ile Ibara ya 22 tumeweka wazi kwamba Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji atakuwa na uwezo wa kuyabaini maeneo na vivutio mahsusi kwa ajili ya wawekezaji wa ndani. Hiki kilikuwa ni kilio cha muda mrefu, kwenye muswada huu tumetambua kwamba Watanzania hawa wana haki ya kufaidika na rasilimali za nchi

yao. Kwa hiyo, katika suala la uwekezaji pia lazima wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea pia mchango wa Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Makunduchi tutauzingatia na yeye ameunga mkono. Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara ameeleza vizuri na yeye ameunga mkono. Ametoa tahadhari kuhusu watumishi wa umma katika maeneo mawili. Suala la kubadilisha mtizamo ni kweli, ni muhimu sana ili tufanikiwe katika uwekezaji huu wawezeshaji wakubwa sana ukiacha taasisi husika ni watumishi wa umma waliopo katika sekta mbalimbali. Tunaendelea kutoa wito kwamba ni muhimu sana watumishi wa umma wakae katika mkao wa kuwezesha uwekezaji kwa sababu uchumi tunaouzungumzia ili ukue tunahitaji uwekezaji mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi hizi ambazo tunazungumzia ili tuweze kupata kodi na kupanua wigo wa kodi lazima biashara zifanyike na uwekezaji mpya uweze kufanyika. Ili watumishi wa umma walipwe mishahara ambayo tunalipwa lazima biashara zifanyike. Kwa hiyo, mtumishi wa umma yeyote ambaye anakwamisha biashara, anakwamisha uwekezaji, anakwamisha shughuli za Serikali, anakwamisha makusanyo ya kodi, anakwamisha hata mishahara yake mwenyewe. Kwa hiyo, ni kwa faida yetu sisi wenyewe kuhakikisha kwamba uwekezaji unakwenda vizuri na biashara zinafanyika katika mazingira ya uhuru na kwa kuzingatia sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lugha za wawekezaji nadhani ni muhimu sana. Tuna-*deal* na wawekezaji wengi kwa sasa, kwa mfano, wawekezaji wengi ambao wanakuja hapa namba moja kabisa wa kigeni ni kutoka China wakifuatiwa na wawekezaji kutoka *Europe* na Asia. Kwa hiyo, ni muhimu tuendelee kutoa mafunzo angalau watu wetu wawe na uelewa wa lugha hizi za msingi tu wafahamu kiswahili vizuri, wafahamu kiingereza na lugha zingine za kimataifa ikiwemo kichina. Kwa hiyo, ni maangalizo muhimu ambayo ni muhimu kuyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusisitiza kwamba Waheshimiwa Wabunge, muswada huu ni maboresho makubwa sana kuangalia zile sheria ambazo tunazo sasa hivi, lakini ni muhimu sana tunaenda kuanzisha taasisi mpya ambayo itakuwa imara, kubwa zaidi yenye mamlaka makubwa ya kuweza kushughulikia masuala ya uwekezaji, pia maeneo maalumu ya kiuchumi hapa nchini *especially economic zones.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nimalizie kwa kutoa shukurani kubwa sana kwa viongozi wetu wa Chama Cha Mapinduzi na Serikali. Pia niseme kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi. Dalili tatu za msingi sana za kushinda mwaka huu wa uchaguzi, moja ni kwamba chama cha siasa lazima kiwe na utulivu, mshikamano na umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka kuchukua hii kuwapongeza viongozi wetu kwa kuhakikisha kwamba Chama Cha Mapinduzi kina utulivu, kina mshikamano, kina umoja. Hakuna chama chochote duniani ambacho kimewahi kushinda bila kuwa na vitu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ili chama kishinde kinahitaji kuwa na wagombea wazuri, imara, makini na wagombea hawa wapatikane mapema iwezekanavyo. Chama Cha Mapinduzi tunakipongeza kwa kupata wagombea wake wa Urais na Mgombea Mwenza na Mgombea wa Zanzibar mapema. Hizo ni dalili kubwa za ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili ya mwisho ni utekelezaji imara wa ahadi zilizotolewa. Kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM wa mwaka 2025 kwa asilimia kubwa mambo yaliyofanyika hakuna shaka kwamba mwaka huu wa uchaguzi ni mwaka wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kutoa hoja, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante Profesa hasa kwa maneno yako ya mwisho hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wageni 73 wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Wajumbe wa Mfuko wa Jimbo, Watendaji Kata wa Mitaa Tarime, Mtaa wa Tarime Mjini kutoka Mkoa wa Mara, karibuni sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka wa 2024, ukurasa wa nne.

Jina Refu la Muswada

*(Jina Refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebesho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebesho yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebesho ya Serikali)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza Ibara mpya ya 46.

Ibara Mpya ya 46

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebesho ya Serikali)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya marekebisho kwenye jedwali.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo Serikali inapendekeza kupanga upya Ibara za Muswada visomeke Ibara ya 47 hadi 69.

**MWENYEKITI:** Baada ya marekebisho hayo Serikali inaomba Ibara hizo za Muswada zisomeke Ibara 47 mpaka 69. Mnaafiki?

*(Mabadiliko za namba za Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipitishe Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya Mwaka 2024 pamoja na marekebisho yake.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya kuweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji Tanzania, kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji, kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini, kuweka utaratibu wa uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi, kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania, 2022, Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, 2002 na Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji, 2006 na masuala yanayohusiana na hayo. Kusomwa mara ya tatu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii sasa Bunge limekamilisha majukumu yake ya kupitisha sheria hii. Sasa imebaki sheria hii kwenda kwenye mamlaka ya nchi na isainiwe ili iwe sheria. Nakupongeza sana Waziri na timu yako kwa kazi nzuri mliyoifanya. Mheshimiwa *AG* hongera kwa kazi nzuri uliyoifanya pamoja na Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote. Haya ndiyo mambo tunayoyataka. Bila uwekezaji nchi yetu haiwezi kwenda mbele. Tusiogope mabadiliko, tusi-*resist* mabadiliko, tukubali mabadiliko kwa sababu ndivyo dunia inavyokwenda na hasa kipindi hiki ambacho nchi nyingi zinataka kubaki peke yake. Sisi tuna uwezo mkubwa sana chini ya uongozi wa jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Hongereni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati inayoshughulika na Hesabu za Serikali za Mitaa, ninaomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati za mwaka 2024 ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2023. Ninaomba Taarifa yote ya Kamati iingie kama ambavyo imewasilishwa, nitakachokisoma hapa ni *summary* ya taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutupatia fursa ya kukutana leo ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Februari, 2025 ili iweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, mwezi Agosti na Oktoba, 2024 Kamati ilichambua Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za halmashauri 55 ambazo ni sawa na 29.83% ya halmashauri zote 184.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka mzima kuanzia Februari, 2024 hadi Februari, 2025 Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na jumla ya halmashauri 69 na kufanya ziara za ukaguzi wa ufanisi wa miradi ya maendeleo katika halmashauri 27, hivyo kufanya jumla ya halmashauri zote zilizofikiwa na Kamati ndani ya mwaka mmoja kuwa ni halmashauri 96 sawa na 52% ya halmashauri zote 184.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati; tarehe 15 Februari, 2024 Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* iliwasilisha Taarifa yake Bungeni kuhusu shughuli za Kamati zilizotekelezwa kwa mwaka 2023. Katika taarifa hiyo, jumla ya mapendekezo nane yalitolewa na baadaye kuwa maazimio ya Bunge. Tarehe 14 Januari, 2025 Kamati ilikutana na *CAG* pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kupokea, kujadili na kuchambua utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya *LAAC* kwa kipindi cha mwezi Februari, 2023 hadi 2024. Matokeo ya utekelezaji ni kama yanavyoainishwa katika Jedwali Namba 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio yaliyotolewa na Bunge; maazimio yaliyotekelezwa kikamilifu ni moja sawa na 10%; maazimio yaliyo katika hatua ya utekelezaji ni tisa sawa na 90% na maazimio yasiyotekelezwa ni sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu kuhusiana na maoni ya utekelezaji wa maazimio haya imeambatanishwa ili Wabunge waweze kusoma taarifa hii kwa kina zaidi kwa sababu hapa tunazungumzia *summary*. Maazimio ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ni kama yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za utekelezaji wa miradi zisizoakisi uhalisia; azimio hili limetekelezwa kwa 60% ambapo nyaraka za kuonesha uchambuzi wa gharama uliofanyika katika halmashauri 10 ziliwasilishwa kwa *CAG* na kuhakikiwa. Hata hivyo, hakuna taarifa rasmi iliyowasilishwa inayobainisha vigezo vya uteuzi wa halmashauri hizo iwapo zinawakilisha kikamilifu miradi yote iliyotekelezwa au namna uchambuzi huo ulivyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio lingine lililotolewa katika eneo hili ni kwamba Serikali ihakikishe gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi zinajumuishwa katika fedha zinazopelekwa kwa halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ya *force account* katika kila halmashauri. Azimio hili pia limetekelezwa kwa 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa wataalamu wa kada ya uhandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu wa majengo katika halmashauri; azimio hili limetekelezwa kwa 70% kwa kuwa licha ya Serikali kuajiri wataalamu wa kada ya uhandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023, bado kuna upungufu wa wataalamu hawa katika halmashauri kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutofanyika kwa tathmini ya mahitaji ya miundombinu muhimu kabla ya utekelezaji wa miradi; utekelezaji wa azimio hili unaendelea na umefikia 70% ambapo taarifa ya tathmini iliyowasilishwa kwa *CAG* kwa uhakiki imebaini kuwa uwepo wa miradi 20 yenye thamani ya shilingi bilioni 7.5 katika sekta ya elimu na afya ambayo haitumiki kutokana na changamoto za ukosefu wa umeme, maji na

barabara ambapo changamoto hizo zinatarajiwa kutatuliwa kati ya mwezi Januari mpaka Juni, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora usiokidhi vigezo vya miradi iliyotekelezwa kwa *force account;* azimio hili limetekelezwa kwa 70% ambapo Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwachukulia hatua wakurugenzi na kutoa mafunzo kwa maafisa wa ngazi za mikoa na halmashauri kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge pia lilitoa azimio juu ya Serikali kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa kwa kutumia *force account* na kukokotoa gharama za uchakavu wa miradi hiyo, kama ilivyoelezwa kwenye mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali pamoja na kuchukua hatua kwa watendaji wote watakaobainika kutekeleza miradi chini ya kiwango. Utekelezaji wa azimio hili umefikia 20% ambapo Serikali imeeleza kuanza taratibu za ufuatiliaji wa miradi yote iliyo chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio lingine katika eneo hili liliitaka Ofisi ya Ukaguzi *(NAOT)* kufanya ukaguzi wa kina juu ya ubora wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya *force account* kwa kuzingatia uhai wa miradi kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali. *CAG* ameitaarifu Kamati kuwa utekelezaji umefikia 60% ambapo kwa kutumia mpango kazi wa mwaka 2024/2025 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweka kaguzi za kiufundi kwenye miradi na kaguzi maalumu ambapo kaguzi hizi zikikamilika taarifa itatolewa kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyopo na itawasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutozingatiwa kwa hatua za kitaalamu za ujenzi; azimio limefikia 80% kwa Serikali kuanza utekelezaji wa azimio hili kwa kutoa maelekezo kwa wakurugenzi wote. Pamoja na kwamba maelezo yametolewa hakuna mwongozo unaowaongoza viongozi wa mikoa na halmashauri ni hatua zipi wachukue pindi yanapotokea matatizo kama haya kinyume na matakwa ya kitaalamu yaliyopo kwenye miongozo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali ikaandae miongozo na siyo kuandika barua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukiukwaji wa mwongozo wa utekelezaji wa mradi kwa kutumia njia ya *force account;* katika eneo hili, Serikali imetekeleza kwa 50% kwa kuwa imeanza kuchukua hatua kwa halmashauri zilizobainika kukiuka miongozo inayotolewa na Serikali na barua za kuanza uchunguzi husika kutoka *PPRA* zimehakikiwa na *CAG*. Kwa hiyo, tunatarajia pia kupata taarifa ya kina kutoka *PPRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukiukwaji wa miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI; azimio la Bunge lilikuwa kuitaka Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe inasimamia na kuchukua hatua dhidi ya watendaji watakaobainika kukiuka miongozo inayotolewa. Kamati imepewa taarifa juu ya hatua mbalimbali za kinidhamu zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa. Pia Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alielekezwa kwa barua kufanya uchunguzi wa maeneo yenye dosari kama yalivyoainishwa na Kamati. Utekelezaji umefikia 60%. Hata hivyo, hakuna mrejesho wa kimaandishi kutoka TAKUKURU juu ya ukamilishaji wa uchunguzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema hapa TAKUKURU ni kichochoro cha kutokuzuia masuala haya yanayotakiwa kupatiwa ufumbuzi na ni bahati nzuri hapa TAMISEMI wenyewe wameandika barua TAKUKURU na TAKUKURU hawajaijibu TAMISEMI yenyewe, kwa hiyo, tunaelekeza Serikali ichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekretarieti za Mikoa kutofuatilia utekelezaji wa miradi; Serikali imetekeleza azimio hili kwa 50% kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji. Hata hivyo, ripoti ya tathmini inayobainisha upungufu wa utendaji kazi kwa Ofisi ya Makatibu Tawala na Mikoa katika kusimamia miradi yote ya maendeleo na namna ya kutatua changamoto zilizojitokeza haijawasilishwa. Serikali iwasilishe hiyo ripoti kwa *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi kutokamilika kwa wakati; hadi Desemba, 2024 jumla ya miradi 137 sawa na 37.5% kati ya miradi 365 iliyohojiwa imekamilika na miradi 228 bado

haijakamilika. Hata hivyo, miradi mingi inatumika bila kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha za kukamilisha miradi hiyo na kufanya azimio hili kutekelezwa kwa 38% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji; uchambuzi wa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kuanzia tarehe 15 hadi 24 Januari mwaka huu, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kupitia programu ya *BOOST,* miradi ya ujenzi wa hospitali za wilaya na miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya halmashauri pamoja na miradi ya ujenzi ya shule za mikoa za sekondari za wasichana. Uchambuzi wa kina wa utekelezaji huo uko kwenye taarifa yetu, lakini hapa nitasema kwa ufupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya ujenzi ya *BOOST; BOOST* ni programu ya kuboresha ujifunzaji katika elimu ya awali na msingi Tanzania Bara. Programu hii ni ya miaka mitano na ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2021/2022 na itatarajiwa kufikia ukomo mwaka 2025/2026. Thamani ya programu hii ni shilingi trilioni 1.15 sawa na dola za Kimarekani milioni 500 ambazo ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Kati ya fedha hizo, dola za Kimarekani milioni 480 zinatolewa kwa utaratibu wa lipa kulingana na matokeo na dola za Marekani milioni 20 zinatolewa moja kwa moja kugharamia shughuli za uendeshaji na uratibu wa programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023; jumla ya shilingi bilioni 230.0 zilitumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye shule 1,338 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za msingi, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu, mabweni na ukarabati wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya ujenzi wa hospitali za wilaya; mwaka 2018/2019 Serikali ilianzisha Mradi wa Ujenzi wa Hospitali za Wilaya. Makadirio ya ujenzi wa hospitali hizi ilikuwa ni shilingi bilioni 6.92 kila hospitali. Mwezi Mei, 2023 Serikali

ilifanya tathmini mpya na gharama mpya za kukamilisha majengo ya hospitali hizo zikawa ni shilingi bilioni 7.58 badala ya bilioni sita niliyoitaja hapo awali. Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali za halmashauri, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 374.86.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya ujenzi ya majengo ya utawala; katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 167.2 katika halmashauri 122 kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo. Hadi tunawasilisha taarifa hii leo, kati ya halmashauri 122 ambazo zilipokea fedha toka mwaka 2022, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala, ni halmashauri 66 pekee ambazo majengo yake yamekamilika na yanatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya ujenzi wa shule za mikoa za wasichana; ujenzi wa shule mpya za sekondari za wasichana za mikoa umetekelezwa chini ya mpango wa elimu ya *SEQUIP* unaosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, hali kadhalika na huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa fedha za dola za Kimarekani milioni 500 sawa na shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyotengwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa shule za bweni ni shilingi bilioni nne kwa kila shule, lakini gharama hizi ziliongezeka hadi shilingi bilioni 4.1 baada ya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha ambao tunatoa taarifa Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 72. Hadi tunawasilisha taarifa sasa hivi ni shule moja tu ya Mkoa wa Ruvuma ndiyo iliyokamilika kwa 100% na shule 25 za mikoa iliyobaki zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kupitia programu zilizotajwa hapo juu. Changamoto za kiujumla; kuhusu changamoto ya mtiririko wa fedha za miradi, baadhi ya halmashauri zimeshindwa kukamilisha miradi kwa wakati kutokana na fedha za miradi hiyo kuchelewa kutoka Serikali Kuu tofauti na mikataba ambayo

halmashauri zimeingia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika. Hali kadhalika, halmashauri ambazo zina mazingira ya tofauti na zile zilizo pembezoni ambazo vifaa vya ujenzi havipatikani kwa urahisi hivyo kuwa na gharama kubwa za ujenzi, kupata fedha za miradi sawa sawa na halmashauri ambazo hazina changamoto hiyo. Kamati imebaini changamoto ya Hazina kutoa fedha kwa baadhi ya halmashauri katika muda unaokaribia mwisho wa mwaka na fedha kuzirejesha Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa linalogusa halmashauri karibia zote. Tulitaka Hazina itoe taarifa ambazo fedha za halmashauri zimerudi katika mwaka huu husika. Hazina haijaletea Kamati, Bunge ikaiandikia barua Wizara ya Fedha, lakini mpaka sasa hatujapata majibu ya hili. Kwa hiyo, ni kiashiria cha dharau kubwa kwa Kamati ya Bunge, lakini kwa dharau kubwa kwa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya halmashauri kuomba kurejeshewa fedha hizo ili iweze kuendelea na utekelezaji wa miradi, kumekuwa na kusuasua kwa urejeshwaji wa fedha hizo na halmashauri nyingine kutorejeshewa fedha hizo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutofanyika tathmini na ufuatiliaji wa miradi; kukosekana kwa usimamizi wa karibu wa miradi bado ni tatizo linalopelekea kukosa ubora. Hii tumeizungumza sana, lakini bado ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miongozo inayotolewa kutokuzingatia tofauti ya kijiografia ya halmashauri zote nchini. Kamati inashauri kuwepo kwa vifungu katika miongozo vitakavyowezesha baadhi ya halmashauri zenye mazingira tofauti kutekeleza miradi kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu wa Kamati unatokana na ukweli kwamba halmashauri zote zimekuwa zikielekezwa kutumia aina moja ya vifaa vya ujenzi bila ya kuzingatia hali halisi ya upatikanaji wa vifaa hivyo kwa baadhi ya halmashauri hasa zilizopo pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kukamilika kwa miradi; Kamati imebaini sababu ni zifuatazo:-

(i) Fedha za miradi kutopatikana kwa wakati;

(ii) Utendaji usioridhisha wa wakandarasi na mafundi;

(iii) Kukosekana kwa usimamizi wa miradi; na

(iv) Fedha za miradi kutumika kinyume na malengo kwa kutaja baadhi; na *(Makofi)*

(v) Kukosekana kwa muunganiko baina ya Taasisi za Serikali kwa mfano *TARURA, TANROADS,* Mamlaka za Maji, *TANESCO* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto ya taasisi za umma kutoshirikiana katika kufanikisha utekelezaji wa miradi; changamoto hii imekuwa ikiongeza gharama za miradi kutokana na halmashauri kufanya shughuli ambazo kimsingi zilifanywa na kutekelezwa na taasisi husika. Tulisema hapa mwaka jana Serikali hamzungumzi na katika utekelezaji wa miradi ya halmashauri taasisi za umma hazizungumzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la uchaguzi usiosahihi wa maeneo ya miradi; kuna changamoto kubwa ya upungufu wa rasilimali watu, kuna changamoto kubwa ya dosari katika taratibu za malipo ya wakandarasi. Hii ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi anatakiwa kuandaa maombi ya malipo kulingana na kiasi cha kazi iliyotekelezwa na kuwasilisha madai yake kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Baada ya Kamati ya Fedha kufanya kikao ili kujiridhisha juu ya maombi ya mkandarasi na kuidhinisha malipo hayo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, twende kwenye mapendekezo…

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa sawa, naomba nimalizie hii halafu naenda kwenye mapendekezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye mapendekezo tunakwenda kwa *time*. Ndiyo Bunge lilivyo, *time*.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; kuhusiana na changamoto ya mtiririko wa fedha za miradi;

Kwa kuwa, kumekuwepo na changamoto ya mtiririko wa fedha za miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu na ambayo malipo ya hati *(certificates)* yanafanywa moja kwa moja na Hazina pamoja na fedha kuchukuliwa na Hazina kabla ya ukamilishaji wa mradi;

Na kwa kuwa, fedha za miradi hazipatikani kwa wakati kumesababisha baadhi ya miradi kutekelezwa kwa kusuasua na kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na mapokezi ya fedha za miradi hiyo kuchelewa tofauti na mikataba;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ihakikishe fedha za miradi zinatolewa kulingana na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge na kwa muda uliopangwa na mkataba;

(ii) Wizara ya Fedha ihakikishe fedha za miradi zilizovutwa zinarejeshwa katika halmashauri husika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili ziweze kukamilisha miradi husika;

(iii) Kwa miradi itakayotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe utoaji wa fedha za miradi unazingatia jiografia za halmashauri husika, upatikanaji wa vifaa pamoja na gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutofanyika kwa tathimini na ufuatiliaji wa mara kwa mara: -

Kwa kuwa, kumebainika kukosekana kwa usimamizi wa karibu wa miradi inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

Na kwa kuwa, hali hiyo imesababisha baadhi ya miradi kukosa ubora unaotakiwa;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Ofisi za *RAS* zifanye tathmini na ufuatiliaji wa miradi yote inayotekelezwa katika halmashauri zote na kuwasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI taarifa hizo kila robo ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miongozo inayotolewa kutozingatia tofauti ya kijiografia: -

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali ambayo haizingatii tofauti ya kijiografia;

Na kwa kuwa, maelekezo hayo yamesababisha halmashauri zenye mazingira tofauti kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati na kwa ufanisi;

Hivyo basi, Bunge linaazimia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe miongozo inayotolewa inatoa fursa kwa halmashauri ambazo zina mazingira ya kipekee kuweza kutekeleza miradi hiyo kulingana na hali halisi ya mazingira yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kukamilika kwa miradi: -

Kwa kuwa, Kamati imebaini ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi na miradi kutokamilika kwa wakati;

Hivyo basi, Bunge linaazimia;

(i) Serikali ihakikishe inakamilisha miradi yote viporo kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya ili lengo la uanzishwaji wa miradi hiyo liweze kufikiwa; na *(Makofi)*

(ii) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* afanye ukaguzi wa kina kwa miradi yote yenye changamoto ambayo imejengwa na Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* na kubainisha iwapo kuna thamani ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukosekana kwa muunganiko baina ya Taasisi za Serikali: -

Kwa kuwa, kumekuwa na changamoto ya taasisi za umma kushirikiana na changamoto hii imekuwa ikiongeza gharama za miradi kwa halmashauri;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ihakikishe kwa miradi itakayotekelezwa kuanzia 2025/2026, taasisi zote za umma zinazotoa huduma katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, zinashirikiana katika kuandaa miundombinu muhimu kama barabara, umeme na maji kabla ya kuanza wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchaguzi usio sahihi wa maeneo: -

Kwa kuwa, baadhi ya halmashauri zimekuwa zikitekeleza miradi bila ya kufanya tathmini ya kina ya kimazingira;

Na kwa kuwa, kutofanyika kwa tathmini ya mazingira kumesababisha baadhi ya halmashauri ama miradi kutekelezwa

katika maeneo ambayo si rafiki, yenye mabonde au miinuko hivyo kuongeza gharama;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya *RAS* ihakikishe inafanya uchambuzi wa kina wa maeneo ambayo miradi inatarajiwa kutekelezwa kabla ya kutoa fedha za utekelezaji wa miradi. Vilevile kila halmashauri ifanye tathmini ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa rasilimali watu: -

Kwa kuwa, Ripoti ya *CAG* imebainisha upungufu wa watumishi wanaotakiwa kutoa huduma kwa wananchi hasa kada ya afya;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa watumishi hao kunasababisha dhamira ya ujenzi wa majengo kutokuwa na maana;

Hivyo Basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ihakikishe kunakuwa na rasilimali watu wa kutosha kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi kulingana na mahitaji ya maeneo husika na miundombinu iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutozingatia taratibu za ulipwaji wa malipo ya wakandarasi: -

Kwa kuwa, *CAG* amebainisha changamoto ya malipo yanayofanyika kwa wakandarasi ambayo ni kutozingatiwa kwa taratibu za malipo, ikiwa ni pamoja na wakandarasi kulipwa kabla ya utekelezaji wa mradi;

Na kwa kuwa, kukiukwa kwa taratibu za malipo kumesababisha miradi kutotekelezwa kwa wakati;

Hivyo Basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali ihakikishe inachukua hatua za haraka juu ya taratibu za malipo zinazofanywa kwa wakandarasi waliotekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri za Kiteto, Kibiti na Ifakara; na

(b) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina katika miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya halmashauri iliyotekelezwa katika Halmashauri za Kiteto, Kibiti na Ifakara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ya Mitaa na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyotolewa kwenye taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**13 FEBRUARI, 2025**

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutupatia fursa ya kukutana leo ndani ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Februari, 2025 ili iweze kujadiliwa.

### 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka mzima, ulizingatia matakwa ya Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, majukumu ya Kamati hii ni yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

## 1.3 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, uandaaji wa Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni umetamkwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa muktadha huo, Muundo wa Taarifa hii umefafanuliwa katika Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ambapo, Taarifa itakuwa na Sehemu ya kwanza inayojumuisha maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati, njia au mbinu na rejea zilizotumika wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Sehemu ya Pili ya Taarifa hii inafafanua kwa kina kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 kuhusu utekelezaji wa miradi ya BOOST, ujenzi wa majengo ya Utawala ya Halmashauri, ujenzi wa Hospitali za Wilaya na ujenzi wa Shule za Mkoa za wasichana iliyotekelezwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Uchambuzi wa eneo hili ndio msingi wa Sehemu ya Tatu yenye maoni na mapendekezo ya Kamati.

## 1.4 Njia zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kukidhi matakwa ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 inayotaka sehemu ya kwanza ya Taarifa kuonesha njia na

mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati, naomba kutaja njia na mbinu hizo kama ifuatavyo:-

a) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa fupi za CAG (*Briefs*) ambazo zinaonesha utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati, Hoja za ukaguzi na Mapendekezo ya CAG katika Halmashauri husika;

b) Mahojiano na Maafisa Masuuli/Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu hoja zilizobainishwa katika Ripoti ya CAG ili kubaini chimbuko la dosari pamoja na athari iliyotokana na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za wakaguzi, majibu ya Wakurugenzi wa Halmashauri iliyokaguliwa pamoja na mashauriano na wadau wengine kuhusu hoja za Ukaguzi zilizojitokeza;

d) Ziara za ukaguzi wa ufanisi katika miradi ya maendeleo ili kubaini thamani ya fedha ya utekelezaji wa miradi hiyo; na

e) Semina na mafunzo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, utumiaji wa njia na mbinu hizo uliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kubaini iwapo Sheria, Kanuni na Miongozo imezingatiwa na Halmashauri zinazohusika kwa lengo la kulishauri Bunge hatua za kuchukua. Katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, Kamati ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma (Sura ya 418) na Kanuni zake za Mwaka 2009;

c) Sheria ya Fedha za Halmashauri (Sura ya 290) na Mwongozo wa Matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa (*the Local Government Financial Memoranda*);

d) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) na Kanuni zake, (kama zilivyo boreshwa mwaka 2016);

e) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na Kanuni zake, 2015;

f) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, Sura 296;

g) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023; na

h) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

## 1.5 Muhtasari wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kukidhi matakwa ya Katiba, Sheria pamoja na Kanuni za kudumu za Bunge, Katika kipindi cha mwaka mzima, Kamati imetekeleza majukumu yake kwa kufanya uchambuzi wa Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ambapo Taarifa yake iliwasilishwa Bungeni mnamo tarehe 29 Oktoba, 2024.

Vile vile, mwezi Machi, 2024 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi katika miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Katika kipindi cha Januari, 2025, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa miradi ya BOOST, ujenzi wa majengo ya Utawala ya Halmashauri, ujenzi wa Hospitali za Wilaya na ujenzi wa Shule za Mkoa za wasichana.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

## 1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Februari, 2024 Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) iliwasilisha Taarifa yake Bungeni kuhusu shughuli za Kamati zilizotekelezwa kwa mwaka 2023. Katika Taarifa hiyo, Jumla ya Mapendekezo Nane (8) yalitolewa na baadae kuwa ni maazimio ya Bunge. Katika kufanya ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge, Tarehe 14 Januari, 2025, Kamati ilikutana na CAG pamoja na Ofisi ya Raisi TAMISEMI ili kupokea, kujadili na kuchambua utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya LAAC kwa kipindi cha Mwezi Februari, 2023 hadi Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kifungu cha 14(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio iliwasilishwa mbele ya Kamati baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupokea majibu ya Serikali na kuyahakiki kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali. Majibu hayo yakiwa na vielelezo yalipokelewa na CAG Mwezi Disemba 2024 kwa ajili ya uhakiki. Aidha, Taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ni kiambatisho namba moja cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa uwasilishwaji wa Taarifa hii, Kamati ilijikita zaidi kuangalia Maazimio ambayo utekelezaji wake haujakamilika kwa Asilimia 100 na kupata maelezo kutoka OR – TAMISEMI juu ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukamilisha utekelezaji wa maazimio hayo. Matokeo ya utekelezaji kwa ujumla yanaonekana katika jedwali Namba 1.

**Jedwali na. 1: Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

| MAAGIZO YA BUNGE | IDADI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| **Maazimio yaliyotolewa na Bunge tarehe 15 Februari, 2024** | | |
| Mazimio yaliyotekelezwa kikamilifu | 1 | 10 |
| Maazimio yaliyo katika hatua | 9 | 90 |

| | | |
|---|---|---|
| ya utekelezaji | | |
| Maazimio yasioyotekelezwa | 0 | 0 |
| **Jumla ya maazimio yaliyotolewa** | **10** | **100** |

**Mheshimiwa Spika**, uhakiki uliofanywa na CAG katika majibu yaliyowasilishwa na Serikali katika kila kipengele cha azimio, ulijikita katika kujiridhisha iwapo maazimio yametekelezwa kikamilifu na vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali vinakidhi matakwa ya kikaguzi. Maazimio ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

**(a) Kuhusu Gharama za Utekelezaji wa Miradi zisizoakisi uhalisia**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya gharama halisi zilizotumika katika kutekeleza miradi kwa kutumia njia ya force account na kubainisha iwapo lengo lililokusudiwa la kupunguza gharama limefikiwa.

Azimio hili limetekelezwa kwa **Asilimia 60** ambapo, nyaraka za kuonesha uchambuzi wa gharama uliofanyika katika Halmashauri kumi ziliwasilishwa kwa CAG na kuhakikiwa. Hata hivyo, hakuna taarifa rasmi iliyowasilishwa inayobainisha vigezo vya uteuzi wa Halmashauri hizo, iwapo zinawakilisha kikamilifu miradi yote iliyotekelezwa, au namna uchambuzi huo ulivyofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Azimio lingine lililotolewa katika eneo hili ni kwamba, Serikali ihakikishe gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi zinajumuishwa katika fedha zinazopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya force account katika kila Halmashauri.

Azimio hili pia limetekelezwa kwa **Asilimia 80** ambapo, Serikali imewasilisha kwa CAG bajeti ya Shilingi Bilioni 8.6 kwa mwaka wa fedha 2024/25 kugharamia usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri, kwa

kiwango cha Shilingi Milioni 30 hadi 100 kwa kila Halmashauri. Vile vile, Serikali imewasilisha kwa CAG taarifa ya kiasi cha Shilingi Bilioni 8.1 kilichotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Disemba, 2024 Kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi yote.

**(b) Kuhusu Upungufu wa Wataalamu wa Kada ya Uhandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo katika Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusiana na upungufu wa wataalamu, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaongeza idadi ya wataalamu (wahandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo) katika Halmashauri zote nchini zenye upungufu wa wataalamu hao ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi. Azimio hili limetekelezwa kwa **Asilimia 70** kwa kuwa, Licha ya Serikali kuajiri wataalamu wa kada ya Uhandisi, Wakadiriaji Majenzi, na Wasanifu Majengo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha 2021/22 na 2022/23, bado kuna upungufu wa wataalamu hawa katika Halmashauri kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Kamati.

**(c) Kuhusu Kutofanyika kwa Tathmini ya Mahitaji ya Miundombinu Muhimu kabla ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya mahitaji ya miundombinu muhimu na kuhakikisha Mamlaka zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme zinashirikishwa kabla ya utekelezaji wa mradi katika maeneo yao. Utekelezaji wa Azimio hili unaendelea na umefikia **Asilimia 70** ambapo, Taarifa ya tathmini iliyowasilishwa kwa CAG kwa ajili uhakiki imebaini uwepo wa miradi 20 yenye thamani ya **Shilingi 7.5 Bilioni** katika sekta za Elimu na Afya ambayo haitumiki kutokana na changamoto za ukosefu wa umeme, maji, na Barabara ambapo changamoto hizo zinatarajiwa kutatuliwa kati ya Mwezi Januari hadi Juni, 2025.

**(d) Kuhusu Ubora usiokidhi vigezo wa Miradi inayotekelezwa kwa force account**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ihakikishe kila Mkurugenzi anafuata taratibu za ujenzi kwa kutekeleza mambo yote muhimu kama upimaji wa udongo, tathmini ya mazingira, ununuzi wa vifaa vyenye ubora, kutumia mafundi wenye taaluma ya mradi husika na kuwachukulia hatua stahiki wote watakaokiuka taratibu hizo. Azimio limetekelezwa kwa **Asilimia 70** ambapo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwachukulia hatua wakurugenzi na kutoa mafunzo kwa maafisa wa ngazi za mikoa na Halmashauri kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge pia lilitoa azimio juu ya Serikali kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa kwa kutumia force account na kukokotoa gharama za uchakavu wa miradi hiyo, kama ilivyoelezwa kwenye mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali pamoja na kuchukua hatua kwa watendaji wote watakaobainika kutekeleza miradi chini ya viwango. Utekelezaji wa Azimio hili umefikia **Asilimia 20** ambapo, Serikali imeeleza kuanza taratibu za ufuatiliaji wa miradi yote iliyo chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Spika**, Azimio lingine katika eneo hili liliitaka NAOT kufanya ukaguzi wa kina juu ya ubora wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account kwa kuzingatia uhai wa mradi (economic life) kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali. Kuhusu utekelezaji wa Azimio hili, CAG ameitaarifu Kamati kuwa, utekelezaji umefikia **Asilimia 60** ambapo, kwa kutumia Mpango kazi 2024/25 ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweka kaguzi za kiufundi kwenye miradi na kaguzi maalum ambapo kaguzi hizi zikikamilika taarifa itatolewa kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyopo.

**(e) Kutozingatiwa kwa Hatua za Kitaalamu za Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliitaka OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ihakikishe miradi yote inayotekelezwa katika Halmashauri inazingatia hatua zote za kitaalamu za ujenzi na kuchukua hatua kwa wataalamu watakaobainika kukiuka taratibu za ujenzi. Azimio limefikia **Asilimia 80** kwa Serikali kuanza utekelezaji wa azimio hili kwa kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote. Pamoja na kwamba maelekezo yametolewa hakuna mwongozo unaowaongoza viongozi wa mikoa na Halmashauri ni hatua zipi wachukue pindi yanapotokea maelekezo ya ziada yaliyo kinyume na matakwa ya kitaalamu yaliyo kwenye miongozo mbalimbali.

**(f) Kuhusu Ukiukwaji wa Mwongozo wa utekelezaji wa Miradi kwa Kutumia Njia ya Force account**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizobainika, Bunge liliazimia kwamba, Serikali (OR –TAMISEMI na PPRA) ichukue hatua stahiki kwa watendaji wote waliokiuka Mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account (Guideline for Carrying out Works under Force Account 2020). Katika eneo hili, Serikali imetekeleza kwa **Asilimia 50** kwa kuwa, imeanza kuchukua hatua kwa Halmashauri zilizobainika kukiuka Miongozo inayotolewa na Serikali na barua za kuanza uchunguzi husika kutoka PPRA zimehakikiwa na CAG.

**(g) Kuhusu Ukiukwaji wa Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI**

**Mheshimiwa Spika**, Azimio la Bunge lilikuwa ni kuitaka OR - TAMISEMI ihakikishe inasimamia na kuchukua hatua dhidi ya watendaji watakaobainika kukiuka miongozo iliyotolewa. Serikali imeanza utekelezaji kwa kumuandikia Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU juu ya kufanyika kwa uchunguzi wa maeneo yenye dosari. Utekelezaji umefikia **Asilimia 60**, hata

hivyo, hakuna mrejesho wa kimaandishi kutoka TAKUKURU juu ya ukamilishaji wa uchunguzi.

**(h) Kuhusu Sekretarieti za Mikoa kutofuatilia utekelezaji wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto moto nyingi zilizobainika katika ufuatiliaji wa miradi, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Makatibu Tawala Mikoa katika kusimamia miradi yote ya maendeleo katika mikoa yao na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao watabainika kutotekeleza wajibu wao kikamilifu hasa katika eneo la kusimamia miradi yote ya maendeleo. Serikali imetekeleza Azimio hili kwa **Asilimia 50** kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji. Hata hivyo, ripoti ya tathmini inayobainisha mapungufu ya utendaji kazi wa Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa katika kusimamia miradi yote ya maendeleo na namna ya kutatua changamoto zilizojitokeza haijawasilishwa.

**(i) Kuhusu Miradi kutokamilika kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati ili ilete tija, Bunge liliazimia kwamba, OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa kusimamia kikamilifu na kuhakikisha miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account ambayo haijakamilika inakamilika kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha ili iweze kutoa huduma iliyokusudiwa. Hadi Desemba 2024, jumla ya miradi 137 (sawa na asilimia 37.5) kati ya miradi 365 iliyohojiwa imekamilika, na miradi 228 bado haijakamilika. Hata hivyo miradi mingi inatumika bila kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha za kukamilisha miradi hiyo na kufanya Azimio hili kutekeleza kwa **Asilimia 38** tu.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya jumla kuhusu uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali yanatekelezwa kikamilifu kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati ya LAAC kwa niaba ya Bunge ilijikita katika kuangalia matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Februari, 2025, Kamati ilitumia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 ili kubainisha na kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu hilo lilitekelezwa kikamilifu kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 14 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la Februari, 2023 kwa njia ya uchambuzi wa taarifa pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina wa maeneo yaliyoshughulikiwa na Kamati katika kipindi kinachotolewa Taarifa ni kama ifuatavyo: -

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Februari, 2024 hadi Februari, 2025, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu

zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya CAG kukamilisha majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati ilipata fursa ya kuipitia na kuichambua Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa na hatimaye Tarehe 29 Oktoba, 2024 maoni na mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa Bungeni na kupelekea kupatikana kwa maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023 ni matokeo ya ukaguzi uliofanywa na CAG katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **184** ambapo kati ya hizo, Halmashauri **181** sawa na **98.37%** zilipata Hati zinazoridhisha za ukaguzi na Halmashauri **3** sawa na **1.63%** zilipata Hati zenye Shaka za ukaguzi. Aidha, katika mwaka huu wa fedha uliokaguliwa, hapakuwa na Halmashauri iliyopata Hati Mbaya ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Mwezi Agosti na Oktoba, 2024, Kamati ilichambua Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za **Halmashauri 55** ambazo ni sawa na **Asilimia 29.89** ya Halmashauri zote 184. Uchambuzi wa Taarifa hizo uliiwezesha Kamati kulitaarifu Bunge juu ya nidhamu ya mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kubainisha maeneo muhimu ambayo Bunge linatakiwa kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mzima kuanzia Februari, 2024 hadi Februari, 2025, Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na jumla ya **Halmashauri 69** na kufanya ziara za ukaguzi wa ufanisi wa miradi ya maendeleo katika **Halmashauri 27** hivyo kufanya jumla ya Halmashauri zote zilizofikiwa na Kamati ndani ya mwaka mmoja kuwa ni **Halmashauri 96** sawa na **Asilimia 52** ya Halmashauri zote 184.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, Maafisa Masuuli (wakurugenzi) walihojiwa na Kamati kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Saba Kamati ilipata fursa ya kipekee ya kuwasilisha Taarifa kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023, uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati katika Mkutano huu wa Bunge utajikita zaidi kwenye eneo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, katika kipindi cha kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 24 Januari, 2025, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kupitia programu ya BOOST, miradi ya ujenzi wa Hospitali za wilaya, miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri pamoja na miradi ya ujenzi wa shule za Mkoa za Sekondari za wasichana. Uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**a) Miradi ya ujenzi kupitia programu ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, BOOST ni Programu ya kuboresha ujifunzaji katika Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara. Programu hii ni ya miaka mitano na ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2021/22 na inatarajiwa kufikia ukomo mwaka 2025/26. Thamani ya programu hii ni **Shilingi Trilioni 1.15** sawa na **Dola za Marekani Milioni 500**, ambazo ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Kati ya fedha hizo, **Dola za Marekani Milioni 480** zinatolewa kwa utaratibu wa lipa kulingana na matokeo na **Dola za Marekani Milioni 20** zinatolewa moja kwa moja kugharamia

shughuli za uendeshaji na uratibu wa Programu (Investment Project Financing – IPF)

**Mheshimiwa Spika**, Programu ya BOOST inatekelezwa kwa ushirikiano wa Wizara mbili ambazo ni Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo inasimamia utekelezaji wa afua za mradi kwenye Mamlaka zote za Serikali za Mitaa (MSM) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inayotoa miongozo na kuweka viwango vya utekelezaji wa afua za programu.

Lengo la utekelezaji wa programu hii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za msingi za Serikali, kuimarisha umahiri wa walimu na ubora wa ufundishaji darasani pamoja na kuimarisha usimamizi wa shule na utawala bora katika Elimu kwenye ngazi ya Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, jumla ya **Shilingi 230,008,000,000** zilitumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye shule **1,338** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za Msingi **302**, vyumba vya madarasa **3,350**, matundu ya vyoo **11,297,** nyumba za walimu **41**, mabweni **2** na ukarabati wa shule **4**.

**b) Miradi ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya za Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ustawi wa wananchi, mwaka 2018/19 Serikali ilianzisha mkakati wa ujenzi wa hospitali za Halmashauri. Katika kutekeleza mkakati huo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya iliandaa michoro ya majengo ya Hospitali za Halmashauri na kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi ambapo, gharama ya kukamilisha ujenzi ilikuwa ni **Shilingi Bilioni 6.92**.

Kutokana na changamoto mbalimbali zilizoibuliwa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, Mwezi Mei, 2023 Serikali ilifanya tathmini mpya ya makadirio ya ujenzi ambapo matokeo ya tathmini hiyo imebainisha gharama mpya ya kukamilisha majengo ya Hospitali hizo kuwa ni **Shilingi Bilioni**

**7.58** badala ya **Shilingi Bilioni 6.92** za awali kwa miundombinu ya majengo 32 ya Hospitali.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ulifanyika kwa awamu ambapo, awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa majengo Saba. Katika awamu hii, kila Halmashauri ilitengewa **Shilingi Bilioni 1.5** kwa ajili ya kuanza kujenga jengo la utawala, jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD), jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la wazazi, jengo la kuhifadhia dawa na jengo la kufulia.

**Mheshimiwa Spika**, awamu ya Pili ya utekelezaji wa mradi ilihusisha ujenzi wa wodi ya watoto, wodi ya wanawake na wodi ya wanaume magonjwa mchanganyiko. Vile vile, Awamu ya Tatu ya mradi ilihusisha ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya upasuaji wanawake, wodi ya upasuaji wanaume na jengo la kuhifadhia maiti na kufanya jumla ya majengo yote yaliyojengwa kwenye Hospitali 67 za awamu ya kwanza kuwa ni majengo 14 ambayo yamegharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 3.1** kwa kila Hospitali.

Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali za Halmashauri, Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi Bilioni 374.86** katika ujenzi wa Hospitali za Wilaya 129, Ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za dharura (EMD) 86, majengo ya kutolea huduma kwa wagonjwa mahututi (ICU) 30 katika Hospitali za Halmashauri na ukarabati wa hospitali kongwe 48 na upanuzi wa hospitali 7 za Halmashauri.

**c) Miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi, Halmashauri ziliibua miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri ambapo miradi hiyo imekuwa ikitekelezwa kwa fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Halmashauri husika.

Wakati wa uanzishwaji wa miradi hiyo, baadhi ya Halmashauri zilitekeleza ujenzi kwa kutumia ramani

zilizoandaliwa na Halmashauri husika. Kutokana na kuwepo kwa changamoto za baadhi ya majengo kuchukua muda mrefu kukamilika kulikosababishwa na ukubwa wa ramani za majengo hayo, Mwaka 2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitoa ramani yenye ghorofa moja kwa ajili ya majengo ya Halmashauri zote. Aidha, Halmashauri zilizoanza ujenzi baada ya kipindi hicho zimeendelea kutumia ramani hizo zilizotolewa na OR – TAMISEMI katika ujenzi wa majengo ya utawala.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi 167,210,474,302.94** katika Halmashauri 122 kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala. Aidha, ujenzi wa majengo haya umekuwa ukifanyika kwa awamu kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha. Ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri umekuwa ukifanyika kwa kutumia mfumo wa Force Account na kwa baadhi ya Halmashauri hutumia Wakandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kuwasilishwa kwa Taarifa hii, kati ya Halmashauri 122 zilizopokea fedha kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala, ni Halmashauri 66 pekee ambazo majengo yake yamekamilika na yanatumika.

**d) Miradi ya ujenzi wa shule za Mikoa za wasichana**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya kuboresha elimu ya sekondari nchini kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari lengo likiwa ni kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana waliopo katika shule za sekondari na kuhakikisha wanafunzi wote wanaoanza masomo ya sekondari wanamaliza elimu hii.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa shule mpya za sekondari za bweni za wasichana za Mkoa umetekelezwa chini ya mradi

wa kuboresha elimu ya sekondari (Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP) unaosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa fedha za Marekani **Dola Milioni 500** sawa na fedha za Kitanzania **Shilingi Trilioni 1.2**.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka wa fedha 2021/22 ambapo kundi la kwanza lilihusisha ujenzi wa shule **10** katika mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mwanza, Singida, Songwe, Njombe, Ruvuma, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Kundi la pili lilihusisha ujenzi wa shule **16** mwaka 2022/23 katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Mtwara, Katavi, Rukwa, Tabora, Mara, Geita, Simiyu, Kigoma, Tanga, Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyotengwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa shule za bweni za wasichana ni **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa kila shule. Aidha, kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi katika maeneo mbalimbali, ofisi ya Rais – TAMISEMI ilifanya mapitio ya gharama na kuongeza kiasi cha **Shilingi 100,000,000.00** kwa kila shule ambapo bajeti ilifikia **Shilingi 4,100,000,000.00.**

Miundombinu iliyopangwa kujengwa katika ujenzi wa shule hizo za Mkoa za wasichana ni pamoja na vyumba vya madarasa **22**, jengo moja la utawala, maabara **4**, matundu **16** ya vyoo, chumba kimoja cha jenereta, bwalo moja, mabweni **9** kwa shule za awamu ya kwanza (mabweni 5 ya wanafunzi 120 na mabweni 4 ya wanafunizi 80 kila moja) na mabweni **12** ya wanafunzi 80 kila moja kwa shule za awamu ya pili, mitaro ya maji, kichomea taka kimoja, matanki ya chini mawili ya maji, matanki mawili ya plastiki, uzio, njia za kutembea, chumba cha wagonjwa kwa shule za awamu ya pili, nyumba tano za walimu, maktaba na chumba cha TEHAMA katika kila shule.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha unaotolea taarifa 2022/2023, Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi 72,559,172,894.25**

katika ujenzi, kati ya fedha hizo, **Shilingi 71,200,000,000.00** zimetolewa kupitia mradi wa SEQUIP ikiwemo **Shilingi 48,000,000,000.00** za awamu ya kwanza ya ujenzi (**Shilingi 3,000,000,000.00** kwa kila shule), **Shilingi 17,600,000,000.00** za awamu ya pili ya ujenzi (**Shilingi 1,100,000,000.00** kwa kila shule).

Vile vile, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi 5,600,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa mabwalo ambapo, **Shilingi 350,000,000.00** imetolewa kwa kila shule. Aidha, **Shilingi 1,359,172,894.25** zimetumika kutoka mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, ni shule moja tu ya Mkoa wa Ruvuma ndiyo iliyokamilika kwa Asilimia 100 na shule 25 za mikoa iliyobaki zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa ujenzi. Licha ya kuwa ujenzi kwa miundombinu ambayo haijakamilika unaendelea, miundombinu muhimu kwa ajili ya kupokea wanafunzi na kuanza masomo imekamilika ikiwemo vyumba vya madarasa, mabweni, matundu ya vyoo, maabara na nyumba za walimu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha miradi inayotekelezwa katika Halmashauri zetu inaleta tija iliyokusudiwa kwa wananchi wa maeneo husika, pamoja na kuliwezesha Bunge kufanikisha jukumu lake la kuisimamia Serikali katika eneo la utekelezaji wa miradi, Kamati imechambua kwa kina utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri, ujenzi wa Hospitali za Wilaya, utekelezaji wa miradi ya ujenzi chini ya mradi wa BOOST pamoja na ujenzi wa shule za Sekondari za mabweni za wasichana. Shughuli hizi za Kamati zimefanyika katika kipindi cha tarehe 13 hadi 24 Januari, 2025 ambapo, katika kipindi hicho, Halmashauri zilizofanya mahojiano na Kamati ni pamoja na: -

a) Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu;
b) Halmashauri ya Mji Babati;
c) Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto;

d) Halmashauri ya Wilaya ya Ngara;
e) Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro;
f) Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa;
g) Halmashauri ya Mji Ifakara;
h) Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko;
i) Halmashauri ya Wilaya ya Mafia;
j) Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti;
k) Halmashauri ya Wilaya ya Songwe;
l) Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa;
m) Halmashauri ya Wilaya ya Meatu; na
n) Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijikita katika kuangalia iwapo kuna thamani ya fedha (value for money) katika miradi ambayo taarifa zake zilijadiliwa na Kamati. Aidha, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati umefafanuliwa kwa kina katika sehemu inayofuata ya Taarifa hii.

### 2.3 Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kupitia programu ya BOOST, Hospitali za Wilaya za Halmashauri, majengo ya utawala ya Halmashauri na shule za Mikoa za wasichana

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 146 (1) na (2) inaeleza madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ambapo pamoja na mambo mengine, ni kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Serikali inatumia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuimarisha maendeleo ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha dhana ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaleta manufaa kwa Taifa, Kamati imefanya vikao na wakurugenzi wa Halmashauri zilizotajwa hapo juu na kufanya uchambuzi wa kina juu ya taarifa za utekelezaji wa miradi ili kubaini juu ya thamani ya fedha za miradi hiyo na iwapo dhumuni la Serikali la utekelezaji wa miradi hiyo limefikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya Kamati kukutana na Halmashauri tajwa, CAG alifanya uhakiki katika miradi yote ya BOOST, majengo ya utawala ya Halmashauri, Hospitali za Wilaya na shule za sekondari za wasichana na kuwasilisha Taarifa za miradi hiyo mbele ya Kamati. Katika Taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kubaini changamoto kadhaa kama ifuatavyo:-

**a) Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya majadiliano ya kina na Maafisa Masuuli (Wakurugenzi wa Halmashauri) kuhusu Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati, yafuatayo yalibainika:-

**(i) Changamoto ya Mtiririko wa fedha za miradi**

**Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa huanzia katika uandaaji wa bajeti ya mradi husika ambapo, Halmashauri huanisha kila mradi utakaotekelezwa katika mwaka unaofuata, muda wa utekelezaji pamoja na chanzo cha fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

Kamati inatambua juhudi za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo, kiasi kikubwa cha fedha kimeelekezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za Elimu, Afya na miundombinu mingineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali kuwekeza katika miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya mtiririko wa fedha hasa kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu na ambayo malipo ya hati madai (certificates) yanafanywa moja kwa moja na Hazina.

Katika eneo hili, baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kukamilisha miradi kwa wakati kutokana na mapokezi ya fedha za miradi hiyo kuwa ni ya kuchelewa tofauti na mikataba ambayo Halmashauri zimeingia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika.

Kucheleweshwa kwa malipo kwa wakandarasi kwa kiasi fulani kunaathiri utekelezaji wa miradi husika kutokana na kukosekana kwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na malipo kwa mafundi pamoja na kuziweka Halmashauri katika hatari ya kutozwa riba ya ucheleweshwaji wa malipo.

**Mheshimiwa Spika**, eneo lingine lililobainika kuwa na changamoto ni kwa baadhi ya Halmashauri ambazo zina mazingira ya tofauti na zile zilizo pembezoni ambazo vifaa vya ujenzi havipatikani kwa urahisi hivyo kuwa na gharama kubwa za ujenzi, kupata fedha za miradi sawa na Halmashauri ambazo hazina changamoto hiyo.

Changamoto hiyo inatokana na kutofanyika kwa uchambuzi wa mahitaji halisi ya fedha za utekelezaji wa miradi kulingana na maeneo husika. Kutofanyika kwa tathmini ya mara kwa mara kunasababisha kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, OR – TAMISEMI imekuwa ikifanya tathmini na kuhuisha gharama za utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, tathmini hiyo imekuwa ikifanyika kikanda na kutoangalia Halmashauri zote kwa upekee wake kwa kuwa, Halmashauri moja katika kanda inaweza ikawa na mahitaji ya kipekee ikilinganishwa na Halmashauri nyingine za kanda hiyo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha za miradi zilizoainishwa katika bajeti zinawasilishwa katika muda uliopangwa na kulingana

na maeneo zilipo Halmashauri ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika utoaji wa fedha za miradi, Kamati imebaini changamoto ya Hazina kutoa fedha kwa baadhi ya Halmashauri katika muda unaokaribia mwishoni mwa mwaka wa fedha. Ili kukidhi matakwa ya kisheria ya utumiaji wa fedha hizo kama taratibu za manunuzi, fedha hizo zimekuwa zikikaa katika Akaunti za Halmashauri hadi mwishoni mwa mwaka bila ya kutumika hivyo kurudishwa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa fedha kurejeshwa Hazina umekuwa ukisababisha miradi kushindwa kutekelezwa kwa wakati uliopangwa. Aidha, licha ya Halmashauri kuomba kurejeshewa fedha hizo ili ziweze kuendelea na utekelezaji wa miradi, kumekua na kusuasua kwa urejeshwaji wa fedha hizo na Halmashauri nyingine kutorejeshewa fedha hizo.

**(ii) Kutofanyika kwa tathmini na ufuatiliaji wa mara kwa mara**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za Makatibu Tawala Mikoa zinapaswa kuhakikisha kunakuwa na ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ili kujiridhisha iwapo fedha za umma zilizoshushwa katika Halmashauri zote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali zimetekeleza kilichokusudiwa na kilichoidhinishwa na Bunge.
Kukosekana kwa usimamizi wa karibu wa miradi kumesababisha baadhi ya miradi kukosa ubora uliostahili kutokana na changamoto mbalimbali ziliyobainishwa na CAG kama ujenzi kinyume na maelekezo yaliyotolewa na OR – TAMISEMI na kutokamilika kwa miundombinu muhimu kwa baadhi ya majengo licha ya majengo hayo kuanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inafahamu juu ya uwepo wa kitengo cha tathmini na ufuatiliaji katika ofisi zote za RAS. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza watendaji wa vitengo hivyo kusimamia kwa karibu na kuhakikisha Sheria, Kanuni na taratibu zote za utekelezaji wa miradi zinafuatwa ikiwa ni pamoja na kujiridhisha juu ya ubora wa miradi hiyo.

Iwapo fedha zitapelekwa bila ya usimamizi madhubuti, Serikali itaingia hasara na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kufanya matengenezo ya miradi ambayo endapo kungekuwa na usimamizi wa karibu, tatizo hilo lingeweza kudhibitiwa.

**(iii) Miongozo inayotolewa kutozingatia tofauti ya jiografia ya Halmashauri zote nchini**

**Mheshimiwa Spika**, OR – TAMISEMI imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kuhusiana na matumizi sahihi ya fedha za utekelezaji wa miradi zinazopelekwa katika Halmashauri zote nchini. Lengo la utoaji wa miongozo hiyo ni kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa miradi, miradi inatekelezwa kama ilivyokusudiwa na tija inapatikana.

Pamoja na dhamira njema ya Serikali katika utoaji wa miongozo hiyo, Kamati inashauri kuwepo kwa vifungu katika miongozo vitakavyowezesha baadhi ya Halmashauri zenye mazingira tofauti kutekeleza miradi kwa wakati na kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuwaepusha na hoja za kikaguzi zinazotokana na kutofuatwa kwa baadhi ya vipengele vya miongozo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri huu wa Kamati unatokana na ukweli kwamba, Halmashauri zote zimekuwa zikielekezwa kutumia aina moja ya vifaa vya ujenzi bila ya kuzingatia hali halisi ya upatikanaji wa vifaa hivyo kwa baadhi ya Halmashauri hasa zilizopo pembezoni.

Mfano wa changamoto kama hiyo imeonekana kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ambayo ipo katika Kanda ya Kaskazini lakini uhalisia uliopo wa maeneo ilipo Halmashauri hiyo ni tofauti na maeneo mengine ya Kanda hiyo. Vile vile, changamoto hiyo imeonekana kwa Halmashauri ya Wilaya ya mafia ambayo upatikanaji wa baadhi ya vifaa ni wa gharama ya juu sana kutokana na uhalisia wa eneo la Halmashauri lilipo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzisaidia Halmashauri zote nchini kufikia lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi wake, ni vema Serikali ikaziangalia baadhi ya Halmashauri kwa namna ya kipekee ili kuondoa hoja za kikaguzi zinazotokana na Halmashauri hizo kushindwa kutekeleza baadhi ya maelekezo kutokana na changamoto zilizopo katika maeneo yao.

**(iv) Kuchelewa kukamilika kwa miradi**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuangalia thamani ya miradi inayotekelezwa katika Halmashauri mbalimbali nchini, Kamati pia imekuwa ikiangalia muda uliotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Lengo likiwa ni kubaini iwapo kuna ufanisi kwa kila mradi ili wananchi waweze kupata manufaa ndani ya muda uliopangwa.

Miradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa kunachelewesha kupatikana kwa faida ya miradi hiyo. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazosababisha miradi mingi kutokamilika katika wakati uliopangwa ikiwa ni pamoja na fedha za miradi kutopatikana kwa wakati, utendaji usioridhisha wa wakandarasi na mafundi, kukosekana kwa usimamizi wa miradi na fedha za miradi kutumika kinyume na malengo kwa kutaja baadhi.

**Mheshimiwa Spika**, wananchi kutopata huduma iliyokusudiwa kutokana na miradi kutokamilika kwa

wakati, kunapunguza tija ya miradi hiyo. Taarifa ya CAG imebainisha sababu mbalimbali za miradi kutokamilika kwa wakati licha ya Halmashauri kupatiwa fedha zote za utekelezaji wa miradi hiyo.

Wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Maafisa Masuuli waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano wamekiri kuwepo kwa changamoto hizo na Kamati imezitaka kuziondoa ili miradi iwe na tija kwa Taifa.

**(v) Kukosekana kwa muunganiko baina ya Taasisi za Serikali katika utekelezaji wa miradi**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya Taasisi za Umma kutoshirikiana katika kufanikisha utekelezaji wa miradi. Changamoto hii imekuwa ikiongeza gharama za miradi kutokana na Halmashauri kufanya shughuli ambazo kimsingi zilipaswa kutekelezwa na Taasisi nyingine.

Ni dhahiri kwamba, miradi mingi imekuwa ikitekelezwa katika maeneo yenye uhitaji ambayo katika kipindi cha utekelezaji wa miradi kunakuwa hakuna miundombinu muhimu kama barabara, maji na umeme. Ili wananchi wa maeneo yote waweze kufikiwa na kupatiwa huduma muhimu, Halmashauri zimekuwa zikilazimika kutumia fedha za miradi kwa ajili ya kutengeneza barabara kuelekea eneo la mradi, jukumu ambalo ni la Mamlaka nyingine (TANROAD au TARURA) Kwa upande wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, Mamlaka za Maji za Wilaya husika zingetumika kufikisha maji eneo la mradi badala ya Halmashauri kuingia gharama ya kuchimba visima au kununua maji kwa gharama kubwa.

Vile vile, changamoto hii imebainika kwa upande wa nishati ya umeme ambapo, fedha za mradi zimekuwa

zikitumika kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya umeme kinyume na maelekezo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hiyo inatokana na Halmashauri kutofanya mawasiliano ya awali na Taasisi husika juu ya dhamira ya kutekeleza miradi katika maeneo yatakayoainishwa ili Taasisi hizo ziweze kutengeneza bajeti ya kuandaa miundombinu muhimu kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kukosekana kwa ushirikiano baina ya Taasisi hizo kunaongeza gharama ya utekelezaji wa miradi, miradi kutokamilika kwa wakati hivyo kuwakosesha wananchi manufaa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali juu ya kuimarisha ushirikiano baina ya Taasisi zake kwa kuwa, lengo la Taasisi zote ni kutoa huduma bora kwa jamii.

**(vi) Uchaguzi usio sahihi wa eneo la mradi**

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa ufuatiliaji kumesababisha baadhi ya miradi kutekelezwa katika maeneo ambayo si rafiki hivyo kuongeza gharama za miradi hiyo. Jambo hili limebainika katika Taarifa zilizowasilishwa na CAG ambapo, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitumia gharama kubwa kuandaa eneo la mradi kutokana na maeneo yaliyochaguliwa kuwa ni ya mabonde au mwinuko jambo ambalo lingeweza kuepukika.

Wakati wa ukaguzi wa miradi, CAG amebaini uwepo wa miradi ambayo imetumia gharama kubwa kutokana uchaguzi usiofaa wa eneo la kutekeleza mradi. Kutozingatiwa kwa vigezo muhimu vya uchaguzi wa maeneo kunakwamisha dhamira ya Serikali ya upatikanaji wa miradi yenye ubora kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hii inaweza ikaondolewa iwapo OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za RAS zitaandaa utaratibu wa kufanya ukaguzi wa maeneo ambayo yamebainishwa na Halmashauri kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi.

Kamati imekuwa ikizitaka Halmashauri zote kuhakikisha zinafanya tathmini ya kina juu ya athari za kimazingira na kufanya usanifu wa maeneo yao ili kujiridhisha juu ya ubora wa maeneo yao na kuepukana na matatizo wakati wa utekelezaji wa miradi.

**(vii) Upungufu wa Rasilimali watu**

**Mheshimiwa Spika**, uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika ujenzi wa miundombinu ya shule na hospitali unapaswa uendane na uwekezaji wa rasilimali watu watakaofikisha huduma bora kwa wananchi. CAG amebainisha uwepo wa upungufu wa watumishi wanaotakiwa kutoa huduma kwa wananchi hasa kwa upande wa kada ya afya.

Upungufu huo umebainika katika Halmashauri mbalimbali ambapo, idadi ya watoa huduma za afya ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya Hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizopo katika Halmashauri hizo.

**Mheshimiwa Spika**, upungufu wa rasilimali watu hasa kwa kada ya afya unatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika ujenzi wa miundombinu muhimu ya afya. Ili miundombinu hiyo iweze kutumika ipasavyo kwa maslahi mapana ya Taifa, Serikali inapaswa kuangalia kwa kina juu ya haja ya kuongeza idadi ya watumishi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa rasimilamali watu kunaondoa thamani ya miradi mikubwa iliyowekezwa katika Halmashauri zetu pamoja na kushindwa kufikia

lengo la utoaji wa huduma. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya uwekezaji katika upande wa rasilimali watu ili lengo la utekelezaji wa miradi liweze kufikiwa kwa maslahi mapana ya nchi.

**(viii) Kutozingatia Taratibu za Ulipwaji wa Malipo ya Wakandarasi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi katika Halmashauri zote nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kumekuwa na dosari kadhaa katika taratibu za malipo ya wakandarasi ambao fedha zao zinalipwa moja kwa moja kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mkandarasi anatakiwa kuandaa maombi ya malipo (certificate) kulingana na kiasi cha kazi iliyotekelezwa na kuwasilisha madai yake kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Baada ya Kamati ya Fedha kufanya kikao ili kujiridhisha juu ya maombi ya Mkandarasi na kuidhinisha malipo hayo, Mkurugenzi atawasilisha maombi hayo Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ambaye naye kwa kushirikiana na Tume ya ushauri wa miradi ya Mkoa watajiridhisha juu ya uhalali wa madai ya Mkandarasi.

Baada ya utaratibu huo kukamilika, hati hizo za madai zitawasilishwa Wizara ya Fedha ili kupata kibali (exchequer) cha kufanya malipo ya Mkandarasi na hela zitaingizwa katika Akaunti husika ya Halmashauri kwa ajili ya kuendelea na taratibu nyingine za malipo.

**Mheshimiwa Spika**, taratibu hizo zimewekwa ili kuondoa changamoto za kufanya malipo ambayo si halali. Hata hivyo, Kamati imebaini baadhi ya Halmashauri kukiuka taratibu hizo kwa kufanya malipo kwa kazi ambazo hazijatekelezwa na wakandarasi kinyume na Sheria na Kanuni za Fedha za Umma. Dosari hiyo imebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya

Kiteto, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na Halmashauri ya Mji Ifakara ambapo kiasi kikubwa cha fedha kimelipwa kwa miradi ambayo haijatekelezwa hivyo kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa matumizi ya fedha za umma zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ili kujiridhisha iwapo kuna thamani ya fedha na kuna matumizi sahihi ya fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa changamoto zilizoainishwa hapo juu unatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano katika kipindi hiki cha Mwezi Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa hoja zilizofafanuliwa hapo juu kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo:-

### 2.3.1 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa ajili ya uchambuzi wa miradi ya ujenzi chini ya BOOST, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pamoja na mradi wa ujenzi wa jengo la Halmashauri kwa kipindi kinachoishia Mwezi Juni, 2023. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika miradi ifuatayo:-

#### (a) Utekelezaji wa Miradi chini ya BOOST

**Mheshimiwa Spika**, Katika miradi iliyotekelezwa chini ya BOOST, Halmashauri ilitekeleza miradi ya ujenzi wa shule mpya ya msingi Flatei Massay (Hydom), shule ya msingi Donga, shule ya msingi Qaloda, shule ya msingi Maretadu Juu na shule ya msingi Qambasirong.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa shule mpya ya msingi ya Flatei Massay (Hydom) ulijumuisha vyumba saba vya madarasa, vyumba viwili vya elimu ya awali, jengo la utawala, matundu Kumi na Sita ya vyoo na kichomea taka kwa gharama za **Shilingi 366,000,000** ambapo kati ya hizi, **Shilingi 17,500,000** ni mchango wa wananchi. Mradi ulitumia njia ya force account na utekelezaji wake ulianza tarehe 6 Juni, 2023 na kukamilika tarehe 3 Septemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliochambuliwa chini ya BOOST ni Ujenzi wa mabweni mawili na nyumba ya Mwalimu 2 in 1 katika shule ya msingi Domanga. Mradi huu wenye gharama ya **Shilingi 373,000,000** (**Shilingi 15,000,000** mchango wa jamii) ulianza kutekelezwa tarehe 5 Juni, 2023 na kukamilika Mwezi Machi, 2024 badala ya tarehe 5 Septemba, 2023 kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, ya mfano ya elimu ya awali na matundu Tisa ya vyoo katika shule ya msingi Qaloda ambayo utekelezaji wake ulianza tarehe 2 Juni, 2023 na umekamilika tarehe 2 Septemba, 2023 kwa kutumia njia ya force Account kwa gharama za **Shilingi 130,315,000** (**Shilingi 4,915,000** mchango wa jamii).

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati ilichambua Taarifa ya mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu Matatu ya vyoo katika shule ya msingi Maretadu Juu wenye gharama ya **Shilingi 62,270,000.** Halmashauri ilitumia njia ya force account ambapo, ujenzi ulianza tarehe 24 Mei, 2023 na kukamilika tarehe 28 Julai, 2023 kukiwa na ongezeko la siku 30.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 81,300,000** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu **Shilingi 75,000,000** na ujenzi wa vyoo matundu matatu **Shilingi 6,300,000** katika shule ya msingi

Qambasirong. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 28 Mei, 2023 kwa kutumia njia ya force account na kukamilika tarehe 27 Agosti, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto za jumla zilizobainika katika miradi ya BOOST ni pamoja na ujenzi wa Paa kinyume na maelekezo ya OR – TAMISEMI, kufanyika kwa manunuzi ambayo hayakuwepo katika mpango wa manunuzi (APP) na dosari kwenye ujenzi wa vyoo kwa wanafunzi wenye ulemavu.

**(b) Utekelezaji wa Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 5,461,283,130.26** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala ambapo gharama za mradi zilizorejewa (Revised) zilikuwa ni **Shilingi 5,620,891,278.80**. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 18 Machi, 2013 na Mkandarasi Mzinga Holdings Company Limited na kutarajiwa kukamilika tarehe 17 Machi, 2023 ambapo tarehe ya ukamilishaji iliyorejewa ni 19 Aprili, 2023.

Awamu ya kwanza ya mradi imekamilika na jengo linatumika, hata hivyo tarehe 30/09/2024 Halmashauri ilipokea **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi kwa awamu ya pili ambapo ilijumuisha ujenzi wa uzio, ununuzi wa samani na ujenzi wa chumba cha mlinzi. Aidha, dosari zilizobainishwa na CAG ambazo Mkandarasi anatakiwa kuzirekebisha ni pamoja na kurekebisha mfumo wa maji safi na maji taka, kurekebisha vigae (tiles) vilivyovunjika kwenye ofisi mbalimbali, kuziba maeneo ya soketi ambazo hazitumiki na kurekebisha lango kuu la kuingilia kwenye jengo.

**(c) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ulijumisha ujenzi wa majengo saba ya Hospital ya Wilaya ya Mbulu ambayo ni wodi ya Mama na Mtoto, OPD, jengo la utawala, jengo la kufulia, jengo la maabara, stoo ya madawa na jengo la mionzi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 01 Machi, 2019 kwa kutumia njia ya force account ambapo kila jengo lilikuwa na Mkataba tofauti na kutakiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2019. Makisio ya gharama za mradi kutoka kwa Mhandisi wa Wilaya yalikuwa ni **Shilingi 2,185,656,642**. Hata hivyo, Halmashauri ilipokea **Shilingi 1,870,000,000** kwa ajili ya utekelezaji kutoka Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inakutana na Afisa Masuuli, Halmashauri ilikuwa inadaiwa na wazabuni **Shilingi 94,642,500** na majengo manne pekee ndiyo yaliyokamilika kwa Asilimia 100 na majengo matatu kutokamilika ambapo, Ujenzi wa wodi ya Mama na Mtoto umefikia Asilimia 65, jengo la utawala Asilimia 60 na jengo la kufulia Asilimia 98. Tarehe 25 Oktoba, 24, Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shilingi 350,000,000** za kukamilisha majengo haya, yaani **Shilingi 240,000,000** kumalizia wodi ya mama na mtoto na **Shilingi 110,000,000** kumalizia jengo la utawala la Hospitali. Umaliziaji wa miradi ndio umeanza na kazi zinaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, awamu nyingine ya mradi huu ilijumuisha ujenzi wa Majengo mengine Matano ya upasuaji, nyumba ya mtumishi (3 in 1), wodi ya upasuaji wanaume, wodi ya wanawake upasuaji, jengo la kuhifadhia maiti (Murtuary) na kichomea taka kwa jumla ya gharama ya **Shilingi 950,014,148**. Majengo yote Matano yalijengwa kwa kutumia njia ya force account na ujenzi ulianza Mwezi Machi, 2022 na kukamilika Mwezi Julai, 2022 na majengo yote yamekamilika lakini manne hayatumiki.

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi huo, Halmashauri ilipokea **Shilingi 500,000,000** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wanaume, wodi ya wanawake na wodi ya watoto kuanzia Mwezi Machi, 2024 na kutarajiwa kukamilika Mwezi Julai, 2024. Hadi kufanyika kwa kikao cha Kamati, majengo yote yalikuwa hayajakamilika na kiasi cha **Shilingi 225,000,000** kinahitajika kumalizia mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa iliyopo katika mradi huu ni kukamilika kwa majengo mengi lakini Hospitali ya wilaya bado haijaanza kutoa huduma za kulaza wagonjwa, kujifungua, upasuaji, huduma za kuhifadhi maiti kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu kama njia za kupita zinazounganisha jengo moja na lingine (Walk ways) na kukosekana kwa vifaa tiba kama taa zinazotumika wakati wa upasuaji hivyo wagonjwa wanaohitaji huduma hizi hulazimika kwenda hospitali ya Hydom ambayo iko mbali sana na kufanya kutofikiwa kwa lengo lililokusudiwa la mradi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya majadiliano ya kina na Afisa Masuuli, CAG na OR – TAMISEMI, ilibainika kuwepo kwa changamoto ya Halmashauri hii kupelekewa fedha sawa na Halmashauri nyinginezo wakati jiografia na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi ni tofauti na maeneo mengine.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Mji Babati

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulifanyika pia katika miradi ya BOOST, Hospitali ya Wilaya pamoja na shule mpya ya Sekondari ya wasichana ya Babati. Katika eneo hili, miradi ifuatayo iliangaliwa:-

**(a) Utekelezaji wa miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Kamati ilifanya uchambuzi wa miradi ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na vyoo matundu sita katika shule ya msingi Hangoni wenye gharama ya **Shilingi 69,100,000** pamoja na ujenzi wa madarasa na vyoo katika shule ya msingi Kiongozi, shule ya msingi Komoto, na shule ya msingi Kwaang'w kwa gharama ya **Shilingi 81,300,000** kwa kila shule moja.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile, Kamati ilichambua Taarifa ya ujenzi wa madarasa tisa, Jengo la utawala, vyoo matundu kumi na sita katika Shule mpya ya mkondo moja S/M Queen Sendiga (Sinai) wenye gharama ya **Shilingi 348,500,000**.

Changamoto zilizobainika katika miradi tajwa hapo juu ni Manunuzi yaliyofanyika katika ujenzi wa shule za msingi Hangoni, Kiongozi, Komoto na Queen Sendiga wenye jumla ya **Shilingi 614,816,485** kutokuwepo kwenye Mpango wa manunuzi.

Changamoto nyingine ni ujenzi wa Paa na uwekeji wa vigae katika shule hizo kufanywa kinyume na maelekezo yaliyotolewa na OR-TAMISEMI pamoja na uwepo wa madeni ya wazabuni walioleta vifaa vya ujenzi katika shule ya msingi Queen Sendiga yenye jumla ya **Shilingi 34,618,625.**

**(b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kama ilivyo katika maeneo mengine, ulijumuisha Ujenzi wa jengo la wodi mama na mtoto kwa gharama ya **Shilingi 608,480,000** (Serikali Kuu Shilingi 500,000,000 na mapato ya ndani Shilingi 108,480,000), Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura **Shilingi 373,782,909** ambapo Serikali Kuu ilitoa

**Shilingi 300,000,000** na **Shilingi 73,782,909** kiliazimwa kutoka katika jengo la mama na mtoto.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri pia ilipokea **Shilingi 1,400,000,000** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa majengo Matano ya mionzi, maabara, jengo la kufulia, Jengo la wagonjwa wa nje na kichomea taka. Makisio ya gharama za mradi kutoka kwa Mhandisi wa Wilaya yalikuwa ni **Shilingi 880,577,460**. Ujenzi wa majengo haya ulitumia njia ya force account ambapo, ulianza Mwezi Februari, 2024 na kutarajiwa kukamilika Mwezi Machi, 2025 baada ya mabadiliko ya muda wa utekelezaji wa mradi.

Hadi Kamati inakutana na Halmashauri hii, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umefikia **Asilimia 97** na kiasi cha fedha kilichotumika kuwa ni **Shilingi 744,138,932.02** na Halmashauri kubakiwa na bakaa ya **Shilingi 655,861,067.98**. Aidha, changamoto ya mradi huu ni kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa majengo kwa wastani wa siku 91-222 na uwepo wa madeni ya wazabuni ambayo hayajalipwa **Shilingi 57,252,000**.

**(c) Utekelezaji wa mradi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana Mkoa wa Manyara**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 31 Mei, 2023, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 3,350,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa awamu ya kwanza ambao ulijumuisha ujenzi wa vyoo matundu kumi na sita na kichomea taka, mabweni nane na samani, nyumba ya mwalimu (2 in 1), maabara ya fizikia, kemia, jiografia na baiolojia, chumba cha wagonjwa, bwalo la chakula, jengo la utawala, chumba cha jenereta, mitaro ya maji, uzio (chain link) mita 350, matenki ya maji aridhini, mashimo ya vyoo na madarasa kumi na mbili na ofisi tatu.

Halmashauri iliingia Mikataba Ishirini na Tatu (23) na mafundi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ulioanza kutekelezwa Mwezi Novemba, 2023 na

ulitarajiwa kukamilika Mwezi Februari, 2024. Hata hivyo, hadi wakati Kamati imekutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri, mradi ulikuwa haujakamilika na wastani wa ukamilishaji wa majengo yote ni **Asilimia 95** na kiasi cha **Shilingi 3,095,861,120.20** kimekwishatumika.

**Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili ya mradi huu ilijumuisha ujenzi wa Mabweni manne na samani, nyumba ya mwalimu (2 in 1), chumba cha computer, maktaba na madarasa kumi na ofisi tatu kwa gharama **Shilingi 1,100,000,000** ambapo Halmashauri iliingia Mikataba Kumi na Nne (14) kwa kutumia njia ya force account. Utekelezaji wa awamu ya pili ulianza Mwezi Oktoba, 2024 na kutakiwa kukamilika Mwezi Januari, 2025.

Aidha, tarehe iliyorejewa ya kukamilisha utekelezaji wa mkataba ni Mwezi, Machi, 2025. Kiasi kilicholipwa hadi Kamati ilipokutana na Afisa Masuuli ni **Shilingi 716,179,934.97** na kubakiwa na bakaa ya **Shilingi 383,820,065.03** ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio na utekelezaji wa mradi umefikia Asilimia 65 kwa wastani wa majengo yote.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni kuwepo kwa ucheleweshaji katika kukamilisha shughuli za mradi, kazi za kiasi cha **Shilingi 139,560,000** hazijafanyika na fedha zake zimeisha na uwepo wa madeni ya wazabuni waliouza vifaa vya ujenzi yenye jumla ya **Shilingi 497,882,500.**

### 2.3.3 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri imetekeleza miradi ya BOOST, Jengo la utawala na majengo ya Hospitali ya Wilaya ambayo Taarifa yake imefanyiwa uchambuzi na Kamati katika kipindi hiki cha Januari. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

## (a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa miradi ya BOOST, Kamati ilichambua miradi mbalimbali ya Ujenzi wa Shule mpya ya mikondo miwili, Shule ya msingi Azimio (Shule Mpya Azimio A) kwa gharama ya **Shilingi 540,300,000** na ulitekelezwa kwa kutumia njia ya force Account. Mradi mwingine uliotekelezwa chini ya Mradi wa BOOST ni mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya mikondo miwili, shule ya msingi chang'ombe (nguzo sita) kwa kutumia njia ya Force Account kwa gharama ya **Shilingi 530,400,000**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulifanyika katika ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na vyoo matundu matatu katika shule za Msingi Ildorokon, Namelock, Chapakazi, na Mbeli, zote kwa gharama ya **Shilingi 81,300,000** kwa kila shule. Miradi hii yote imekamilika na inatumika.

Vile vile, Kamati imefanya uchambuzi juu ya miradi ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na vyoo matundu matatu katika shule ya msingi Zambia kwa gharama ya **Shilingi 106,300,000**, ujenzi wa madarasa ya Elimu ya awali ya mfano katika shule ya msingi Mbigiri kwa gharama ya **Shilingi 69,100,000** pamoja na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya msingi Taigo kwa gharama ya **Shilingi 53,300,000**.

Miradi yote imekamilika na inatumika. Licha ya miradi hiyo kukamilika na kuanza kutumika, changamoto kadhaa zilibainika ambazo ni usimamizi usio thabiti wa miradi hali iliyosababisha shule mpya ya msingi ya Nguzo Sita kutekelezwa katika viwango visivyoridhisha.

Vile vile, Shule saba zilifanya malipo kwa Mafundi ujenzi jumla ya **Shilingi 55,618,875** bila kukata retention yenye thamani ya **Shilingi 2,780,946** kutokana na kutokuwepo kwa kipengele kinachoruhusu makato hayo kwenye mikataba ya mafundi kinyume na Aya ya 25.5 ya

Mwongozo wa Utekelezaji wa Kazi kwa Force Account (Mei 2020).

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa jengo la Utawala**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitekelezwa na Mkandarasi Pacha Construction Co. Ltd kwa kusimamiwa na Mshauri Elekezi Mbeya University of Science and Technology kwa gharama ya **Shilingi 4,621,351,211** (**Shilingi 4,424,124,211** malipo ya Mkandarasi na **Shilingi 197,227,000** malipo ya Mshauri Elekezi). Utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 27 Agosti, 2016 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 27 Februari, 2018. Hata hivyo, kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu, tarehe iliyorejewa ya ukamilishwaji wa mkataba ilikuwa ni terehe 15 Disemba, 2024 na kusababisha kuongezeka kwa muda wa mradi (time extensions) kwa siku 2483 (Miaka 6 na miezi 9).

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji, gharama za mradi pia ziliongezeka kwa **Shilingi 161,405,320.00**. Hadi Kamati inakutana na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, jumla ya **Shilingi 4,507,421,222.35** zilikwishatumika (Shilingi 4,345,969,622.35 malipo kwa Mkandarasi na Shilingi 161,451,600.00 malipo kwa Mshauri elekezi).

Katika mradi huu, majengo yaliyopaswa kujenga ni pamoja na jengo la utawala, kazi za nje, kibanda cha mlinzi, nyumba ya jenereta, ununuzi na uwekaji wa jenereta, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua (nje), uandaaji wa michoro na uandaaji wa nyaraka za zabuni na usimamizi wa ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, thamani ya fedha iliyolipwa kwa Mkandarasi ni **Asilimia 100.11** wakati utekelezaji wa mradi (physical) kwa wastani wa majengo yote ni **Asilimia 90**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa iliyowasilishwa na kubaini dosari kadhaa katika

utekelezaji wa mradi huu. Dosari zilizobainika ni pamoja na Mkandarasi kulipwa fedha pasipo uthibitisho wa kazi kufanyika **Shilingi 184,827,920** kinyume na Sheria, Kanuni na taratibu. Katika eneo hili, ukaguzi ulibaini kuwa, Halmashauri ililipa jumla ya **Shilingi 300,982,670** kwa mkandarasi kupitia Cheti Na. 9 pasipo kazi hizo kutekelezwa. Hata hivyo, tarehe 05 Januari, 2025, CAG alifanya uhakiki na kujiridhisha kuwa, katika malipo yaliyofanywa kupitia Cheti namna 9, kazi za thamani ya **Shilingi 116,154,750** ndizo zilizofanyika na hivyo kazi za **Shilingi 184,827,920** bado hazijafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine iliyobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni uwepo wa kazi tatu zenye thamani ya **Shilingi 231,000,000**, ambazo zipo kwenye mkataba, lakini hazijatekelezwa na hazijalipwa. Licha ya Halmashauri kupokea **Shilingi 300,000,000** kutoka Serikali Kuu na kuchangia **Shilingi 33,000,000** kutoka mapato ya ndani, jumla ya **Shilingi 219,070,011.78** zimetumika kwa kazi ambazo hazikuwa katika mkataba na kubakiwa na kiasi cha **Shilingi 113,929,988.22** kiasi ambacho hakitoshi kulipia kazi ambazo hazijatekelezwa za ujenzi wa Vibanda viwili vya walinzi **Shilingi 8,000,000**, ujenzi wa kibanda cha jenereta **Shilingi 3,000,000** na ununuzi wa jenereta 500-KVA **Shilingi 220,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ya mradi huu ni Mkandarasi kutokamilisha kurejesha kwa fedha za Awali (Advance Payment) **Shilingi 223,247,311.34**. Changamoto hii ilitokana na Mkandarasi kulipwa malipo ya Awali kiasi cha **Shilingi 645,777,667.80** ambapo Mkandarasi ameshalipa kiasi cha **Shilingi 422,530,356.46** (Cheti Na.9) na kiasi cha **Shilingi 223,247,311.34** bado hakijakatwa kwenye malipo aliyowahi kulipwa mpaka sasa. Hata hivyo, dhamana ya malipo hayo imekwisha muda wake tangu 27 Februari, 2018, hivyo Halmashauri haina uhakika wa kurejesha kiasi hicho endapo hakitakatwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, hapakuwa na utaratibu mzuri wa ukataji wa malipo ya awali (Advance payment). Aidha, Kamati ilielezwa kuwa wakati wa mchakato wa kusimamia utekelezaji wa mradi, Mkandarasi alitoa taarifa ya kufilisika (*diclaire bunkrupt*) kabla ya kukamilika kwa mradi.

**(c) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Majengo ya Hospitali**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ilitekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la maabara, jengo la mama na mtoto na jengo la upasuaji kwa kutumia njia ya force account kwa gharama ya **Shilingi 958,990,300** (Fedha kutoka Serikali Kuu Shilingi 900,000,000 na Mapato ya ndani Shilingi 58,990,300) Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 24 Januari, 2023 na ulitakiwa kukamilika tarehe 24 Aprili, 2023. Kulikuwa na ongezeko la muda wa utekelezaji wa mradi kwa siku 189 ambapo tarehe iliyorejewa ya kukamilika kwa mradi ilikuwa ni tarehe 30 Oktoba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, majengo yote matatu yamekamilika lakini jengo la upasuaji halitumiki kwasababu ya kutokamilika kwa njia za kuunganisha majengo (walkways). Hata hivyo, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 200** kwa ajili ya ujenzi wa *walkways*. Kamati inasisitiza juu ya ukamilishaji wa walkways ili jengo la upasuaji liweze kutumika na kuleta tija.

**2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilifika mbele ya Kamati kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa miradi ya BOOST, ujenzi wa jengo la Ofisi ya utawala ya Halmashauri wilaya na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo ni kama ifuatavyo:-

## (a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya utekelezaji wa miradi Kumi na Moja ya BOOST iliyohusisha ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kwenye shule za msingi. Miradi hiyo iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imekamilika lakini kumebainika changamoto chache ambazo ni kutokamika kwa miundombinu ya vyoo katika shule ya msingi Rwinyana pamoja na kutokamilika kwa sehemu za shimo la maji taka katika shule ya msingi Murugaragara.

## (b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri iliingia Mkataba na Mkandarasi Home Africa Investment Corporation Limited kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la ghorofa moja kwa gharama ya **Shilingi 3,599,127,670.69**. Mradi huu ulikuwa unasimamiwa na Mshauri Elekezi Ray Associates Limited (P.O Box 1765 Mwanza) na Jv Gaugepro Consult (T) Ltd (P.O.Box 45848 Dsm). Mradi huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ulitakiwa kuanza tarehe 01 Julai, 2023 na kutakiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa utekelezaji wa mradi huu, kumekuwa na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji wa mradi ambapo tarehe ya ukamilishaji wa mradi iliyorejewa kwa mara ya pili ilikuwa ni tarehe 29 Januari, 2025. Asilimia ya kukamilika kwa mradi (Physical) kwa wastani wa majengo yote ni **Asilimia 94**.

Hata hivyo, Kiasi kilicholipwa (cummulative) hadi kufikia wakati wa kikao na Afisa Masuuli kilikuwa ni **Shilingi 1,848,984,956** sawa na **Asilimia 55** ya gharama zote za mradi. Vile vile, Mkandarasi anadai jumla ya **Shilingi 248,546,232** na Bakaa mpaka kukamilika (Ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio) ni **Shilingi 1,750,142,714.69**. Aidha, changamoto kubwa ya mradi

huo ni kuchelewa kwa malipo ya Mkandarasi kutoka kwa Mfadhili wa mradi huo.

**(c) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilitekeleza mradi huu kwa kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na maabara kwa **Shilingi 550,000,000**, wodi ya wazazi pamoja na jengo la upasuaji kwa **Shilingi 554,000,000**, jengo la utawala, mionzi na jengo la kufulia kwa **Shilingi 840,000,000** (kiasi kilicholipwa ni Shilingi 684,415,781, kiasi ambacho wazabuni wanadai Shilingi 40,000,000 na bakaa mpaka kukamilika ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio Shilingi 115,584,219).

**Mheshimiwa Spika**, dosari zilizobainika katika mradi huu ni kutokamilika kwa miundombinu muhimu kama mabeseni kwa ajili ya matumizi ya wodi ya wazazi na jengo la upasuaji na kutokamilika kwa mfumo wa umeme. Vile vile, jengo la utawala, mionzi na jengo la kufulia bado hayajakamilika.

**2.3.5 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa miradi ya BOOST na ujenzi wa majengo ya Hospitali kwa mwaka wa fedha 2022/23. Matokeo ya Uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilitekeleza miradi mbalimbali kama ujenzi wa darasa moja na matundu matatu ya vyoo katika shule ya msingi Bungo kwa kutumia force account kwa gharama ya **Shilingi 27,400,000.00**, Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu matatu ya vyoo katika shule ya msingi

Kambarage kwa **Shilingi 49,400,000.00**. Miradi mingine iliyochambuliwa ni ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu matatu ya vyoo katika shule ya msingi Kilongo, shule ya msingi Nane Nane, shule ya msingi Muungano na shule ya msingi Kingolwira kwa gharama ya **Shilingi 71,400,000.00** kwa kila shule moja.

Vile vile Halmashauri ilitekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali ya mfano na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi Mgolole kwa gharama ya **Shilingi 60,800,000.00**. Kamati pia iliangalia ujenzi wa shule mpya ya msingi Viwandani yenye mikondo miwili na ujenzi wa shule mpya ya msingi Mgaza kwa **Shilingi 475,300,000.00** kwa kila shule.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto iliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya BOOST ni ujenzi wa miundombinu ya shule mpya ya Mgaza yenye thamani ya **Shilingi 475,300,000** kujengwa katika eneo linalomilikiwa na chuo kikuu cha kilimo Sokoine kutokana na uwepo wa wananchi wengi wanaohitaji huduma katika eneo la Chuo.

**(b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Manispaa.**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilitekeleza ujenzi wa majengo tisa ya Hospitali ya Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya **Shilingi 2,000,000,000.00**. Mradi huu ulijumuisha ujenzi wa jengo la Maabara, jengo la OPD, jengo la wazazi, jengo la mionzi, jengo la Kufulia, jengo la Dawa, jengo la wodi ya wanawake, jengo la wodi ya wanaume na jengo la wodi ya Watoto. Ujenzi wa majengo hayo ulitumia njia ya force account kwa gharama za ufundi **Shilingi 305,531,000**. Utekelezaji ulianza rasmi tarehe 29 Agosti, 2021 na kutakiwa kukamilika tarehe 15 Machi, 2024. Hata hivyo, hadi Kamati inakutana na Afisa Masuuli majengo nane

yamekamilika na yanatumika isipokuwa jengo la wodi ya watoto ambalo lipo hatua ya boma.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha miundombinu ya Hospitali na utoaji wa huduma, Halmashauri inapaswa kuhakikisha inaharakisha ujenzi wa njia za watembea kwa miguu 'walks ways' kwa ajili ya kuunganisha majengo ya hospitali na kurahisisha utoaji na uhamishaji wa wagonjwa kutoka jengo moja kwenda lingine.

**2.3.6 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Kilosa**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vilivyofanyika Mwezi Januari, 2025, Kamati iliangalia utekelezaji wa miradi ya BOOST, ujenzi wa majengo ya Ofisi za Utawala za Halmashauri na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2022/23. Uchambuzi uliangalia yafuatayo:-

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa za miradi ya BOOST zilizowasilishwa mbele ya Kamati zilijumuisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo katika shule ya Msingi Ruaha A na shule ya msingi Madudumizi kwa gharama ya **Shilingi 98,800,000** kwa kila shule moja pamoja na ujenzi wa shule ya mkondo mmoja Ng'apa na shule ya msingi Kidandala kwa gharama ya **Shilingi 306,900,000** kwa kila shule.

Vile vile, Kamati iliangalia mradi wa ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa na matundu nane ya vyoo katika shule ya msingi ya Nyaranda na kwa **Shilingi 124,400,000**, Ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi Myombo kwa **Shilingi 124,400,000**. Mradi mwingine ulioangaliwa ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, vyumba viwili vya

madarasa ya awali na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Mabana kwa **Shilingi 110,200,000**.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa shule ya msingi Misungwi ya mikondo miwili ulifanyika kwa kutumia force account kwa **Shilingi 475,000,000**. Aidha, Halmashauri ilitekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu matatu ya vyoo katika shule ya msingi Machatu na shule ya msingi Unone kwa **Shilingi 49,400,000** kwa kila shule moja.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto ambazo zimebainishwa na CAG katika miradi hii ni ujenzi wa shule tatu mpya za msingi katika viwanja ambavyo Halmashauri bado haina hati miliki na kutoweka vigae (tiles) vyooni, kutokamilisha mfumo wa majitaka vyooni na kutomalizia awamu ya pili mfumo umeme madarasani.

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa majengo ya Ofisi za Utawala ya Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, kupitia zabuni Na. LGA/074/2022-23/w/01, Halmashauri iliingia mkataba na Mkandarasi Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa moja la Utawala la Halmashauri kwa gharama ya **Shilingi 3,775,859,403** (gharama zilizorejewa).

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 11 Agosti, 2023 na ulitarajiwa kukamilika 10 Agosti, 2026. Hata hivyo hadi Halmashauri inafika kutoa maelezo mbele ya Kamati, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umesimama na kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** sawa na **Asilimia 26** kilikuwa kimeshalipwa na utekelezaji wa mradi ulifikia (physical) **Asilimia 22.6**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu, kiasi cha **Shilingi 937,525,397** kati ya **Shilingi 2,937,525,397** zilizopokelewa Mwezi Juni, 2024 kutoka Serikali

Kuu zilirejeshwa Hazina ambapo kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** kimeshatumika.

**Mheshimiwa Spika**, dosari nyingine ya mradi huu ni uwepo wa vifaa vyenye thamani ya **Shilingi 78,087,800** (Nondo, binding wire, misumari, condute pipes) vilivyonunuliwa na kuhifadhiwa kutotumika kwa muda mrefu kwa kuwa mkandarasi ametelekeza mradi. Hali hii inaweza kupelekea vifaa husika kupoteza ubora na kutofaa kwa matumizi ya ujenzi na kuisababishia Serikali kupata hasara.

**(c) Utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, Mkurugenzi wa Halmashauri aliingia mkataba na Mkandarasi Amar Builders Ltd kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya kwa gharama ya **Shilingi 900,000,000**. Mradi huu ulijumuisha ukarabati wa majengo ya OPD, MENO, TB, Walk Way, jengo la upasuaji, wodi ya wanaume, jengo la X-Rays, vyoo, jengo la utawala, wodi ya watoto, pamoja na ujenzi wa maabara. Mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 01 Septemba, 2024 na kupaswa kukamilika tarehe 30 Disemba, 2024. Mpaka Kamati ilipofanya kikao na Halmashauri, jumla ya kiasi cha **Shilingi 292,838,050** kilishalipwa na kubakiwa na bakaa ya **Shilingi 607,161,950** ikijumuisha bakaa ya kipindi cha matazamio na utekelezaji wa mradi kwa wastani wa majengo yote umefikia **Asilimia 35**.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto iliyobainika katika mradi huu ni mradi kutokamilika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ambapo, ukarabati wa jengo la OPD, kinywa na meno, TB, Walk Way, upasuaji, wodi ya wanaume, jengo la X-RAYS, vyoo, jengo la utawala na wodi ya watoto bado haujaanza kutekelezwa.

Aidha, Mkurugenzi ameieleza Kamati kuwa, ucheleweshwaji huu umechangiwa na kuchelewa kufuatilia msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT Exemption).

### 2.3.7 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Mji Ifakara

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, mradi wa jengo la Utawala la Halmashauri na miradi ya BOOST ulifanyika ili kubaini tija ya miradi hiyo. Maeneo yaliyoangaliwa ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipatiwa **Shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), jengo la maabara, kichomea taka, jengo la uzazi na upasuaji (Martenity Complex), jengo la kufulia, jengo la mionzi na ujenzi wa bohari ya madawa (Pharmacy Building).

Ujenzi wa majengo hayo ulianza tarehe 30 Mei, 2022 kwa kutumia force account na kutakiwa kukamilika tarehe 30 Agosti, 2022. Hata hivyo, Mpaka muda ambao Kamati inakutana na Halmashauri, malipo yalishafanyika kwa **Asilimia 100** lakini kukamilika kwa mradi (Physical) kwa wastani wa majengo yote ni **Asilimia 65**.

**Mheshimiwa Spika**, dosari iliyobainika katika mradi huu ni fedha zote kutumika na majengo kutokamilika kwa wakati uliopangwa na Halmashauri bado inahitaji jumla ya **Shilingi 342,936,168** kukamilisha mradi huu.

#### (b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la utawala

**Mheshimiwa Spika**, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara aliingia mkataba na Mkandarasi Wakala wa Majengo Tanzania - TBA kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala. Mshauri elekezi wa mradi huu alikuwa ni Wakala wa Majengo Tanzania – TBA ambapo, zabuni ya kwanza ilikuwa ni Zabuni Na. LGA/174/2016-2017/BW/32- yenye thamani ya **Shilingi 7,414,582,407**, hata hivyo, muda wa

zabuni hii uliisha pasipo mradi kukamilika na Mkandarasi alishalipwa **Shilingi 4,213,720,101.51**.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri iliingia Mkataba mwingine kwa Zabuni Na. LGA//174/2022-2023/W/03 wenye thamani ya **Shilingi 4,561,995,189**. Zabuni hii ilifanyika kwa kazi ambazo hazikufanyika katika zabuni ya kwanza ambayo muda wake uliisha ambayo nayo muda wake uliisha pasipo mradi kukamilika na Mkandarasi ameshalipwa **Shilingi 502,467,332** na kufanya jumla ya fedha iliyolipwa kwa Mkandarasi kwa zabuni zote mbili kuwa ni **Shilingi 4,716,187,433.51**.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 03 Juni, 2018 na ulipaswa kutekelezwa kwa miaka mitatu hadi tarehe 03 Juni, 2021. Licha ya kiasi tajwa hapo juu kulipwa kwa mkandarsi ambayo ni sawa na **Asilimia 64** ya gharama yote ya mradi, mradi umetekelezwa kwa **Asilimia 47** tu.

**Mheshimiwa Spika**, dosari zilizobainika katika utekelezaji wa jengo la utawala ni mkandarasi kulipwa zaidi ya kiwango cha utekelezaji wa mradi kinyume na Sheria katika hati ya malipo Na.4 kwa kiasi cha **Shilingi 189,584,730** ambapo, kiasi cha **Shilingi 63,194,910** kimesharejeshwa na kubakiwa na deni la **Shilingi 126,389,820** kiasi ambacho hakijarejeshwa hadi sasa. Dosari nyingine ni pamoja na mkandarsi kutelekeza mradi na kutokuwepo eneo la mradi na kutokurejeshwa kwa malipo ya awali (advance payment) **Shilingi 647,754,608** na kufanya jumla ya deni lote kuwa ni **Shilingi 774,144,428**.

**Mheshimiwa Spika**, dosari nyingine iliyobainika ni CAG kushindwa kupata uthibitisho juu wa uwepo wa bakaa ya fedha za mradi na fedha za zuio kwenye akaunti ya Amana **Shilingi 644,260,372**.

### (c) Utekelezaji wa miradi ya BOOST

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya Awali na matundu Sita ya vyoo katika shule ya msingi kanyenja kwa **Shilingi 60,800,000**, na ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu Matatu ya vyoo katika shule ya msingi Udzungwa kwa **Shilingi 71,400,000**.

Vile vile, Kamati ilichambua taarifa za ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu Matatu ya vyoo katika shule ya msingi Mbalaji, shule ya msingi Maendeleo na shule ya msingi Mbasa kwa **Shilingi 49,400,000** kwa kila shule na ujenzi wa shule mpya ya msingi uwanja wa ndege kwa gharama ya **Shilingi 306,900,000**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ambazo zimebainika katika utekelezaji wa miradi hii ni uwepo wa mapungufu katika utekelezaji wa mikataba ya mafundi kwa kuwa kipengele cha 6.1.2 cha mikataba kilitaka kukata fedha za zuio wakati wa kuwalipa mafundi, lakini fedha hizo zilikuwa hazikatwi na hivyo kusababisha kutotimiza masharti ya mkataba kwenye kipindi cha matazamio. Changamoto nyingine ni kutokamilika kwa baadhi ya kazi kama uwekaji wa tiles kwenye vyoo, kutokujenga kichomea taka, mfumo wa maji vyooni na kutokujenga uzio kwenye madarasa ya awali pamoja na miradi kuchelewa kukamilika.

### 2.3.8 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla miradi iliyowasilishwa katika Kamati imegawanyika katika makundi matatu yenye thamani ya jumla ya **Shilingi 8,024,514,637**. Uchambuzi wa kina wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**(a) Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilitumia njia ya force account kwa ajili ya ujenzi wa majengo Kumi na Nne pamoja na ujenzi wa njia za watembea kwa miguu kwa gharama ya **Shilingi 4,101,478,270**. Kwa mujibu wa mikataba ambayo Halmashauri imeingia na mafundi, mradi ulitakiwa kuanza Mwezi Februari, 2022 na kipindi cha utekelezaji wa mradi kwa wastani kilitakiwa kuwa ni miezi Minne.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati ilipokutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri hii, baadhi ya majengo yalikuwa yamekamilika na yanatumika isipokuwa njia za watembea kwa miguu, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la upasuaji. Kutokamilika kwa majengo hayo kulitokana na fedha za mradi jumla ya **Shilingi 410,532,914** ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio kuchukuliwa na mfuko mkuu wa Serikali mwishoni mwa mwaka 2023/24.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2024/25 hadi Disemba, 2024 Halmashauri ilipokea **Shilingi 150,000,000** kati ya **Shilingi 410,532,914** zilizochukuliwa na hivyo mapokezi ya fedha yalikuwa pungufu kwa **Shilingi 260,532,914** kiasi ambacho kilipaswa kukamilisha kazi zilizobaki katika ujenzi wa njia za watembea kwa miguu, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la upasuaji.

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa jengo la ofisi ya Utawala la Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 28 Januari, 2022, Halmashauri ilianza ujenzi wa jengo la Ofisi za Utawala za Halmashauri kwa awamu ya tatu kwa gharama ya **Shilingi 3,300,000,000**. Hadi Mwezi Januari, 2025, jumla ya **Shilingi 3,086,579,380** zimekwishatumika ambapo, jengo la Ofisi za Utawala pekee ndilo lililokamilika na ujenzi wa ukumbi wa

mikutano na uzio wa ofisi za Halmashauri umefikia **Asilimia 87.5** kila moja.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ya utekelezaji wa mradi huu ni **Shilingi 468,840,112** ambayo ni bakaa mpaka kukamilika mradi ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio kuchukuliwa na mfuko mkuu wa Serikali mwishoni mwa mwaka 2023/24. Hata hivyo, katika kipindi cha Mwaka 2024/25 hadi Disemba, 2024, Halmashauri ilipokea **Shilingi 300,000,000** kati ya **Shilingi 468,840,112** zilizochukuliwa na hivyo mapokezi ya fedha kuwa ni pungufu kwa **Shilingi 168,840,112**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine katika utekelezaji wa mradi huu ni kutokurejeshwa kwa malipo yaliyozidi kazi zilizofanyika **Shilingi 237,429,424**. Katika eneo hili, Mwaka 2018/19 Halmashauri iliingia mkataba na M/s Wakala wa Majengo (TBA) namba LGA/139/HQ/2018/2019/W/08 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri awamu ya tatu.

Cheti cha mwisho kilichoambatana na barua yenye Kumb. Na. GC:270/612/VOLIII/127 ya tarehe 24/05/2022 kilionyesha thamani ya kazi zilizofanyika kuwa ni **Shilingi 561,385,887** ambapo Halmashauri ilikuwa imeshamlipa TBA kiasi cha **Shilingi 798,815,311** na kupelekea malipo ya ziada (overpayment) **Shilingi 237,429,424** madai ambayo bado hayajarejeshwa.

**(c) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua miradi mbalimbali iliyotekelezwa kupitia mradi wa BOOST katika shule Kumi na Moja za msingi. Miradi iliyojadiliwa na Kamati ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi Itumbiko kwa gharama ya **Shilingi 72,800,000** na ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi Kiga na shule ya msingi Rutenga kwa **Shilingi 118,200,000** kwa kila shule moja na ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi Kumkobe, Kata ya

Nyamtukuza na shule ya msingi Nyanzuki, Kata ya Kasanda kwa gharama ya **Shilingi 361,500,000** kwa kila shule moja

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine iliyochambuliwa ni ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi Bukirilo, Kata ya Gwanumpu na shule ya msingi Kigarama, Kata ya Kiziguzigu yenye gharama ya **Shilingi 110,600,000** kwa kila moja na ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi Gwarama, Kata ya Gwarama kwa **Shilingi 172,400,000.**

**Mheshimika Spika**, Dosari iliyobainika katika miradi ya BOOST ni miradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa na kusababisha manufaa ya miradi kutopatikana kwa wakati.

### 2.3.9 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati katika Halmashauri hii ni Miradi ya BOOST, ujenzi wa Jengo la Utawala na ujenzi wa Jengo la Wazazi (Martenity Complex) katika Hospitali ya Wilaya. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Utekelezaji wa miradi ya BOOST

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi hii ulihusisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na vyoo matundu Sita katika shule ya msingi Dongo kwa gharama ya **Shilingi 114,456,712**, ujenzi wa shule mpya ya msingi sikula kijiji cha dongo (mkondo mmoja) pamoja na shule mpya ya msingi shalaza kwa gharama ya **Shilingi 306,900,000** kwa kila shule.

Mradi mwingine uliofanyiwa uchambuzi ni ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na vyoo matundu matatu shule ya msingi Baleni kwa gharama ya **Shilingi 71,400,000** pamoja na ujenzi wa nyumba moja (mbili kwa moja), vyumba vitatu vya madarasa na vyoo matundu matatu shule ya msingi Bweni kwa gharama ya **Shilingi 166,400,000**.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa miradi hiyo, changamoto za jumla zilizobainika ni kukosekana kwa uzio kuzunguka madarasa ya awali katika shule ya msingi Dongo, Sikula na Shalaza, kutotengenezwa kwa madawati katika shule za msingi Sikula, Shalaza, Baleni na Bweni pamoja na kutoungwanishwa kwa mfumo wa umeme na maji safi katika shule ya msingi Bweni.

**(b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi wa mikutano**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kupitia Zabuni Na. LGA/008/2017/2018/W/08 iliingia makubaliano na Mkandarasi JV; M/s Samka Contractors Co. Ltd and Jossam & Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi wa mikutano kwa gharama za awali **Shilingi 5,753,527,443.40**. Mshauri Elekezi wa mradi huu alikuwa ni MUST CONSULTANCY BUREAU (MCB) ambapo, utekelezaji ulianza tarehe 13 Julai, 2018 na tarehe iliyorejewa ya ukamilishaji wa mradi ni tarehe 28 Machi, 2025.
Kuongezeka kwa muda wa utekelezaji kuliongeza gharama ya mradi kwa **Shilingi 350,088,510.04** na kufikia **Shilingi 6,103,615,953.44**. Hadi Kamati inakutana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mafia kwa ajili ya majadiliano, kiasi cha **Shilingi 5,684,805,834.10** sawa na **Asilimia 93** kilikuwa kimeshalipwa na utekelezaji wa mradi (physical) umefikia **Asilimia 95**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ya utekelezaji wa mradi huu ni Mkandarasi kutokamilisha kazi kwa wakati hali iliyosababisha kuongezeka kwa gharama za mradi.

**(c) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Jengo la Wazazi (Martenity Complex) katika Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 13 na 16 Januari, 2023, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 270,174,714** kutoka kwa Mfadhili KOFFIH na **Shilingi 250,000,000** kutoka Serikali Kuu mtawalia kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi

(Maternity complex) Hospitali ya Wilaya. Tarehe rasmi ya kuanza kwa mradi ni 28 Mei, 2023 na ulipaswa kukamilika 28 Agosti, 2023.

Mpaka muda ambapo Kamati inakutana na Halmashauri, fedha zote **Shilingi 520,174,714.00** zilikwishalipwa na mradi umekamilika kwa **Asilimia 97** kwa wastani wa majengo yote. Aidha, mradi umesimama kutokana na ukosefu wa fedha ambapo kiasi cha **Shilingi 70,000,000** kinahitajika kukamilisha mradi.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto za utekelezaji wa mradi huu ni kutowekwa kwa vipooza hewa "AC", kutowekwa "granite" kwenye meza za zege ndani ya jengo na kutokamilika kwa uwekaji wa mfumo wa maji taka kulikosababishwa na kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi kutokana na ukosefu wa fedha.

### 2.3.10 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za miradi ya BOOST, ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti zilifanyiwa uchambuzi na Kamati na matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Utekelezaji wa Miradi ya Boost

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa miradi ya BOOST, Halmashauri ilitekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa shule ya msingi Hongo, mkondo mmoja na shule ya msingi Mpembwene mkondo mmoja kwa gharama ya **Shilingi 306,900,000** kwa kila moja. Vile vile, Kamati imechambua Taarifa za ujenzi wa madarasa matatu na matundu manne ya vyoo katika shule za msingi Kilulatambwe na Makima kwa gharama ya **Shilingi 73,200,000** kwa kila shule.
Aidha, Kamati pia imechambua Taarifa za mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali, vyoo matundi

sita na bembea katika shule ya msingi Mlanzi ambavyo ujenzi wake umetumia gharama ya **Shilingi 60,800,000**.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa taarifa za miradi hiyo ya BOOST, changamoto zilizobainika ni mradi wa shule za msingi Itonga na Mpembwene kutokamilika licha ya kuanza kutumika ambapo, viti na meza bado havijanunuliwa na vyuma vya kushikilia watu wenye uhitaji maalumu kwenye vyoo vya jengo la utawala bado havijawekwa.

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti iliingia makubaliano na Mkandarasi SUMA JKT kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri kwa gharama ya **Shilingi 5,358,829,757**. Mshauri ekekezi wa mradi huu ni Aru Built Environment Consulting Company Ltd (ABECC).

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulianza rasmi kutekelezwa tarehe 10 Oktoba, 2017 na kutakiwa kukamilika tarehe 10 Aprili, 2019. Hata hivyo, kumekuwa na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji wa mradi ambapo, tarehe ya ukamilishwaji wa mkataba iliyorejewa ni tarehe 17 Aprili, 2025.

Kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu, hadi Kamati inakutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, mradi huu umetekelezwa (physical) kwa **Asilimia 82** na jumla ya **Shilingi 4,011,763,093** sawa na **Asilimia 75** za gharama za mradi zimekwishatumika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto kadhaa zilizobainishwa na CAG baada ya kufanya uhakiki wa mradi huu, Kamati imebaini ukiukwaji wa taratibu za malipo kwa Mkandarasi ambapo, Halmashauri imekuwa ikinunua vifaa na kuvikabidhi kwa mkandarasi badala ya kufanya

malipo ya moja kwa moja kwa mkandarasi kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa malipo mengine ya nyuma.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya Mradi, Mkandarasi SUMA JKT alimwandikia msimamizi wa mradi ABECC wa Chuo Kikuu Ardhi – Dar Es Salaam ili kubadili njia za malipo kutoka "Certificate" kwenda kwenye utaratibu wa malipo wa "milestone ".

Aidha, Halmashauri iliridhia mabadiliko hayo ya malipo kinyume na taratibu. Kwa muktadha huo, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 389,196,752.70** kutoka Hazina na kuilipa fedha hiyo kwa mkandarasi Suma JKT kwa utaratibu wa Milestone (yaani Halmashauri inanunua vifaa na Mkandarasi analipwa gharama za ufundi pekee)

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine katika utekelezaji wa mradi huu, ni Mkandarasi SUMA JKT kutokuwepo katika enepo la mradi kwa muda mrefu.

**(c) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ulijumuisha ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya wanaume waliofanyiwa upasuaji, wodi ya wanawake waliofanyiwa upasuaji na chumba cha kuhifadhia maiti, mradi huu ulitekelezwa kwa njia ya force account kwa gharama ya **Shilingi 800,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezwaji wa miradi yote tajwa hapo juu ulianza rasmi tarehe 13 Juni, 2022 na ilipaswa kukamilika 13 Septemba, 2022. Licha ya mradi huu kuanza kutumika na malipo yote kufanyika kwa **Asilimia 100**, mradi huu umekamilika (physical) kwa **Asilimia 98** ambapo, shughuli ambazo hazijatekelezwa ni ujenzi wa njia za watembea kwa miguu, ununuzi wa majokofu ya kuhifadhia maiti, mashine ya kusaidia kupumua na vifaa vya usingizi pamoja na kukamilisha sehemu ya kusafishia vifaa vya upasuaji.

### 2.3.11 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songwe

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua Taarifa za miradi ya BOOST, Ujenzi wa jengo la Utawala na Ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2022/23. Uchambuzi huo uliangalia mambo yafuatayo:-

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Kamati ilifanikiwa kuchambua Taarifa za miardi Minne inayotekelezwa na Halmashauri kupitia mradi wa BOOST. Miradi iliyopitiwa na Kamati ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, matundu matatu ya vyoo na nyumba moja ya walimu (2 in 1) katika shule ya msingi Rukwa kwa gharama ya **Shilingi 156,000,000** na ujenzi wa shule ya Msingi ya mikondo miwili kaloleni (shule mpya ya kikuyuni) kwa **Shilingi 538,500,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua taarifa za ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu manne ya vyoo shule ya masingi Kanga kwa **Shilingi 108,000,000** pamoja na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu ya matatu ya vyoo elimu msingi na madarasa mawili pamoja na matundu sita ya vyoo elimu ya awali katika shule ya msingi Namkukwe kwa gharama ya **Shilingi 125,100,000**.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya miradi hiyo kukamilika na kuanza kutumika, dosari zilizobainika ni vyoo viwili vya watu wenye mahitaji maalum vya elimu ya awali kutowekwa milango na upungufu wa viti vya watoto wa awali katika shule ya msingi Namkukwe.

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Jengo la Utawala**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 25 Septemba, 2017 Halmashauri ilianza ujenzi wa jengo la utawala ambapo utekelezaji wa

mradi ulifanyika kwa awamu tatu na kutakiwa kukamilika tarehe 27 Aprili, 2020. Awamu ya kwanza ya utekelezaji ilifanywa na SUMA JKT (kandarasi) kwa gharama ya **Shilingi 471,000,000**, awamu ya pili ilitekelezwa pia na SUMA JKT (kandarasi) kwa gharama ya **Shilingi 999,485,016** na awamu ya mwisho ilitekelezwa na TBA kwa gharama za ujenzi **Shilingi 461,550,472**.

**Mheshimiwa Spika**, mawanda ya mradi huo yalikuwa ni ujenzi wa msingi wa jengo la ghorofa mbili, ujenzi wa nguzo za wima na ulalo; pamoja na sakafu za juu, ujenzi wa kuta za jengo, upauaji, uwekaji wa mifumo ya awamu ya kwanza na ya pili ya umeme, ving'amuzi vya moto na maji pamoja na umaliziaji.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi 5,815,262,000** kwa ajili ya mradi huu na kiasi cha **Shilingi 4,521,458,000** kimekwishatumika. Aidha, kazi zilizosalia katika utekelezaji wa mradi ni ufungaji wa mfumo wa TEHAMA, ving'amuzi vya viashiria vya moto, ufungaji wa viyoyozi, uwekaji na ufungaji wa samani, ununuzi wa jenereta, ujenzi wa kibanda cha walinzi, upakaji rangi katika kuta za uzio, taa za nje (Secuirty Light) na ujenzi wa mgahawa.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Oktoba, 2023 Halmashauri ilipokea **Shilingi 1,293,804,000** kutoka Hazina kwa ajili ya kumalizia kazi zilizoainishwa hapo juu na Halmashauri ililipa kiasi cha **Shilingi 229,455,530** kati ya mwezi Nne na wa Tano. Hata hivyo fedha hizo hazikufika kwa wahusika kutokana na changamoto za mifumo ya malipo. Vile vile, Halmashauri ilikamilisha mchakato wa manunuzi kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA vya **Shilingi 489,928,696**, Vifaa vya Umeme na uzio vya **Shilingi 49,023,500** na Ununuzi wa samani **Shilingi 188,800,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kusuasua kwa malipo, Halmashauri haikuweza kuingia mikataba hiyo ingawa michakato iliishafika mwisho na fedha zote kiasi cha **Shilingi**

**1,293,804,000** kilichukuliwa na Hazina Mwezi Juni, 2024 na hakijarejeshwa.

**(c) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuangalia miradi mingine, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambapo, kulikuwa na ukamilishaji wa ujenzi wa wodi tatu (watoto, wanaume na wanawake) kwa ajili ya magonjwa ya ndani kwa gharama ya **Shilingi 157,921,550** (Shilingi 127,438,696 Bakaa ya fedha ya Serikali Kuu na Shilingi 30,482,850 Mapato ya ndani).

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa Hospitali, Halmashauri ilipokea **Shilingi 218,962,624** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji. Ujenzi umekamilika tarehe 30 Disemba, 2023 lakini jengo hili halitumiki kwa kukosa vifaa tiba ambavyo vimeagizwa Bohari ya Dawa tangu 19 Oktoba, 2023.

Halmashauri pia ilitekeleza ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti kwa gharama ya **Shilingi 125,804,125** kuanza tarehe 01 Februari, 2022 na kukamilika tarehe 01 Mei, 2022. Vile vile, Kamati ilfanya uchambuzi wa ujenzi wa wodi ya upasuaji wanaume na wodi ya upasuaji wanawake kwa fedha kutoka Serikali Kuu **Shilingi 165,397,276** na **Shilingi 162,397,276** mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine iliyofanyiwa uchambuzi ni ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura kwa gharama ya **Shilingi 300,000,000** na nyumba ya watumishi (3 in 1) kwa gharama ya **Shilingi 90,000,000** ambapo miradi hiyo imekamilika na inatumika. Vile vile, Halmashauri ilijenga kichomea taka kwa gharama ya **Shilingi 60,000,000** kuanzia tarehe 5 Agosti, 2023 na kukamilika tarehe 5 Novemba, 2023.

### 2.3.12 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati uliangalia Taarifa za miradi ya BOOST, ujenzi wa jengo la Halmashauri na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Uchambuzi ulijumuisha yafuatayo:-

#### (a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi huu, taarifa zilizochambuliwa ni kuhusu ujenzi wa shule mpya ya Msingi Nyasa (Kilosa) kwa gharama ya **Shilingi 331,600,000** ambapo ujenzi huu umekamilika. Vile vile, Halmashauri imetekeleza mradi wa ujenzi wa shule ya Msingi Marudio na shule ya msingi Chiwindi kwa **Shilingi 77,100,000** kwa kila shule.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia iliangalia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya mfano elimu ya awali, matundu sita ya vyoo, uzio na nyumba ya walimu (2 in 1) katika shule ya msingi Lumeme kwa gharama ya **Shilingi 161,300,000**.

Baada ya uchambuzi wa taarifa hizi, Kamati ilibaini dosari kadhaa ambazo Halmashauri inapaswa kuzirekebisha kama kutokamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji pamoja na kutofungwa kwa mifumo ya kuvunia maji ya mvua katika shule za msingi Nyasa, Marudio, Chiwindi na Lumeme.

#### (b) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 11 Februari, 2019, Halmashauri ilianza ujenzi wa Majengo ya Utawala, OPD, Kufulia, Maabara, Mionzi, Stoo ya Dawa na Wodi ya Wazazi. Mradi huu wenye gharama ya **Shilingi 1,800,000,000** ulipaswa kukamilika 11 Agosti, 2019. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi, tarehe ya ukamilishaji wa mkataba iliyotejewa kwa wastani wa majengo yote ni

Mwezi Aprili, 2020 ambapo, miradi yote imekamilika na imeanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, majengo mengine yaliyojengwa katika mradi wa Hospitali ya Wilaya ni ujenzi wa majengo ya wodi ya wanaume, wodi ya wanawake na wodi ya watoto kwa **Shilingi 491,376,520**. Ujenzi wa majengo haya ulianza tarehe 10 Mei, 2021 na ulipaswa kukamilika Mwezi Septemba, 2021. Hata hivyo, kulikuwa na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji wa miradi kwa wastani wa miezi miwili.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa Hospitali pia ulijumisha ujenzi wa majengo ya upasuaji, wodi ya upasuaji wanaume, wodi ya upasuaji wanawake na jengo la kuhifadhia maiti vyote kwa gharama ya **Shilingi 800,000,000**. Ujenzi wa majengo ulianza tarehe 21 Februari, 2022 na kupaswa kukamilika 20 Julai, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa jengo la huduma za dharura (EMD) uligharimu **Shilingi 300,000,000** kuanzia tarehe 21 Machi, 2022 na kukamilika 24 Agosti, 2022 na mradi umekamilika na unatumika.

**Mheshimiwa Spika**, dosari zilizobainika katika mradi huu ni jengo la kuhifadhia maiti, wodi ya watoto pamoja na wodi za upasuaji wanawake na wanaume kukamilika lakini kutotumika kutokana na ukosefu wa majokofu ya kuhifadhia maiti na upungufu wa watumishi kwenye majengo ya wodi ya watoto na wodi za upasuaji.

Vile vile, dosari nyingine iliyobainika ni kuharibika kwa baadhi ya miundombinu kama kudondoka kwa PVC, Gutters na Gypsum powders kwenye dari kwa majengo ya Utawala, OPD, wodi ya watoto na jengo la Maabara.

**(c) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa jengo la utawala**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ulitekelezwa kwa awamu mbili mbapo, awamu ya kwanza ilifanywa na Mkandarasi TBA (Design and Build)

kuanzia tarehe 22 Juni, 2017 kwa gharama ya **Shilingi 649,694,825.00**.

Katika awamu hii, muda wa utekelezaji wa mradi huu uliongezeka kwa siku 360 ambapo tarehe ya kukamilisha mkataba ni tarehe 13 Disemba, 2018 badala ya muda uliopangwa awali tarehe 18 Disemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili ya mradi ilitekelezwa na Mkandarasi SUMA JKT LINDI kwa gharama za Mkataba wa Ujenzi **Shilingi 2,895,433,294.92** (Bila VAT) na gharama za Mkataba kwa Mkandarasi Mshauri ni **Shilingi 95,621,799**.
Utekelezaji wa mradi katika awamu hii ulianza tarehe 05 Julai, 2019 na kutakiwa kukamilika tarehe 15 Julai, 2020. Hata hivyo, hadi Kamati ilipokutana na Afisa Masuuli, mradi ulikuwa umesimama na jumla ya **Shilingi 3,834,304,762** zimeshalipwa.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto za utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na fedha za mradi za ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa **Shilingi 390,980,442** na kiasi cha **Shilingi 500,000,000** kurudishwa hazina kutokana na kuchelewa kutumika kwenye mradi.

### 2.3.13 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kwa taarifa za miradi iliyowasilishwa ni kama ifuatavyo:-

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, miradi ya ujenzi iliyofadhiliwa na fedha za BOOST yenye jumla ya **Shilingi 970,100,000** ilichambuliwa na Kamati. Miradi hiyo ilijumuisha ujenzi wa shule mpya ya msingi Mwandu Ikindilo ya mikondo miwili iliyojengwa kwa gharama ya **Shilingi 540,300,000**.

Kamati pia ilichambua taarifa za ujenzi wa shule mpya ya msingi Mwanhuzi iliyojumuisha ujenzi wa jengo la utawala, ujenzi wa vyumba saba vya madarasa msingi na Ofisi mbili, ujenzi wa vyoo vya wanafunzi matundu nane, ujenzi wa madarasa mawili ya awali na matundu sita ya vyoo na uzio shule ya awali na ujenzi wa kichomea taka kwa gharama ya **Shilingi 348,500,000**.

Mradi mwingine uliochambuliwa ni ujenzi wa madarasa matatu na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Malugala kwa gharama ya **Shilingi 81,300,000**.

**Mheshimiwa Spika**, dosari zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya BOOST ni kutofuatwa kwa makadirio ya ujenzi (BOQ) Katika ujenzi wa shule mpya ya msingi Mwandu Ikindilo na kupelekea kutowekwa kwa mabeseni mawili ya kunawia mikono.

Dosari nyingine ni ujenzi wa shule mbili mpya za msingi katika viwanja ambavyo Halmashauri haina hati miliki zenye jumla ya thamani ya **Shilingi 888,800,000** na Mikataba mitatu iliyokwisha muda wake na mafundi kuendelea na kazi bila kuwepo na nyongeza ya muda (Extension of time) na kutohuishwa (Renewal) kwa mikataba yenye thamani ya **Shilingi 20,760,000**.

**(b) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ilipokea jumla ya **Shilingi 900,000,000** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Fedha hii ilitumika katika ujenzi wa majengo manne yaani, ujenzi wa jengo la kutolea huduma wagonjwa wa nje (OPD), Jengo la kufulia, kichomea taka na Jengo la maabara.

**Mheshimiwa Spika**, miradi hii haijakamilika na changamoto zilizobainika ni Mikataba mitatu iliyokwisha muda wake na

mafundi kuendelea na kazi bila kuwepo na nyongeza ya muda (Extension of time) na kutohuishwa (Renewal) yenye thamani ya **Shilingi 93,120,000** pamoja na kuchelewa kuanza na kumaliza mradi wa ujenzi wa majengo manne ya Hospitali ya Wilaya.

**2.3.14 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa jengo la utawala, ujenzi wa majengo katika Hospitali ya Wilaya na miradi ya BOOST zilijadiliwa kwa kina na Kamati. Maeneo yaliyoangaliwa ni yafuatayo:-

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya BOOST**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za miradi ya BOOST zilijumuisha ujenzi wa shule mpya yenye mikondo miwili katika shule ya msingi Losirwa kwa **Shilingi 664,300,000** (Shilingi 638,300,000 kutoka Serikali Kuu na Shilingi 26,000,000 ya mapato ya ndani). Mradi mwingine ni ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu matatu ya vyoo katika shule ya Msingi Ololosokwan kwa gharama ya **Shilingi 106,300,000** kutoka Serikali Kuu na ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu sita ya vyoo katika shule ya Msingi Wasso kwa **Shilingi 88,600,000**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizopo katika mradi huu ni ujenzi wa shule mpya ya Losirwa na shule ya msingi Wasso kutokamilika kwa wakati ulipopangwa.

**(b) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri iliingia Mkataba na Mkandarasi M/s Tanzania Building Agency (TBA) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la ghorofa moja, kibanda cha mlinzi (Gate house), kibanda cha kuhifadhi jenereta (Power house), ujenzi wa mandhari (car parking, garden and

road), ujenzi wa uzio (fence) na ununuzi wa samani kwa gharama za **Shilingi 3,149,708,033**.

Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 19 Machi, 2021 na kupaswa kukamilika tarehe 18 Machi, 2022. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kutekelezwa kwa mradi, Tarehe ya ukamilishwaji wa Mkataba iliyorejewa (revised) ilikuwa ni 30 Januari, 2025.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi kulisababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa kiasi cha **Shilingi 371,921,126.98** kulikotokana na kuongeza kwa bei hivyo kufanya mradi kuwa na gharama ya **Shilingi 3,521,629,159.98**. Hadi Afisa Masuuli anafika mbele ya Kamati, kiasi cha **Shilingi 2,887,161,078** kilikwishatumika na utekelezaji wa mradi bado unaendelea.

**(c) Utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Hospital ya Wilaya ya Ngorongoro (Awamu ya Kwanza) ulianza Mwezi Januari, 2019 ambapo ulijumuisha ujenzi wa jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la stoo ya Dawa, jengo la mama na mtoto (RCH) lenye chumba cha upasuaji, jengo la maabara, jengo la mionzi na jengo la Kufulia kwa gharama ya **Shilingi 1,893,000,000**.

Ujenzi wa majengo hayo ulianza 31 Januari, 2019 na kupaswa kukamilika 31 Mei, 2019 kwa kutumia njia ya force account. Aidha, tarehe iliyorejewa ya ukamilishaji wa mkataba ni 31 Agosti, 2019 na gharama za mradi zilizorejewa ni **Shilingi 1,979,749,242.21**. Kiasi kilicholipwa hadi Halmashauri inakutana na Kamati ni **Shilingi 1,893,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Hospital ya Wilaya ya Ngorongoro awamu ya Pili ulijumuisha ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya wanawake na wodi ya wanaume kwa **Shilingi 560,958,310**. Katika awamu hii, ujenzi ulianza tarehe

02 Julai, 2021 na kupaswa kukamilika tarehe 02 Septemba, 2021 hata hivyo, ujenzi wa awamu ya pili bado unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa hospitali ya wilaya awamu ya tatu ulijumuisha ujenzi wa majengo manne ambayo ni jengo la upasuaji, wodi ya wanawake upasuaji, wodi wanaume upasuji na jengo la kuhifadhia maiti ambapo, gharama ya majengo yote ni **Shilingi 1,042,694,360** na mradi upo katika hatua za umaliziaji.

**Mheshimiwa Spika**, awamu nyingine ya utekelezaji wa mradi (awamu ya nne) ni ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura na nyumba ya watumishi (3 kwa 1). Majengo haya yalijengwa kwa **Shilingi 573,105,330** na kiasi kilicholipwa hadi wakati wa kikao ni **Shilingi 464,761,165**. Vile vile, katika awamu ya Tano, Halmashauri ilijenga kichomea taka kwa gharama ya **Shilingi 60,014,148**.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Taarifa, changamoto iliyobainika ni mradi huu kutokamilika katika kipindi kilichoainishwa katika Mkataba. Kamati imeisisitiza Halmashauri kuhakikisha majengo yote yanakamilika ili tija iweze kupatikana.

### 2.4 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha fedha za umma zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zinatumika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo, Mwezi Machi, 2024, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Dodoma, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga, Kagera, Geita, Mara na Simiyu.

Ukaguzi uliofanyika katika Mikoa tajwa hapo juu ulijumuisha miradi ya Sekta ya afya, elimu na utawala. Aidha, dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo:-

### 2.4.1 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri hii, Kamati ilifanya ukaguzi katika mradi wa ujenzi wa kituo cha afya katika kijiji cha Manda wenye thamani ya **Shilingi 500,000,000**. Mradi huu ulioanza kutekelezwa tarehe 03 Novemba, 2011 kwa kutumia njia ya force account ulitarajiwa kukamilika tarehe 03 Aprili, 2022. Hata hivyo hadi Kamati ilipofanya ziara mwezi Machi, 2024, mradi huu ulikuwa haujakamilika.

Changamoto zilizobainika katika mradi huu ni pamoja na kutokuwepo kwa maji safi na salama hali inayosababisha jengo la maabara kutotumika na kuhatarisha usalama wa wagonjwa pamoja na watoa huduma, kutokuwepo kwa vifaa tiba hali iliyosababisha huduma ya upasuaji kwa magonjwa mengine kushindwa kuanza, kutotumika kwa vifaa tiba na samani vyenye thamani ya **Shilingi 104,024,200** kwa sababu ya kituo kutokukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Kamati pia ilifanya ukaguzi katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mlowa Barabarani kwa gharama ya **Shilingi 3,250,140,148**. Mradi huu ulitekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2018/19, awamu ya Pili mwaka 2020/21 na awamu ya Tatu 2021/22.

Aidha, hadi Kamati inafanya ziara tarehe 14 Machi, 2023, mradi huu ulikuwa unatumika lakini baadhi ya maeneo yalikuwa hayajakamilika kwa ukamilifu wake. Baadhi ya dosari zilizobainika ni pamoja na kutokufungwa kwa PVC na Gata kwenye majengo ya utawala, OPD, Maabara, Mionzi, Bohari ya Dawa, jengo la kufulia na jengo la wazazi.

### 2.4.2 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Halmashauri lenye gharama ya **Shilingi Bilioni 3.** Utekelezaji wa mradi ulianza tangu tarehe 03 Juni, 2021 na Mkandarasi MCB Company Ltd ambaye mkataba wake umesitishwa kutokana na kukiuka makubaliano (muda wa mkataba kuisha na mradi kutokamilika) ambapo matarajio ya kukamilika kwa kazi yalikuwa ni tarehe 03 Juni, 2022. Hadi mkataba unasitishwa na Halmashauri, Mkandarasi alikwishalipwa kiasi cha **Shilingi 375,161,650.00** kati ya **Shilingi 560,245,000.00** zilizoainishwa katika mkataba. Aidha, kazi iliyofanywa na mkandarasi huyo ilikuwa ni **Asilimia 65**.

Baada ya kuvunjika kwa mkataba wa awali, tarehe 21 Novemba, 2023 Halmashauri iliingia Mkataba mwingine na local Fundi Morris Joseph Makoi kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Halmashauri, kujenga ukuta, kusawazisha eneo la nje na kujenga eneo la maegesho kwa gharama ya **Shilingi 156,200,000.00.** Ujenzi huo ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2024 na kiasi kilichotumika hadi Kamati ilipofanya ukaguzi Mwezi Machi, 2024 ni **Shilingi 2,882,615,002.48** na utekelezaji wa mradi ulifikia **Asilimia 85**.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa na Kamati ni ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya uliotekelezwa kwa kutumia njia ya force account na mafundi mbalimbali kwa gharama ya **Shilingi 1,800,000,000**. Hadi Kamati inafanya ziara mradi ulikuwa umefikia **Asilimia 80** na fedha zote zilikwishatumika.

Changamoto zilizobainika katika mradi huu ni Sakafu maalum (Epoxy) katika chumba cha upasuaji ndani ya jengo la mama na mtoto yenye thamani ya **Shilingi 3,400,000** kutojengwa kwa ustadi hivyo kupelekea kuvimba na kuwa na viashiria vya kubanduka, uwepo wa nyufa katika majengo ya mradi, na ujenzi wa stoo ya dawa

pamoja na jengo la utawala kusimama tangu mwezi Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa na Kamati ni ujenzi wa shule mpya ya sekondari Keikei ambapo Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 470** za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ujenzi umefanyika kwa kutumia njia ya force account ambapo, utekelezaji ulianza tarehe 18 Februari, 2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 18 Aprili, 2022. Hata hivyo, hadi kufanyika kwa ziara hii ujenzi katika baadhi ya majengo umesimama kutokana na fedha kuisha.

### 2.4.3 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Mji Kondoa

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 10 Juni, 2022 Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 400** kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kolo na mradi kutakiwa kukamilika tarehe 10 Oktoba, 2022. Katika mradi huu, kiasi chote cha fedha kimekwishatumika na utekelezaji wa mradi (physical) umefikia **Asilimia 60**. Hadi Kamati ilipofanya ziara, mradi ulikuwa umesimama na Halmashauri iliomba **Shilingi Milioni 100** kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi.

Changamoto zilizobainika katika mradi huu ni pamoja na kusimama kwa mradi, kutoanza kwa ujenzi wa jengo la kufulia (Laundry), kichomea taka (Incinerator) pamoja na njia ya kutembelea (walkway), kusimama kwa ujenzi wa jengo la wazazi na upasuaji (Maternity and Theatre) na kutokamilika kwa kazi ya uwekaji wa vioo vya milango na upigaji polish (Vanish) kwenye majengo ya OPD na Maabara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilikagua ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Tura iliyopokea **Shilingi Milioni 470** kutoka Serikali Kuu. Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 09 Februari 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 17 Aprili 2022. Hata hivyo kulikuwa na nyongeza ya muda hivyo mradi kutakiwa kukamilika tarehe 17 Mei 2022 na hadi kipindi cha ziara

mradi ulikuwa umefikia **Asilimia 85** na kiasi cha **Shilingi Milioni 587** kilishatumika.

Licha ya kiasi chote cha fedha kilichopokelewa kutumika, bado Halmashauri ilikuwa na madeni ya wazabuni na mafundi ujenzi yenye thamani ya **Shilingi 106,179,156** ambayo yalikuwa hayajalipwa na bado kuna kazi ambazo hazikukamilika. Aidha, changamoto zilizobainika ni kutotumika kwa Maktaba na jengo la Tehama kutokana na kukosekana kwa vifaa, ujenzi wa maboma ya maabara zote tatu kutofanyiwa ukamilishaji (Finishing works), maji kutounganishwa kwenye vyoo na kuhatarisha usalama wa afya ya watumiaji, na uwepo wa nyufa za sakafu kwenye jengo la utawala, maktaba na madarasa.

### 2.4.4 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa Halmashauri nyingine, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Kidato cha Tano na Sita Shule ya Sekondari Tumati. Mradi huu wenye thamani ya **Shilingi 750,100,000** ulipokea jumla ya **Shilingi 749,400,000** kutoka Serikali Kuu na **Shilingi 700,000** ni Nguvu za wananchi. Utekelezaji wa mradi huu ulitumia njia ya force account ambapo majengo yaliyojumuishwa katika mradi ni pamoja na madarasa manne yenye Block I na Block II zenye 2 in 1, madarasa manne yenye Block III na Block IV zenye 2 in 1, mabweni manne na choo chenye matundu Kumi na Nne.

Kulingana na mikataba yao, majengo yote yalitakiwa yawe yamekamilika ifikapo tarehe 25 Disemba, 2023. Aidha, kumekuwa na kuongezeka kwa muda wa mradi kwa miradi yote (time Extension) hadi kufikia siku 119 bila makubaliano ya nyongeza ya muda. Hadi Kamati inafanya ziara katika mradi huu, **Shilingi 699,589,516** zilikwishatumika na mradi ulikuwa haujakamilika kwa **Asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi mwingine, Halmashauri pia ilipokea **Shilingi 3,690,000,000** kutoka Serikali Kuu na kutumia **Shilingi 60,000,000** fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi, jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la utawala, jengo la kufulia, jengo la maabara, jengo la stoo ya dawa, jengo la mionzi, jengo la upasuaji la wanaume, jengo la wodi ya upasuaji wanawake, jengo la kuhifadhia maiti, na jengo la nyumba ya watumishi (3 in 1).

Utekelezaji wa mradi huu ulianza tangu Mwaka 2019 na baadhi ya majengo yalitakiwa kukamilika Mwaka 2019 na Majengo mengine yalitakiwa kukamilika Mwaka 2022. Aidha, hadi kufanyika kwa ziara ya Kamati, mradi huu ulikuwa haujakamilika na kiasi cha **Shilingi 2,750,000,000** kilikwishatumika na kwa upande wa jengo la wodi ya wazazi na jengo la utawala ujenzi wake ulikuwa umesimama. Aidha, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ulikamilika kwa **Asilimia 89**.

### 2.4.5 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati

**Mheshimiwa Spika**, Mkandarasi SUMA JKT CONSTRUCTION COMPANY LIMITED alitekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Mradi huu uliopokea jumla ya **Shilingi 3,460,000,000** kutoka Serikali kuu ambapo, ulianza kutekelezwa tarehe 11 Aprili, 2021 na kutarajiwa kukamilika tarehe 10 Oktoba, 2021. Hata hivyo, hadi kufanyika kwa ziara ya Kamati, mradi huu ulitekelezwa kwa **Asilimia 80** na kiasi cha **Shilingi 3,052,883,539.25** (Malipo ya Fundi **Sh. 425,650,000**, Vifaa vya Ujenzi **Sh. 2,627,233,539.25**) sawa na **Asilimia 97** ya fedha zote kilikwishatumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Babati ambapo mradi ulitekelezwa kwa kutumia njia ya force Account. Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi**

**150,000,000** kutoka Serikali Kuu ambapo, mradi ulitakiwa kuanza tarehe 16 Agosti 2022 na kukamilika tarehe 16 Disemba 2022. Hata hivyo, kumekuwa na kuongezeka kwa muda wa mradi (time Extension) hadi kufikia tarehe 12 Juni 2024.

Hadi Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huu, mradi ulikuwa umekamilika kwa **Asilimia 80** na fedha zilizokwishatumika ni **Asilimia 87** na kuna vifaa vya mabomba na umeme ambavyo havijatumika vyenye thamani ya **Shilingi 19,387,900.83**. Aidha, changamoto zilizobainika ni mradi kutokamilika kwa wakati, uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu kutokamilika, kazi za dari kama vile uwekaji wa mikanda ya gypsum kutokamilika pamoja na mifumo ya maji safi na maji taka kutokamilika.

### 2.4.6 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri hii, Kamati ilifanya ukaguzi wa ujenzi wa Kituo Cha Afya Uru Kusini kilichotekelezwa kwa kutumia njia ya force account. Mradi huu ulitekelezwa kwa miezi mitatu na Halmashauri ilipokea **Shilingi 790,000,000** kutoka Serikali kuu, **Shilingi 45,000,000** kutoka katika mapato ya ndani, **Shilingi 7,000,000** nguvu ya wananchi na **Shilingi 21,000,000** ni kutoka kwa wadau wa maendeleo na kufanya jumla ya gharama za mradi wote kuwa **Shilingi 863,000,000**.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2024, mradi ulikuwa umekwishatumia **Shilingi 757,622,529.28** kiasi ambacho ni gharama za vifaa na gharama za fundi. Aidha, kulikuwa na bakaa ya **Shilingi 77,377,470.72** ikijumuisha fedha za matazamio na mradi ulikamilika kwa **Asilimia 99**.
Changamoto zilizobainika ni jengo la upasuaji kutoanza kutumika kwa sababu ya kutonunuliwa na kufungwa kwa kitanda maalum kwa ajili ya upasuaji pamoja na taa maalum kwa ajili ya chumba cha upasuaji, kukosekana kwa umeme, na kutokuwa na mtaalam wa usingizi (Anaesthesia). Changamoto nyingine ni kutotumika kwa jengo la kufulia

kwa sababu ya kutonunuliwa na kufungwa kwa mashine ya kufulia na kukosekana kwa umeme.

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi mwingine, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilipokea jumla ya **Shilingi 3,270,582,654.10** kwa awamu nne kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ambapo, awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa jengo ilitekelezwa na SUMA JKT kwa kutumia njia ya force account na awamu ya tatu ya ujenzi wa uzio imetekelezwa na Mkandarasi 3D Builders Ltd.

Hadi kufanyika kwa ukaguzi wa jengo hili, mradi ulikuwa umefikia **Asilimia 98** na ujenzi wa uzio ulikuwa umefikia **Asilimia 45** ambapo, jumla ya **Shilingi 2,970,582,654** zilikwishatumika na fedha za kukamilisha mradi kiasi cha **Shilingi 607,036,009.17** zilikuwepo kwenye akaunti ambapo **Shilingi 806,040,588.64** ni kwa ajili ya ukamilishaji wa maeneo yaliyobakia na **Shilingi 101,035,420.63** ni bakaa kwa ajili ya maombi ya kibali cha ujenzi wa miundombinu ambayo haikuwepo katika mpango wa awali. Mradi huu ulikuwa umetekelezwa kwa miezi 30 kuanzia tarehe 6 Septemba, 2021 hadi 20 Aprili, 2024 ambapo kwa Mkataba wa awali, mradi huo ulitakiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi 16 na siku 22.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha juu ya uwepo wa thamani ya fedha katika miradi ya sekta ya elimu, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Njia Panda uliotekelezwa kwa kutumia njia ya force account kwa gharama ya **Shilingi 470,000,000** za mradi wa SEQUIP. Hadi kufanyika kwa ziara ya Kamati, kiasi cha fedha kilichotumika ni **Shilingi 463,628,370** ambapo, Bakaa mpaka kukamilika (Ikijumuisha bakizo la kipindi cha matazamio) ni **Shilingi 6,371,630.** Aidha, Asilimia ya kukamilika kwa mradi (Physical) iliyofikiwa ilikuwa ni **90** ambapo, jengo la Maktaba halijakamilika na kazi zilizobaki ni uwekaji vioo vya madirisha, umaliziaji sakafu na upakaji rangi kwa gharama ya **Shilingi 8,425,250**.

### 2.4.7 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shilingi 3,665,638,648** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya uliohusisha ujenzi jengo la utawala, wagonjwa wa nje, jengo la kufulia, stoo ya dawa, maabara, jengo la mionzi, wodi ya wanaume, wodi ya wanawake, wodi ya watoto, wodi ya wazazi, upasuaji, wagonjwa wa dharura, jengo la kuhifadhia maiti, kichomea taka, nyumba ya watumishi (three in one), na njia za kupita kwa wagonjwa.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 11 Januari, 2019 kwa kutumia njia ya force account ambapo, kwa mujibu wa mikataba, mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 17 Julai, 2022. Aidha, hadi Kamati inakagua mradi huu, kiasi chote cha **Shilingi 3,665,638,648** kilikwishatumika na utekelezaji wa mradi ulifikia **Asilimia 95**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali Kuu pia ilitoa jumla ya **Shilingi 3,631,628,933.25** kwa ajili ya ujenzi wa Makao makuu ya Halmashauri mradi ambao ulianza kutekelezwa tarehe 12 Mei, 2015 na Mkandarasi M/S Elerai Construction Co. Ltd (LGA/HQ/ 041/BW/2/ 2014/2015) kwa gharama ya **Shilingi 2,797,798,768** ambapo ujenzi ulisimama kutokana na kukosekana kwa fedha za malipo ya Mkandarasi. Wakati ujenzi unasimama, mkandarasi alikuwa ameshalipwa kiasi cha **Shilingi 879,440,194.25**.

Baada ya kupatikana tena kwa fedha za mradi, Mwaka 2020/2021 Halmashauri iliingia mkataba mwingine na Mkandarasi Elerai Construction Company Ltd (LGA/HQ/044/2020/2021/BW/01) kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa gharama ya **Shilingi 592,069,050**.

Vile vile, Halmashauri iliingia mkataba mwingine na Mkandarasi Levis Mwenewanda kwa Mkatabata LGA. 044/2021/2022/W/7 wa **Shilingi 252,854,300** kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la utawala. Aidha, Halmashauri iliingia

Mkataba na Mkandarasi Betar Investment Ltd LGA/044/HQ/2022/2023/W/06 kwa gharama ya **Shilingi 499,986,717.19** kwa ajili ya kufanya kazi za nje (land scaping).

Aidha, hadi kufanyika kwa ukaguzi, mradi huu ulikuwa umekamilika kwa **Asilimia 95** na kiasi cha **Shilingi 3,590,137,132.17** kilikwishatumika. Haya hivyo, changamoto iliyobainika ni mkataba wenye thamani ya **Shilingi 192,000,000** wa ununuzi wa Samani za jengo la utawala uliofanyika nje ya mfumo wa TANEPS na kutowasilishwa PPRA ili kuchapishwa kama inavyotakiwa na Kanuni ya 20 (1) ya PPR, 2013

### 2.4.8 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri hii, Kamati ilifanya ukaguzi katika miradi mitatu ambapo kati ya hiyo ni mradi wa ujenzi wa Kituo cha kimataifa cha mabasi Moshi (Ngangamfumuni). Mradi huu ulioanza kutekelezwa tarehe 28 Januari, 2019 ulikuwa na gharama ya **Shilingi 28,864,649,322.84** ambapo, muda wa awali wa ukamilishaji wa mradi kwa mujibu wa mkataba ulikuwa ni tarehe 28 Januari, 2021 na baada ya ongezeko la muda ilikuwa ni tarehe 12 Novemba, 2021.

Mawanda ya Wigo wa Awali (Original Contract) yalikuwa ni Ujenzi wa jengo la abiria, hoteli na maeneo ya kupakia na kushusha abiria ambapo wakandarasi waliopatikana walikuwa ni CRJE East Africa Ltd - mkandarasi mkuu **Sh. 19,932,910,739.64**, Atlas Plumbers and Builders - ltd mkandarasi msaidizi maji **Sh. 1,569,767,688**, Dieynem Company Ltd - Mkandarasi msaidizi umeme **Sh. 3,151,179,259.64**, Mkandarasi msaidizi Lift **Sh.909,445,911.60** (Mkataba haukusainiwa), Mkandarasi msaidizi Tehama **Sh. 856,373,823.98** (Mkataba haukusainiwa), Mkandarasi msaidizi viyoyozi **Sh.1,498,069,100** (Mkataba haukusainiwa), na Digital Space Consultancy Ltd, equa Serve Ltd and UNDI consulting group Ltd - Mkandarasi mshauri **Sh. 946,902,800**.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulisimama tangu 14 Mei, 2022 kutokana na kukosekana kwa fedha za kutekeleza mradi kwa wakati na hadi Kamati inafanya ukaguzi wa mradi huu, kiasi cha **Sh. 7,485,564,619.58** kutoka Serikali kuu na **Sh 820,000,000** toka mapato ya ndani kilikuwa kimeshalipwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na kufanya jumla ya fedha iliyotumika kuwa **Sh 8,305,564,619.58** ambayo ni sawa na **Asilimia 29** ya fedha zote za mradi.

Vile vile, Hadi ukaguzi unafanyika, mradi ulikuwa umetekelezwa kwa **Asilimia 30** tu (Physical) na kusimama kwa mradi kwa takribani miezi 21 kuanzia Mei 2022 kumesababisha kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi kwa kiasi cha **Sh. 565,099,008.85** ikijumuisha gharama za kulinda mradi **Sh. 452,319,350.85** na gharama ya riba kiasi cha **Sh 112,779,658.20**. Aidha, gharama ya mradi hadi kukamilika inakisiwa kuwa ni **Sh. 29,429,748,331.69** (Mkataba wa awali Sh 28,864,649,322.84 + gharama ya kulinda na gharama ya riba Sh. 565,099,008.85).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilikagua mradi wa upanuzi wa jengo la utawala wenye thamani ya **Shilingi 2,000,000,000** ambapo, njia ya force account ilitumika. Katika utekelezaji wa mradi huu, wahandisi walikuwa ni Notra Tech Ltd **Sh 143,591,000** ambaye mkataba wake ulisitishwa kwa kushindwa kumaliza kazi kwa wakati na Greenics Ltd **Sh. 75,654,000** anaendelea na ujenzi baada ya mjenzi wa awali kushindwa. Vile vile, TEMESA **Sh 40,000,000** kwa kazi ya kuweka mfumo umeme, Tehama na Mawasiliano.

Mradi huu ulianza kutekelezwa 1 Julai, 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 31 Disemba, 2022. Hata hivyo hadi kufanyika kwa ziara ya ukaguzi katika mradi huu, mradi ulikuwa umefikia **Asilimia 85** na kiasi ambacho kimeshatumika ni jumla ya **Shilingi 1,127,592,585.49** ambayo ni sawa na **Asilimia 56** ya fedha zote za mradi (Notra Tech Ltd - Sh 98,759,457.08, Geenics Ltd - Sh. 51,106,000 na Vifaa vya ujenzi Sh.977,727,128.41).

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliopitiwa na Kamati ni ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kata Msandaka ambapo, Halmashauri ilipokea **Shilingi 470,000,000** za mradi wa SEQUIP na kuongeza mapato ya ndani **Shilingi 150,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo hivyo kufanya jumla ya gharama za mradi kuwa **Shilingi 620,000,000**.

Licha ya mradi huu kukamilika na kuanza kutumika, Kamati ilibaini changamoto kadhaa kama jengo la Tehama na Maktaba kutotumika kwa sababu ya kutosimikwa kwa miundombinu ya Tehama na maktaba na jengo la utawala limekamilika lakini hakuna samani kwa ajili ya watumishi (walimu).

### 2.4.9 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkoa wa Kilimanjaro, Kamati ilimalizia ukaguzi wake katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwa kufanya ukaguzi katika miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pamoja na ujenzi wa Kituo cha Afya Kirya.

Kamati ilianza ukaguzi wake kwa upande wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaojumuisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la maabara, jengo la dawa, jengo la mionzi, jengo la wazazi, jengo wodi wagonjwa mchanganyiko, jengo la kufulia na jengo la kuhifadhia maiti.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitekelezwa kwa kutumia njia ya force account ambapo, Halmashauri ilipokea **Shilingi Bilioni 2** kutoka Serikali Kuu na kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri kiasi cha **Shilingi 77,516,634** na kufanya jumla ya fedha zote zilizotumika kutekeleza mradi kuwa ni **Shilingi 2,077,516,634**. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 28 Juni, 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 20 Februari, 2024.

Hadi Kamati inafanya ziara ya ukaguzi katika mradi huu, utekelezaji wa mradi ulifikia **Asilimia 60** na majengo mawili tu ndiyo yaliyokamilika na makisio ya kukamilisha kazi zilizobaki kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri ni **Shilingi 2,450,686,634.**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 500** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kirya kilichojumuisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Maabara, ujenzi wa wodi ya wazazi na jengo la upasuaji.

Ujenzi ulianza tarehe 18 Februari, 2022 na ulitarajiwa kukamilika 22 Oktoba, 2022. Hata hivyo hadi Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huu, kiasi chote cha fedha kilikwishatumika na mradi ulifikia **Asilimia 80** ambapo, jengo la mama na mtoto na upasuaji lilikuwa halijakamilika.

### 2.4.10 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Korogwe

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa Kamati katika Halmashauri hii ulijikita katika kuangalia ufanisi katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Mradi huu ulijumuisha ujenzi wa jengo la utawala, jengo la dawa, jengo la mionzi, jengo la maabara, jengo la OPD, jengo la kufulia, jengo la wazazi, jengo la wodi ya wanaume, jengo la wodi ya wanawake, jengo la wodi ya watoto, jengo la upasuaji, jengo la wodi za upasuaji za wanawake na wanaume, na jengo la kuhifadhia maiti.

Halmashauri iliingia jumla ya Mikataba 11 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambapo, Mikataba 10 ni ya mafundi ujenzi kwa kutumia njia ya force account na Mkataba mmoja ni Mkandarasi M/S SHELUTETE CONSTRUCTION COMPANY LIMITED. Aidha, Mradi wote ulikuwa na gharama ya **Shilingi 3,100,000,000.00** ambapo, gharama za vifaa ni **Shilingi 1,960,498,000**, gharama za fundi ujenzi ni **Shilingi 344,502,000** na gharama za mkandarasi ni **Shilingi 795,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 01 Aprili, 2019 na kutarajiwa kukamilika tarehe 29 Machi, 2023 ambapo kila fundi alikuwa na muda wake wa utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa mikataba yao. Hata hivyo, hadi Kamati ilipofanya ukaguzi (physical), mradi huu ulikuwa umefikia **Asilimia 86** tu ya utekelezaji na jumla ya kiasi cha **Shilingi 3,043,207,707** sawa na **Asilimia 98** ya thamani ya Mkataba wote (Fundi Sh. 343,438,031 + Vifaa vya ujenzi Sh.1,931,534,836 + Mkandarasi Sh. 768,234,841) kilikuwa kimeshalipwa.

### 2.4.11 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Mji Korogwe

**Mheshimiwa Spika**, katika kuziwezesha Halmashauri kupata fursa za kiuchumi, Halmashauri ilichukua Mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Kilole. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 28 Disemba, 2016 kwa siku 365 ambapo tarehe ya ukamilishaji ilikuwa ni tarehe 27 Disemba, 2017. Aidha, kulikuwa na nyongeza ya siku 90 ambapo tarehe ya ukamilishwaji wa Mkataba iliyorejewa (revised) ilikuwa ni tarehe 05 April 2018.

Mradi ulitekelezwa na Mkandarasi M/S RAVJI CONSTRUCTION LTD kwa gharama ya **Shilingi 1,223,491,373** ambapo, gharama za Mshauri elekezi ilikuwa ni **Shilingi 215,563,735.78** hivyo kufanya mradi wote kuwa na gharama ya **Shilingi 1,439,055,108.78**. Aidha, kipindi cha matazamio kilikuwa ni miezi 12 na kiliisha tarehe 04 Aprili 2019 na mradi umekamilika kwa **Asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na soko kukamilika tayari kwa matumizi kusudiwa, hadi kipindi ambacho Kamati imefanya ziara ya ukaguzi Mwezi Machi, 2024 bado soko hili lilikuwa halijaanza kutumika ikiwa ni muda wa miaka saba tangu kukamilika kwake. Aidha, changamoto ambayo Kamati ilizibaini ni uanzishwaji wa mradi kutozingatia Kanuni za uendeshaji wa miradi (Principles of Projects Management) kwa kutofanya upembuzi yakinifu wa kijamii (social feasibility

study) na baadhi ya sehemu ya dari (ceiling board) kuanza kunyofoka.

### 2.4.12 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi katika miradi miwili inayotekelezwa na Halmashauri hii ambayo ni mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na mradi wa ujenzi wa Majengo Kumi na Tisa katika Shule mpya ya Sekondari ya Chartur.

Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri ilipokea **Shilingi 500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wanaume, wanawake na watoto katika awamu ya kwanza. Katika kipindi ambacho Kamati ilifanya ukaguzi, Jengo la wodi ya wanaume na wanawake lilikuwa limekamilika kwa **Asilimia 90** na jengo la wodi ya watoto lilikuwa limekamilika kwa **Asilimia 45**.

**Mheshimiwa Spika**, Katika awamu nyingine, jumla ya **Shilingi Milioni 800** zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi za upasuaji wanaume na wanawake na jengo la kuhifadhia maiti kwa gharama za fundi **Shilingi 109,907,341**. Hadi kufanyika kwa ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, fedha yote **Shilingi Milioni 800** ilikwishatumika (Fundi Shilingi 100,775,491, Vifaa vya ujenzi Shilingi 633,632,427 na matumizi mengineyo Shilingi 65,592,078) na utekelezaji wa miradi yote ilifikia **Asilimia 85**.

Aidha, changamoto zilizobainika ni kutumia fedha za mradi **Shilingi 72,549,841** kukamilisha jengo la watoto lililoanzishwa na wananchi bila ya kupata kibali cha OR –Tamisemi pamoja na kutumia **Shilingi 427,450,160** (133%) katika ujenzi wa wodi ya wanaume na wanawake zaidi ya makisio ya **Shilingi 320,830,450** yaliyoandaliwa na Mhandisi katika majengo hayo na kufanya kuwepo kwa ongezeko la mradi kwa **Shilingi 106,619,710** licha ya majengo hayo kutokamilika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa elimu, Kamati pia ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa Majengo Kumi na Tisa katika shule mpya ya Sekondari ya Chartur ambapo, Serikali ilitoa jumla ya **Shilingi Bilioni 1** kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo ambapo, ujenzi ulianza tarehe 7 Septemba, 2021 na kutarajiwa kukamilika tarehe 7 Disemba, 2021.

Hadi kufikia kipindi ambacho Kamati inafanya ziara, Halmashauri ilikwishatumia jumla ya **Shilingi 998,977,560** (Malipo ya Fundi Shilingi 108,778,781, Ununuzi wa vifaa vya ujenzi Shilingi 844,554,222 na gharama nyinginezo Shilingi 45,644,557) na utekelezaji wa mradi ulifikia **Asilimia 56**. Aidha, Halmashauri iliomba Serikalini **Shilingi Milioni 700** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi huu. Changamoto kubwa ya mradi huu ni makisio ya ujenzi wa shule yaliyoandaliwa na Halmashauri **Shilingi 2,321,312,570** kuwa tofauti na maelekezo ya OR –Tamisemi ambayo ilitoa **Shilingi 1,000,000,000** na kuanza utekelezaji wa mradi bila ya kuwa na kibali cha mabadiliko ya gharama kutoka OR – Tamisemi.

### 2.4.13 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Jiji la Tanga

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipanga kutekeleza mradi wa mradi wa ujenzi wa Jengo la Soko la machinga (Machinga complex) kwa gharama ya **Shilingi 1,328,603,000** ambapo fedha hizo zilitoka katika vyanzo mbalimbali kama Serikali Kuu (UVIKO) **Shilingi 540,340,273**, Mapato ya ndani **Shilingi 243,216,247** na fedha za mradi wa Green and Smart Cities **Shilingi 517,238,874** ambazo ziliingia Halmashauri mwezi Oktoba, 2023.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 03 Agosti, 2022 kwa kutumia njia ya force account kwa gharama ya fundi ya **Shilingi 281,400,000** na ulitarajiwa kukamilika tarehe 21 Disemba, 2022. Tarehe ya ukamilishwaji wa Mkataba ilirejewa kwa mara kadhaa, na tarehe iliyorejewa kwa mara ya mwisho ilikuwa ni tarehe 12 Disemba, 2023.

Pamoja na rejea hizo zilizofanyika, hadi Kamati ilipofanya ziara ya ukaguzi, mradi huu ulikuwa haujakamilika na kiasi kilicholipwa kilikuwa ni **Shilingi 783,556,520** na mradi ulikuwa upo katika hatua za msingi. Aidha, kulikuwa na vifaa vya ujenzi vilivyoachwa bila matumizi na bila utunzaji unaoridhisha vyenye thamani ya **Shilingi 424,362,740**, vikiwa vinaharibika kutokana na hali ya hewa kama mvua na unyevu na kusababisha kupata kutu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi wa kimkakati wa ujenzi wa jengo la Kitega Uchumi kituo cha mabasi Kange ambalo linatekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Tanga. Mradi huu wa kimkakati wenye thamani ya **Shilingi 8,498,298,758.51** uliokuwa ukitekelezwa kwa fedha kutoka Serikali kuu ambapo mawanda ya awali yalihusisha ujenzi wa jengo la Kitega Uchumi kituo cha mabasi Kange pekee kwa gharama ya **Shilingi 8,163,025,889.51**.

Baada ya kuongeza wigo wa utekelezaji, mradi ulihusisha ujenzi wa jengo hilo pamoja na kununua na kusimika generator. Nyongeza ya wigo huo umefanya kuongezeka kwa gharama za mradi kwa **Shilingi 335,272,869**. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 25 Julai, 2019 na Mkandarasi M/S Mohammedi Builders Ltd kwa Mkataba LGA/128/2018 - 19/HQ/W/SP 43 na kutarajiwa kukamilika tarehe 25 Julai, 2020. Hadi kufanyika kwa ukaguzi, jumla ya **Shilingi 7,412,179,688.63** zilikuwa zimekwishatumika na mradi ulikuwa umefikia **Asilimia 98** na Jengo lipo katika hatua ya umaliziaji.

### 2.4.14 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipeleka **Shilingi Milioni 250** kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ya Wilaya ya Pangani ambapo, mawanda ya mwisho ya kazi baada ya nyongeza yalijumuisha ujenzi wa ICU pamoja na ujenzi wa jengo la mitungi ya gesi.

Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 18 Machi, 2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 20 Juni, 2022. Hata hivyo kutokana na nyongeza ya muda, mradi ulikamilika tarehe 30 Juni, 2023. Gharama ya mradi ilikuwa ni **Shilingi 297,257,500** ambapo malipo ya fundi ni **Shilingi 34,938,000**.

Changamoto zilizobainika ni mradi kukamilika na vifaa kuletwa na Serikali kuu lakini ICU ilikuwa haitumiki kwa sababu hapakuwa na jenereta yenye uwezo wa kuendesha vifaa vya ICU pindi umeme wa Tanesco utakapokatika na Halmashauri haikutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa Jenerata.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Madanga uliojumuisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la maabara, kichomea taka, jengo la wazazi na upasuaji (combined), jengo la kufulia na ujenzi wa njia za kuunganisha majengo (Walk ways) kwa gharama ya **Shilingi 522,562,000** (Tozo - Serikali Kuu Shilingi 500,000,000 na Mapato ya ndani Shilingi 22,562,000). Aidha, gharama ya fundi ilikuwa ni **Shilingi 88,197,640**.

Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 15 Novemba 2021 na tarehe tarajiwa ya kukamilisha mkataba ilikuwa ni tarehe 15 Februari, 2022 na baada ya marejeo tarehe mpya ya ukamilishaji wa mkataba ilikuwa ni tarehe 01 Mei, 2022. Hadi Kamati ilipofika katika eneo la mradi, jengo la wodi ya wazazi na upasuaji (Maternity and theatre combined) lilikuwa halijakamilika na fedha za mradi zilikwishatumika zote hivyo ujenzi ulisimama.

### 2.4.15 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyo kwa Halmashauri nyingine, Serikali ilipeleka jumla ya **Shilingi 2,550,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga. Fedha za utekelezaji wa mradi huu zilipokelewa

kwa awamu Nne ambapo, awamu tatu za kwanza ilikuwa ni **Shilingi 1,800,000,000** na awamu ya Nne zilipokelewa **Shilingi 750,000,000**.

Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 23 Machi, 2024 na Fundi M/S 838 KIKOSI CHA JESHI (MARAMBA) JKT wa S.L.P 6005 TANGA kwa gharama ya **Shilingi 351,585,024.93** na Mkandarasi M/S NICHOLAUS KILOBA wa S.L.P 31986 DAR ES SALAAM kwa gharama ya **Shilingi 47,000,000**.

Hadi kufikia wakati wa ukaguzi, jumla ya **Shilingi 2,517,624,410.65** zilikwishatumika na kubakiwa na **Shilingi 32,375,589.35**. Licha ya kiasi hicho cha fedha kutumika, bado kulikuwa na majengo ambayo hayakukamilika kwa **Asilimia 100** na majengo ya wodi ya wanaume magonjwa mchanganyiko (medical), wodi ya watoto na jengo la kuhifadhia maiti ujenzi wake ulikuwa haujaanza kabisa na fedha zake zilikwishapokelewa na kutumika katika maeneo mengine kinyume na Mwongozo wa OR – Tamisemi.

### 2.4.16 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 470** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Rukoma ambapo, utekelezaji wake ulianza tarehe 08 Februari 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 08 Aprili 2022. Hata hivyo, hadi kipindi cha ukaguzi tarehe 16 Machi, 2024 mradi ulifikia **Asilimia 90** na kiasi cha **Shilingi Milioni 570** kilikwishatumika. Licha ya fedha zote kutumika, maabara ya fizikia (Physics), maktaba na jengo la TEHAMA zilikuwa hazijakamilika na hapakuwa na umeme katika shule hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa na Kamati ni ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bukoba ambao ulianza kutekelezwa tarehe 26 Januari, 2019 kwa kutumia njia ya force account na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Aprili, 2021. Hata hivyo mradi ulikamilika tarehe 30 Juni, 2022 kwa

gharama ya **Shilingi 3,201,508,027.48** ambapo **Shilingi 3,100,000,000** ni fedha kutoka Serikali Kuu na **Shilingi 101,508,027.48** ni fedha za mapato ya ndani.

Changamoto kubwa iliyobainika katika mradi huu ni baadhi ya majengo (majengo sita kati ya kumi na tano yaliyojengwa) ambayo yalikamilika kutoanza kutumika kutokana na ukosefu wa vifaa pamoja na Mashine ya kufulia iliyonunuliwa kutofungwa na badala yake kuhifadhiwa katika jengo la kuhifadhia dawa.

### 2.4.17 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kitobo yenye gharama ya **Shilingi Milioni 470** chini ya mradi wa SEQUIP ambao, ulianza kutekelezwa tarehe 24 Februari, 2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 17 Oktoba, 2023. Hata hivyo, hadi kufanyika kwa ziara ya Kamati ujenzi katika baadhi ya majengo ulikuwa haujakamilika licha ya Halmashauri kuongeza **Shilingi Milioni 100** ya mapato ya ndani katika mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi pia ulifanyika katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Missenyi ambapo, mradi ulianza kutekelezwa tarehe 01 Septemba, 2021 kwa kutumia njia ya force account na kutarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2024. Thamani ya jumla ya Mradi ni **Shilingi 3,000,000,000** ambapo, hadi siku Kamati inakagua mradi huu, **Shilingi 2,600,000,000** kutoka Serikali Kuu zilipokelewa na **Shilingi 1,800,000,000** zilikuwa zimeshatumika. Aidha Mradi huu ulipokea pia fedha kutoka mapato ya ndani ya **Shilingi 144,000,000** na kutoka Programu ya utekelezaji wa maji na usafi wa mazingira wa vijijini (WASH) **Shilingi 72,997,000** ambazo pia zilikwishatumika.

**2.4.18 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Halmashauri hii, Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa Hospitali ya Manispaa ya Bukoba ulioanza kutekelezwa tarehe 04 Agosti, 2021 kwa kutumia njia ya force account na kutarajiwa kukamilika tarehe 10 Juni, 2023 kwa gharama ya **Shilingi 2,300,000,000** kutoka Serikali Kuu. Hata hivyo, hadi siku Kamati inatembelea mradi huu, mradi ulikuwa bado haujakamilika kwa **Asilimia 100** na majengo yaliyokamilika baadhi yalikuwa hayatumiki.

**2.4.19 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Mji Geita**

**Mheshimiwa Spika**, ulifanyika ukaguzi wa mradi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Geita unaotekelezwa na Halmashauri ya Mji Geita pamoja na Kampuni ya Uchimbaji Dhahabu Geita (GGML) kupitia fedha za Uwajibikaji wa Mmiliki wa Leseni za Uchimbaji Madini kwa Jamii (CSR) za mwaka 2021, 2022 na 2023. Utekelezaji wake unafanyika kwa makubaliano ya kutenga fedha kutokana na fungu la CSR kila mwaka hadi mradi huu utakapokamilika.

Mradi ulikadiriwa kuwa na thamani ya **Shilingi 3,720,000,000** na utekelezaji wake ulianza rasmi tarehe 05 Mei, 2020 kwa njia ya force account. Utekelezaji umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokamilika kwa wakati na kubadili wakandarasi mara kwa mara. Kutokana na mabadiliko hayo, tarehe 16 Julai, 2021 utekelezaji wa mradi ulianza tena chini ya mkandarasi mwingine ambapo thamani yake ya jumla kwa mujibu wa mkataba ilikuwa ni **Shilingi 2,658,169,050,81** na ulitarajiwa kukamilika tarehe 03 Agosti, 2023.

Hadi kufikia wakati wa ziara ya Kamati, **Shilingi 2,283,107,047.56** zilikwishatumika na kiasi kilichobakia kilikuwa ni **Shilingi 1,436,892,952.44** na mradi ulikuwa bado haujakamilika. Aidha, changamoto ya mradi huu ni kutokuwepo kwa makubaliano (MOU) kati ya Halmashauri

na GGML kuonesha majukumu ya kila pande katika utekelezaji wa mradi huu na kutokuwa na muda maalumu (time frame) na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa mradi hivyo, kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi ambapo, **Shillingi Millioni 480** ziliongezeka bila ya kuwa na uthibitisho wa matumizi yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Bulela ambapo, **Shilingi 460,000,000** zilitengwa kutoka mapato ya ndani katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2023/2024 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Utekelezaji wake ulianza tarehe 01 Novemba, 2021 na kutakiwa kukamilika tarehe 02 Januari, 2022. Hata hivyo hadi kipindi Kamati ilipotembelea kwa ajili ya ukaguzi tarehe 19 Machi, 2024 mradi huu ulikuwa bado haujakamilika licha ya kiasi chote cha fedha kutumika.

**2.4.20 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea **Shilingi 2,900,000,000** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala la Ofisi ya Halmashauri. Utekelezaji wake ulianza tarehe 10 Mei, 2021 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 10 Mei, 2022. Changamoto zilizobainika katika mradi huu ni Halmashauri kuingia Mkataba wa ujenzi pasipokuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha katika kipindi cha Mkataba na kutokamilika kwa ujenzi wa fensi kuzunguka eneo la jengo la Utawala na kibanda cha mlinzi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa na Kamati ni ujenzi wa shule Mpya ya Sekondari ya Nyasaricho kwa gharama ya **Shilingi 1,000,000,000** fedha za Mradi wa EP4R na **Shilingi 630,000,000** kutoka kwenye fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri na mradi ulitarajiwa kukamilika tarehe 15 Machi, 2022. Changamoto kubwa iliyobainika ni kutokukamilika kwa majengo ya bwalo la chakula, jiko la nje na kichomea taka.

### 2.4.21 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Tarime

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la Ofisi ya Halmashauri wenye thamani ya **Shilingi 3,115,458,992.30** ambapo, utekelezaji wake ulianza tarehe 26 Aprili, 2018 na kutarajiwa kukamilika tarehe 01 Januari, 2022. Aidha, dosari zilizobainika katika mradi huu ni kutokamilika kwa ujenzi wa fensi kuzunguka eneo la jengo la utawala, *landscaping* na kibanda cha mlinzi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa ni ujenzi wa Soko la Kisasa Kata ya Bomani kwa thamani ya **Shilingi 9,534,067,234.99.** Mradi huu ulianza tarehe 19 Januari, 2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 17 Mei, 2024. Hadi tarehe 22 Machi, 2024 ambapo Kamati ilikagua mradi huu, kiasi cha **Shilingi 5,772,132,847.75** kilishatumika na mradi ulikuwa umekamilika kwa **Asilimia 82**. Changamoto iliyobainika ni ucheleweshwaji wa malipo kwa Mkandarasi jambo lililochelewesha ukamilishaji wa ujenzi wa soko.

### 2.4.22 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2020/2021, 2021/2022, Halmashauri ilitekeleza mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya wenye thamani ya kiasi cha **Shilingi 1,902,975,983** na Mradi huu ulikamilika tarehe 30 Juni, 2022. Dosari zilizoibuliwa na Kamati wakati wa ukaguzi wa mradi huu ni kutokamilika kwa kazi za umaliziaji (Finishing) kama vile skimming katika baadhi ya majengo hazikufanyika kwa ufanisi, pamoja na kutofuata Kanuni, taratibu na miongozo ya manunuzi wakati wa utekelezaji wa miradi.

### 2.4.23 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma

**Mheshimiwa Spika**, Katika Halmashauri hii Kamati ilitembelea Miradi miwili (2) ambayo ni Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Rwamlimi na Shule Mpya ya Sekondari katika kata ya Kigera.

Katika ujenzi wa zahanati ya Rwamlimi, mradi ulipaswa kutumia **Shilingi 550,000,000** zilizopokelewa kutoka Serikali Kuu. Hata hivyo, Halmashauri ilitumia jumla ya **Shilingi 632,068,000** na bado kulikuwa na kazi ambazo zilikuwa hazijakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shillingi Milioni 470** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari iliyojengwa katika Kata ya Kigera. Hadi Kamati inafanya ziara katika mradi huu, jumla ya **Shilingi 652,718,648** ilikwishatumika na mradi ulitekelezeka kwa **Asilimia 80.99** tu, vile vile, Halmashauri iliijulisha Kamati kuwa bado inahitaji kiasi cha **Shilingi 153,233,543** ili kukamilisha ujenzi wa shule hiyo.

### 2.4.24 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Butiama

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama uliopaswa kukamilika kwa **Shilingi 1,300,000,000** zilizopokelewa kutoka Serikali Kuu. Wakati wa utekelezaji wa mradi huu, Halmashauri iliongeza **Shilingi 32,000,000** kutoka katika mapato ya ndani na kufanya jumla ya fedha zote zilizotumika kuwa ni **Shilingi 1,332,000,000**. Licha ya fedha zote kutumika, utekelezaji wa mradi huu uliofikia **Asilimia 89** ulisimama ambapo, Mkandarasi Chabhoke Construction Company Ltd alipaswa kukamilisha mradi huu tarehe 6 Juni, 2022 na kiasi kilichohitajika ili kukamilisha mradi ni **Shilingi 153,793,125**.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ilipokea fedha za SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Kamugegi kwa gharama ya **Shilingi Milioni 470** mradi ambao ulipaswa kukamilika tarehe 6 Julai, 2022. Hadi tarehe 25 Machi, 2024 wakati wa ziara ya Kamati, jumla ya **Shilingi 525,000,000** zilikwishatumika na mradi ulifikia **Asilimia 72** tu na fedha zilizotakiwa ili kuweza kukamilisha mradi huu ni **Shillingi 173,059,072**.

### 2.4.25 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo katika Halmashauri nyingine, Kamati ilifanya ziara katika miradi miwili inayotekelezwa na Halmashauri hii. Mradi wa kwanza uliokaguliwa ni mradi wa Kiwanda cha chaki, gypsum na vifungashio ambao ni mradi wa kimkakati katika Mkoa wa Simiyu.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ni moja kati ya Hamashauri 17 Nchini zilizotengewa Bajeti ya kutekeleza miradi ya kimkakati kwa mwaka wa fedha 2018/19. Hivyo, hadi kufikia mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ni **Shillingi 10,165,086,421.00** kutoka Serikali kuu na Halmashauri ilitoa kiasi cha **Shillingi 62,113,000.00** cha mapato ya ndani kutekeleza mradi huu. Mradi huu ulikuwa katika hatua ya umaliziaji na ulitarajiwa kuanza uzalishaji mnamo tarehe 15 Mei, 2024 baada ya Mkandarasi kumaliza majaribio yake ya siku 15 (Testing and Commissioning).

Changamoto iliyobainika katika mradi huu ni kukosekana kwa umakini wakati wa uandaaji wa andiko la mradi (project plan) ambapo ilipelekea kusahau vitu muhimu kama vile uzio na jengo la utawala, hivyo kupelekea kushindwa kununua mashine za vifungashio kwani kiasi cha **Shillingi 1,236,655,253.81** kilichopaswa kununua mashine hizo, kilitumika kujenga uzio na jengo la utawala.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa pili uliokaguliwa na Kamati ulikuwa ni ujenzi wa jengo la kutolea huduma za dharura (EMD) ambapo, Halmashauri ilipokea jumla ya **Shillingi 311,828,579** ambazo fedha kutoka Serikali kuu (COVID – 19) na mapato ya ndani. Ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 17 Februari, 2022 na kukamilika Julai, 2022 na mradi ulianza kutumika tarehe 10 Machi, 2023 baada ya kupokea vifaa tiba.

### 2.4.26 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa Kamati katika Halmashaur hii ulijikita katika miradi miwili. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa vibanda vya Biashara Soko Kuu, tarehe 1 Novemba, 2022 Halmashauri ilianza ujenzi wa vyumba 106 vya wafanyabiashara katika soko kuu. Mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Mei, 2024 kwa kutumia fedha za makusanyo ya mapato ya ndani.

Wakati kamati inafanya ukaguzi, mradi ulikuwa umeshatumia jumla ya **Shilingi 1,121,016,306.16** na ujenzi bado ulikuwa unaendelea ambapo ulifikia **Asilimia 85**. Aidha, hadi kukamilika kwake, mradi huu ulitarajiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,880,567,850**.

Aidha, Dosari zilizobainika katika mradi huu ni kubadilika kwa ramani kulikopelekea kuchelewa kumalizika kwa mradi, na kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kulikotokana na kupanda kwa gharama za vifaa pamoja na kutokuwepo kwa andiko la mradi (project plan) ambalo lingeonesha muda wa kurejeshwa kwa gharama za ujenzi, taratibu za uendeshaji wa vibanda hivyo na muda ambao faida ingeanza kupatikana.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine uliokaguliwa na Kamati ni ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana Shinyanga ambapo, Halmashauri ilipokea fedha za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo katika awamu ya kwanza, Serikali ilitoa jumla ya **Shilingi 3,000,000,000**, na awamu ya pili Halmashauri ilipokea **Shilingi 1,100,000,000** na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa kuwa ni **Shilingi 4,100,000,000**.

Wakati wa utekelezaji wa mradi huu, Halmashauri iliongezewa **Shilingi 285,000,586**. Hata hivyo, mpaka muda Kamati inafanya ukaguzi, mradi ulifikia **Asilimia 86** na kiasi cha **Shilingi 3,908,379,581** kilikwishatumika na kubakiwa na

**Shilingi 476,621,005**. Aidha, Halmashauri iliijulisha Kamati kuwa bado inahitaji kiasi cha **Shilingi 722,000,000** kwa ajili ya kumalizia miundombinu mbalimbali kama vile, ununuzi wa jenereta, gari, taa za solar na uwekaji wa mifereji ya kuvunia maji.

### 2.4.27 Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri hii, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa jengo la wodi ya mama na mtoto ulioanza kutekelezwa tarehe 15 Juni, 2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 15 Juni, 2025. Mradi ulitekelezwa kwa fedha kutoka Serikali kuu na mapato ya ndani kwa gharama za **Shillingi 6,791,250,594.23** ambapo, Mkandarasi alikuwa ni SUMA JKT. Hadi Kamati inatembelea eneo la mradi jumla ya **Shilingi 1,560,825,399.88** zilishatumika ambapo **Shilingi Bilioni 1** ni kutoka Serikali kuu na **Shillingi 560,825,399.88** zilitokana na mapato ya ndani na mradi ulifikia **Asilimia 30** ya utekelezaji.

Changamoto iliyobainika katika mradi huu ni kuanza ujenzi kabla ya mchoro kupata kibali cha OR – TAMISEMI ambapo kulikuwa na makosa kwenye mchoro huo, hali iliyopelekea mradi kusimama mpaka mabadiliko ya mchoro yatakapofanyika pamoja Mjenzi na Mhandisi mshauri kuwa ni mtu mmoja ambaye ni SUMA JKT.

**Mheshimiwa Spika**, katika mradi mwingine, Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shillingi Millioni 500** fedha za Tozo kwa awamu mbili kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya cha Kinaga na kila awamu ilipokea **Shilingi Milioni 250**. Katika awamu ya pili, ujenzi wa majengo ulikamilika isipokuwa ujenzi wa njia za wagonjwa (Walk ways) wenye gharama ya **Shilingi 57,680,000**.

Vile vile, Halmashauri iliongeza kiasi cha **Shilingi 77,560,412.51** kutoka katika mapato ya ndani na kufanya jumla ya fedha zilizotumika kuwa ni **Shilingi 577,560,412.51**.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa kina wa Taarifa za utekelezaji wa miradi ya BOOST, miradi ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya na miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ufuatiliaji wa fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ndiyo jicho la Bunge katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Ili kutekeleza kikamilifu jukumu hilo, Maoni ya Kamati ni kuhakikisha, miradi yote inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa inazingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu.

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kuwashirikisha katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla. Ili dhamira hiyo iweze kufikiwa, Maafisa Masuuli waliopewa dhamana ya kusimamia matumizi ya fedha za Umma wanatakiwa kuhakikisha kunakuwa na ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili thamani ya fedha iweze kupatikana.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Kamati yanatokana na changamoto na dosari zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mapendekezo hayo yanalenga kuondoa changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya

mradi wa BOOST, ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri na ujenzi wa Hospitali za Wilaya. Mapendekezo ya Kamati ni kama yafuatayo: -

### 3.3.1 Changamoto ya Mtiririko wa fedha za miradi

**KWA KUWA,** kumekuwepo kwa changamoto ya mtiririko wa fedha za miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu na ambayo malipo ya hati madai (certificates) yanafanywa moja kwa moja na Hazina pamoja na fedha kuchukuliwa na Hazina kabla ya ukamilishaji wa mradi;

**NA KWA KUWA,** fedha za miradi kutopatikana kwa wakati kumesababisha baadhi ya miradi kutekelezwa kwa kusuasua na kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na mapokezi ya fedha za miradi hiyo kuwa ni ya kuchelewa tofauti na mikataba ambayo Halmashauri zimeingia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika;

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihakikishe fedha za miradi zinatolewa kulingana na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge na kwa muda uliopangwa katika Mikataba**;**
b) Serikali (Wizara ya Fedha) ihakikishe fedha za miradi zilizovutwa zinarejeshwa katika Halmashauri husika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu ili ziweze kukamilisha miradi husika;
c) kwa miradi itakayotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026, OR – TAMISEMI ihakikishe utoaji wa fedha za miradi unazingatia jiografia ya Halmashauri husika, upatikanaji wa vifaa pamoja na gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

### 3.3.2 Kutofanyika kwa tathmini na ufuatiliaji wa mara kwa mara

**KWA KUWA**, kumebainika kukosekana kwa usimamizi wa karibu wa miradi inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imesababisha baadhi ya miradi kukosa ubora uliostahili kutokana na kutekeleza miradi kinyume na maelekezo yaliyotolewa na OR – TAMISEMI na kutokamilika kwa miundombinu muhimu kwa baadhi ya majengo licha ya majengo hayo kuanza kutumika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi za RAS zifanye tathmini na ufuatiliaji kwa miradi yote inayotekelezwa katika Halmashauri zao na kuwasilisha OR – TAMISEMI taarifa ya kila robo mwaka itakayoainisha changamoto na dosari zilizopo katika miradi hiyo ili Serikali iweze kuchukua hatua za haraka.

### 3.3.3 Miongozo inayotolewa kutozingatia tofauti ya jiografia ya Halmashauri zote nchini

**KWA KUWA**, Serikali imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kuhusiana na matumizi sahihi ya fedha za utekelezaji wa miradi zinazopelekwa katika Halmashauri zote nchini bila ya kuzingatia jiografia ya kila Halmashauri;

**NA KWA KUWA**, maelekezo hayo yamesababisha Halmashauri zenye mazingira tofauti (zilizopo pembezoni, milimani na visiwani) kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati na kwa ufanisi unaotakiwa;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba, OR – TAMISEMI ihakikishe Miongozo inayotolewa inatoa fursa kwa Halmashauri ambazo zina mazingira ya kipekee kuweza kutekeleza miradi hiyo kulingana na hali halisi ya mazingira yaliyopo.

### 3.3.4 Kuchelewa kukamilika kwa miradi

**KWA KUWA**, Kamati imebaini ucheleweshaji katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kusababisha miradi kutokamilika kwa wakati;

**NA KWA KUWA**, miradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa kunachelewesha kupatikana kwa faida ya miradi hiyo kinyume na dhamira ya Serikali;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihakikishe inakamilisha miradi yote viporo kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya ili lengo la uanzishwa wa miradi hiyo liweze kufikiwa, na
b) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi wa kina katika miradi yote yenye changamoto ambayo imejengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kubainisha iwapo kuna thamani ya fedha (value for money).

### 3.3.5 Kukosekana kwa muunganiko baina ya Taasisi za Serikali katika utekelezaji wa miradi

**KWA KUWA**, kumekuwa na changamoto ya Taasisi za Umma kutoshirikiana katika kufanikisha utekelezaji wa miradi nchini;

**NA KWA KUWA**, Changamoto hii imekuwa ikiongeza gharama za miradi kutokana na Halmashauri kufanya shughuli ambazo kimsingi zilipaswa kutekelezwa na Taasisi nyingine;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kwa miradi itakayotekelezwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi zote za Umma zinazotoa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashirikiana katika kuandaa miundombinu muhimu kama Barabara, umeme na maji kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi.

### 3.3.6 Uchaguzi usio sahihi wa eneo la mradi

**KWA KUWA**, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitekeleza miradi bila ya kufanya tathmini ya kimazingira ili kubaini iwapo eneo husika litafaa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi;

**NA KWA KUWA**, kutofanyika kwa tathmini ya mazingira kumesababisha baadhi ya miradi kutekelezwa katika maeneo ambayo si rafiki yenye mabonde au miinuko hivyo kuongeza gharama za miradi hiyo;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba, OR – TAMISEMI (kwa kushirikiana na Ofisi za RAS) ihakikishe inafanya uchambuzi wa kina wa maeneo ambayo miradi inatarajiwa kutekelezwa kabla ya kutoa fedha za utekelezaji wa miradi. Vile vile, kila Halmashauri ifanye tathmini ya mazingira kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi.

### 3.3.7 Upungufu wa Rasilimali watu

**KWA KUWA**, Ripoti ya CAG imebainisha uwepo wa upungufu wa watumishi wanaotakiwa kutoa huduma kwa wananchi hasa kwa upande wa kada ya afya;

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa watumishi hao kunasababisha dhamira ya Serikali ya kutoa huduma bora kwa wakati na kwa wananchi wote kutofikiwa kutokana na idadi ya watoa huduma za afya kuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya Hospitali, vituo vya afya na zahanati;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kunakuwa na Rasilimali watu wa kutosha kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi kulingana na mahitaji ya maeneo husika na miundombinu iliyopo.

### 3.3.8 Kutozingatia Taratibu za Ulipwaji wa Malipo ya Wakandarasi

**KWA KUWA**, Taarifa ya CAG imebainisha changamoto za malipo yanayofanyika kwa Wakandarasi ambazo ni kutozingatiwa kwa taratibu za malipo ikiwa ni pamoja na wakandarasi kulipwa kabla ya utekelezaji wa mradi;

**NA KWA KUWA**, kukiukwa kwa taratibu za malipo kumesababisha miradi kutotekelezwa kwa wakati;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali (Wizara ya Fedha) ihakikishe inachukua hatua za haraka juu ya taratibu za malipo zilizofanywa kwa Wakandarasi waliotekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Halmashauri ya Wilaya na Kibiti, na Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara; na

b) Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina katika miradi ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Halmashauri ya Wilaya na Kibiti, na Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya kamati naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa uongozi wako katika kipindi chote cha Bunge la 12 hadi kufikia sasa. Uongozi wako thabiti na miongozo mbalimbali uliyoitoa imeiwezesha Kamati ya LAAC kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Aidha, natambua na kuthamini mchango wao adhimu katika utekelezaji wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** weledi na ushirikiano wao, imeisaidia Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi na tija katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Halima James Mdee, Mb. - Mwenyekiti
2) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb. - Mjumbe
3) Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb. - Mjumbe
4) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb. - Mjumbe
5) Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb. - Mjumbe
6) Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb. - Mjumbe
7) Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb. - Mjumbe
8) Mhe. Lemburis Saputu Mollel, Mb. - Mjumbe
9) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb. - Mjumbe
10) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb. - Mjumbe
11) Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mb. - Mjumbe
12) Mhe. Abdul Yusuf Maalim, Mb. - Mjumbe
13) Mhe. Mussa Omar Salim, Mb. - Mjumbe
14) Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb. - Mjumbe
15) Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb. - Mjumbe
16) Mhe. Simai Hassan Sadiki, Mb. - Mjumbe
17) Mhe. Jacob Tarimo Priscus, Mb. - Mjumbe
18) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naomba pia kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwani Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT). Vile vile, napenda kuishukuru OR – TAMISEMI kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati kwa kutoa ufafanuzi kila ilipohitajika kufanya hivyo. Mwisho japo sio kwa umuhimu napenda kuishukuru Wizara ya Fedha kwa uwepo wao na ushirikiano wao katika vikao vya Kamati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ya

Mitaa na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati yaliyotolewa kwenye Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Halima James Mdee, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
13 Februari, 2025

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa tunaanza uchangiaji, Mheshimiwa Tarimo, wajiandae Mheshimiwa Mchungahela, Mheshimiwa Simai Sadiki na Mheshimiwa Jesca. *(Makofi)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kuanza kuchangia hii Taarifa yetu ya Kamati. Niungane kabisa na mapendekezo yote ya Kamati kama tulivyokuwa tumeyawasilisha kwenye taarifa. Pia ninaomba kutoa mapendekezo ya ziada ambayo kama Bunge sasa mkiyaona yanafaa basi mtayachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tatizo la kuchagua eneo ambalo siyo rafiki kwa mradi, tumegundua mambo mawili; moja, kuna maeneo wameenda kujenga kwa mfano shule, eneo ambalo ni la bonde, msingi unachukua fedha kubwa. Unakuta fedha imeisha mradi haujakamilika. Huo ni upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo miradi imetekelezwa hakuna watu. Unakuta wanasiasa au pengine katika kupanga wamepeleka maeneo ambayo wanufaika wa mradi huo hawapo. Unakuta ni kituo cha afya, lakini wagonjwa hakuna. Unakuta ni shule, lakini madarasa ni tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda kwenye mradi mmoja ambao ulikuwa haujakamilika, tukauliza wanafunzi wapo wapi ambao walitakiwa waingie kwenye hayo madarasa mwezi Januari, wakatuambia kwamba waliopo wanatosheleza madarasa yaliyopo na bado kuna madarasa yanabaki. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba uchambuzi au uchaguzi wa eneo la mradi haukuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la upungufu wa watumishi, imeonekana kwenye halmashauri nyingi zenye upungufu mkubwa, ni halmashauri zilizopo pembezoni au vijijini na siyo kwamba hazipati mgao wakati ambapo tunaenda kutoa ajira mpya. Wale watu wanapata ajira na baada ya muda mfupi wanahamia mijini kwenye zile halmahsauri zenye mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo nililokuwa nalo ni kwamba ikibidi tuangalie yale maeneo kama kuna wataalamu wa asili yaani wale wa kutoka maeneo hayo, wapewe kipaumbele ili tuondoe hili tatizo la kuhama. Hii ni kwa sababu imeonekana watu wanapelekwa huko baada ya muda mfupi wanaenda maeneo ambayo ni ya mijini kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Moshi ambayo yana mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na matatizo kwenye miradi inayotekelezwa na taasisi ambazo ni za kwetu sitaki kuzitaja (Taasisi za Serikali) ambazo zimechukua kandarasi ya kutengeneza miradi kwenye taasisi nyingine za Serikali. Sasa uwajibikaji hapa umekuwa mgumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta ni Taasisi ya Serikali imepewa hela, mradi hauna kiwango, fedha imeshatolewa, mradi haujakamilika, uwajibikaji unakuwa mgumu. Tuangalie namna bora ambapo Taasisi za Serikali zinachukua kandarasi kwenye maeneo ambayo tunatengeneza hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo eneo la *hybrid;* tulikuja na *terminology* ya *hybrid* kwa sababu mradi unaonekana unatekelezwa kwa *force account,* lakini kuna mkandarasi

ambaye ndiye amepewa fedha kwa ajili ya kulipa watu. Sasa tunajiuliza hii inakuwaje? Au unakuta mradi unatekelezwa na mkandarasi, lakini hana fedha, ameomba atanguliziwe fedha kama vile na yeye ana *force account*. Kwa hiyo, tukasema ni vizuri hii miongozo isimamiwe ili hii miradi iweze kuleta tija kule ambako inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mradi tumeutaja kabisa Mradi wa Stendi ya Ngangamfumuni pale Moshi Mjini. Ninajua Serikali inajitahidi sana kuhakikisha tunapata fedha ya kukamilisha. Nami ningeomba ni mahali ambapo tumeshaingiza fedha zaidi ya shilingi bilioni nane, sasa tumekwama tunashindwa kuuacha na kutoa hiyo fedha. Ni vizuri tufunge roho, tutoe hela, mkandarasi amalizie, ni chanzo cha mapato kwa Moshi Mjini kitaisaidia halmashauri kujisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mchungahela, wajiandae Mheshimiwa Simai Sadiki, Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Maganga na Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kama Wabunge tumeshuhudia na kuona kwamba tusiwe wachoyo, kukaa kusubiri mtu afe ndipo tuanze kumsifia au kumvika taji. Kwa jinsi utekelezaji wa majukumu yake unavyoonekana waziwazi katika kila kona ya nchi hii na maendeleo makubwa katika nchi hii yanavyokuwa yakionekana kila mahali, imeonekana dhamira yake ya uwazi kabisa kwamba anaitendea mambo mema nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo sisi kwa niaba ya wananchi tunalo jukumu la kuonesha haya mambo waziwazi kwa wananchi wetu katika mazingira waliyokaa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo sasa nitaendelea kufanya hivi kwa sababu ninawiwa kuona kwamba jambo analolifanya ni jema, pamoja na sifa hizi njema hali kadhalika kuna changamoto hapa na pale ambazo zinaweza zikaonekana katika utimizaji wa majukumu kwa maeneo kadhaa, hususani katika vipengele vya halmashauri ambazo sisi kama Wabunge au Wajumbe wa Kamati ya *LAAC* tumeona.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi changamoto kadhaa kama zitaondolewa bila shaka yale makando kando madogo yataonesha kuwa mambo mengi ni mazuri katika utekelezaji katika Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka nizungumze hapa ambalo lenyewe limekuwa ni changamoto kubwa, ni changamoto inayotokana na uteuzi. Sisi tunafahamu kuwa jukumu la uteuzi ni jukumu la Mheshimiwa mwenyewe, lakini pamoja na hayo bado kuna watu wa karibu ambao wanashauri. Hatuna shaka hata mara moja kwa Mheshimiwa, lakini tunashauri wale ambao wanaweza kumshauri kwenye jambo hili basi wamshauri kwa weledi kusudi yeye atekeleze jukumu hili kwa ufasaha mzuri na liwe jema kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, imetokea mara kadhaa kuna mtu ameharibu katika eneo fulani kwa maana Maafisa Masuuli kwa mfano, ameharibu katika eneo lake la kazi, lakini baada ya muda mfupi unakuta mtu huyo huyo amechukuliwa amehamishiwa eneo lingine, amefanyiwa uteuzi lakini kwa kuhamishiwa katika eneo lingine la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limekuwa mara nyingi sana likituharibia, japo dhana yake ni nzuri, lakini unakuta yule mtu alishaharibu kule alikotoka hali inayofanya hata huko anapokwenda bila shaka atakwenda kuharibu.

Sasa Mheshimiwa Rais yeye siye Mungu, hawezi kujua kila kinachoendelea katika kila eneo. Hawa watu wa karibu yake ni watu wenye jukumu la kumshauri kwamba huyu ameharibu hapa, kwa hiyo, hastahili kuendelea na hili jukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo ambalo nilitaka nilizungumzie kwa *issue* hii kwamba kunatakiwa kuwe na *clearance*. Kabla mtu hajahamishwa katika eneo lingine basi kuwepo na utaratibu wa kum-*clear* mtu huyu kwamba huyu yuko safi, hapa anapohamia atafanya kwa weledi. Ninafikiri hilo litakuwa jambo jema sana la kutu-*guide* sisi tukaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza linahusiana na Maafisa Masuuli na utendaji wao wa kazi kutokuwa wa wazi. Jambo hili limesababisha pia changamoto kubwa, mara nyingi sana kumekuwa na usiri katika utekelezaji wa majukumu hasa kwenye miradi. Unakuta ni mradi umekwenda eneo fulani lakini hapo hapo unakuta watu (wadau na wananchi) wakitaka kupata taarifa hazitolewi kwa uwazi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchungahela muda wako umekwisha. Mheshimiwa Simai Sadiki, ajiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja ya Kamati pamoja na mapendekezo yote yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Taifa limekuwa likishuhudia mabadiliko makubwa ya kimapinduzi katika ujenzi wa miundombinu ya sekta mbalimbali zikiwemo afya pamoja na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali yetu ya Tanzania inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kuwekeza fedha nyingi kwa

kupeleka katika miradi ya afya na elimu. Tunapowekeza kwenye afya maana yake tumewekeza kwenye uhai na ustadi wa jamii, lakini tunapowekeza kwenye elimu maana yake tumewekeza kwenye ujenzi wa Taifa ambalo litakuwa ni bora zaidi kimaadili na mtiririko wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo tunapata picha kwa nini Serikali imeamua kuwekeza fedha nyingi katika taasisi ya elimu nzima. Ukiangalia kwa udhati kabisa ripoti ya Kamati, ukiunganisha na ripoti ya CAG utabaini kwamba kwenye kasoro ndiko kunakotekelezwa. Tusingeweza kuzungumza kasoro au mafanikio ya miradi ile kama Serikali haijawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa umakini zaidi inawezekana ukabaini kwamba kasoro na changamoto zilizopo katika miradi hii ni ndogo zaidi kuliko mafanikio na tija ya miradi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwa undani zaidi ni kwa nini changmoto na kasoro hizi zinatokea, wakati mwingine unaweza ukabaini kwamba miradi hii, mara nyingi tunapokwenda kuitekeleza, kabla ya kuanza, tunakosa kufanya tathmini za kina kuhusu uhalali na undani wa eneo hilo na kama linatosha na linamilikiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema tunaangalia kigezo cha kwamba eneo hili linatosha maana yake nini? Tunapaswa, kama Taifa kuwekeza katika miradi kama vile elimu na afya tuwekeze katika maeneo makubwa yatakayoweza kutosheleza mahitaji ya maisha ya sasa na ya baadaye. Hii ni kwa sababu sasa hivi tuna uwezo wa kujenga shule, lakini baada ya miaka miwili au mitatu, tunakuta eneo lile ni dogo, jamiii imeongezeka, na hatuna tena eneo la kutanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile inawezekana tukakuta eneo lipo, lakini zamani tulikuwa tuna maeneo makubwa ambayo Serikali iliweka. Hata hivyo, maeneo hayo yalikuwa yanakosa hati, wananchi walikuwa wanavamia. Lengo la Serikali lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunatenga maeneo makubwa kwa ajili ya

ujenzi, kwa sababu taasisi kama vile elimu na afya zimekuwa na kawaida ya kukua na kupanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu una uwezo wa kuanza na *primary*, sekondari na baadaye chuo kikuu. Si kwamba ni lazima sekondari ukajenge kwake, chuo kikuu ukajenge kwake na sekondari ukajenge kake. Vilevile unaweza ukawa na eneo moja tu ukajenga vitu vyote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye afya na yenyewe vilevile unaweza ukanza na zahanati, eneo lile lile ukajenga kituo cha afya na baadaye ukaja hospitali. Si kwamba kila kitu uende ukajenge kwake. Maana yake ni nini? Ni lazima kuwe na ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Ardhi na TAMISEMI katika ujenzi na matumizi mazuri ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuangalie kigezo kingine; je, tunapojenda miradi hii ya sasa, eneo hili linafaa? Tunaposema linafaa, maana yake ni lazima tuangalie kwamba linafaa kimazingira. Kuna maeneo mengine tunapojenga unaweza kukuta tunatumia gharama kubwa jambo ambalo si lazima kutumika kwa wakati ule. Unaweza kukuta msingi tunaokwenda kujenga unakula takribani nusu ya gharama za mradi mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bado hatujawa na uchache wa maeneo kiasi hicho. Kuna maeneo mengine tunakwenda kujenga, unakuta mtoto akitaka kwenda shule, anavuka barabara tatu, nne mpaka tano kitu ambacho kimesababisha ajali nyingi kwa watoto wetu. Hivyo ili kupata kigezo cha eneo kufaa lazima pia tuangalie usalama wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunapojenga shule unakuta kabisa ipo katika eneo ambapo mji unapanuka na kuendelea kuelekea eneo hilo. Hata hivyo, tunalazimisha kujenga shule pale. Baada ya muda mfupi, unakuta shule hiyo imezungukwa na *bar, hotel,* stendi za *taxi* na mabasi na maduka hali ambayo inaathiri maadili ya watoto wetu kielimu, kwa

sababu mazingira yana nafasi kubwa katika kumfunza mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote kwa yote, niwashukuru sana Serikali yetu kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya kwa sasa. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca, wajiandae Mheshimiwa Maganga, Mheshimiwa Bulaya. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI jiandae pia.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* na nitatoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijaendelea mbali naipongeza sana Serikali kwa kuwa sisi tumefanya kazi na *CAG* ni jicho letu. Tunajua kazi kubwa ya *CAG* ni kufanya udhibiti wa fedha za umma na kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa sababu kwanza wameonesha nia ya dhati ya kuiwezesha Ofisi ya *CAG* kwa kuwapandishia bajeti kutoka shilingi bilioni 67 mpaka sasa wamefikia shilingi bilioni 112. Pia kuwaongezea watumishi 164 na kuwawekea maabara ya kisasa kabisa inayowasaidia wao kufanya uchunguzi wa kina, hasa kwa zile fedha za Serikali zilivyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu ya jambo nitakalokwenda kulisema. Kamati yetu imepitia miradi mikubwa mitatu; kwenye elimu, afya na majengo ya utawala. Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye elimu. Kwenye elimu ya awali na msingi, zaidi ya shilingi bilioni 230 imekwenda kuboresha miundombinu ya shule zetu za awali na msingi, lakini kwenye elimu yetu ya sekondari kupitia *SEQUIP*, Serikali imepeleka fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga shule za sekondari za sayansi za wasichana kwenye kila mkoa ambapo

shule zile zimegharimu zaidi ya shilingi 4,100,000,000 kwenye kila mkoa, kwa kuanza na mikoa 10 baadaye mikoa 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba taarifa yetu inasema kwamba shule iliyokamilika ni moja ya Mkoa wa Ruvuma, lakini hizi shule nyingine nazo ziko kwenye hatua nzuri ya kuweza kutumika, kwa sababu miundombinu yake imekamilika. Kwa hiyo, taratibu nyingine zinaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majengo ya utawala, Serikali imepeleka fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala kwenye halmashauri zaidi ya 122 nchini, 66 zimekamilika na nyingine bado, lakini ni nia ya dhati ya Serikali kuona kwamba utendaji kazi wa halmashauri zetu unaendelea kuwa mzuri, ninawapongeza sana. Zipo changamoto ambazo zimesemwa kwenye maoni ya Kamati, tunaomba zizingatiwe, ikiwepo mtiririko wa fedha kuzingatia miongozo, kuona fedha zinakwenda kwa wakati, kufuatilia zile taratibu za manunuzi ili miradi hii iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii imepeleka zaidi ya shilingi bilioni 374.86 kwenye halmashauri 129 nchini, kwa ajili ya ujenzi na kuimarisha miundombinu ya afya ikiwemo, ukarabati wa hosipitali, ujenzi wa *ICU*, majengo ya dharura na majengo mengine yote yanayohusiana na miundombinu ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunaipongeza Serikali, wapo watu wengine wanaona kama wivu hivi, lakini haya ndiyo mambo ambayo yamefanyika. Pragramu ya kuboresha huduma za afya nchini imeanza tangu mwaka 2018/2019, lakini kwa mwaka huu mmoja tu, tayari hospitali 129 kwenye halmashauri zimepelekewa fedha za kutosha na zimejengewa hospitali na ndiyo maana tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawaomba Watanzania, nchi hii ni ya kwetu, hatuna nchi nyingine tuliyowekewa akiba kama hii tukiivuruga. Sasa basi ninachoomba kuwaambia Watanzania, duniani tunavyoishi kuna watu wenye sifa mbili. Hizi ni

sifa, maana nikisema hapa usije ukasema nimesema tusi, ni sifa za watu. Wapo watu wapumbavu na wapo watu wajinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujinga unafutwa kwa mtu kutafuta maarifa, lakini sifa kubwa ya mpumbavu ni kukataa maarifa kwanza na upumbavu ni kupenda uovu. Upumbavu ni kutengeneza fitina; hizi maana nimezichukua kwenye Biblia. Mpumbavu anapenda kutengeneza fitina.

Sasa ninawaomba Watanzania, nchi yetu iko salama na nchi hii Mungu aliweka makimbilio ya nchi nyingi, ndio maana sisi tulikuwa viongozi wa kuhakikisha tunapambania nchi za Kusini mwa *SADC* zipate uhuru. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SAPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa, unga mkono hoja, ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, eeh! Ah, nilikuwa nimeona kuna...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda umekwisha, *rules are rules*. Mheshimiwa ninakuomba ukae.

Mheshimiwa Nicodemas Maganga, ajiandae Mheshimiwa Bulaya na ajiandae Mheshimiwa Katimba.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mchana wa leo. Ahsante sana, ninashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na nchi, kwa kuweza kupata fursa na nafasi hii ya kuweza kuijadili na kuishauri hoja ya Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaungana na Wanakamati, mimi siyo Mjumbe wa Kamati hii, lakini ninawaunga

mkono. Nimeisoma taarifa kwa mtiririko, jinsi walivyopangilia ushauri wao kwa kuishauri Serikali wapo vizuri. Kuna hoja ukurasa wa nane inasema kwamba utekelezaji wa hoja tulizoishauri Serikali hapa ni 60%. Hii inaonesha kwamba ni kwa jinsi gani hawako tayari kufuata ushauri wetu tunaposhauri Bungeni. Ni 60% badala ya 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukurasa wa tisa nimeona hapa na penyewe kuna changamoto kubwa. Hivi sasa nitumie fursa hii na kuiomba Serikali, pale tunapoishauri kwenye mawimbi wawe *serious* kidogo ili waweze kuendana na sisi Wabunge jinsi tunavyohitaji mahitaji, ili tuweze kuisimamia vizuri Serikali na kuhakikisha azma ya wananchi wetu waliotuamini kuja hapa, wanafanya hivyo kama wanavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninatumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwanza kwa kuniletea Mkurugenzi mwingine mpya kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbogwe, ninampongeza sana. Pia ninawapongeza wananchi wangu wa Mbogwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa majukumu yangu ya Kibunge. Hakika nitaendelea kusimama imara kuhakikisha kwamba Mbogwe tunapiga hatua kutoka pale tulipo kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuniletea *DAS* mwingine tena. Sasa kwenye usimamizi wa pesa za Serikali kwenye Wilaya ya Mbogwe, tunaenda kumaliza changamoto zote za wananchi ambazo zimekuwa zikiwasumbua kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiishie kushukuru tu na kupongeza, nizungumzie shida ambayo inatusumbua sisi Wabunge wa vijijini ambayo ni kuhusiana na watumishi. Amezungumza Mbunge wa Moshi, watumishi wanapoajiriwa wanakuja kwetu kwenye majimbo ya vijijini, lakini baada ya muda wanahamishwa wanaenda mjini. Serikali ione kila sababu ya kuweza kusimamia na kutenda haki, hawa watumishi na wao waweze kuishi vijijini, kwa sababu sisi Wabunge tunaishi humo humo vijijini. Inakuwa shida kidogo pale watumishi wanapokaa

kidogo halafu wanahamishwa wanaenda sehemu nyingine, hii inasumbua sana. Matokeo yake wale wananchi wa vijijini wanakosa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili hapa tunayo maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu ya wananchi toka mwaka 2012. Kijiji cha Kashero, pale Lulembela nina boma huwa linanisumbua sana kila wakati. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali Kuu iweze kutoa pesa kwenye maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi ili haya maboma yaweze kukamilika na yaweze kuanza kufanya kazi. Tuna maboma ya zahanati, tuna maboma ya shule yote yanahitaji pesa. Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba upo uweze kutusaidia sana kwenye *angle* hii ili kusudi tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shida za miundombinu; wakandarasi wengi hawalipwi kwa wakati mwafaka. Nina *messages* nyingi ninazipata kwa wakandarasi kwamba wametengeneza barabara, lakini bado wanahangaikia malipo. Mvua zilinyesha sana mwaka jana, sasa Serikali ione kila namna ya kupeleka pesa kwa wakandarasi hawa ili kusudi tuendelee kuboresha barabara pamoja na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia changamoto nyingine ni umeme; yapo maeneo ambayo yanahitaji kuwekewa umeme kwenye vitongoji vyetu. Tunaiomba Serikali itoe pesa ili kusudi wananchi wetu waweze kuunganishiwa umeme ili na wao waweze kupata huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu shule chakavu, tuna shule chakavu nyingi kwenye majimbo yetu. Hapa na penyewe Serikali ipaangalie, watoto wanakaa chini, hakuna madawati, vumbi nyingi, watoto wanateseka sana. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali hapa na penyewe iweze kutoa pesa ili tuweze kusaidia wananchi wetu, tuweze kuendelea na maisha mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninapenda kuwapongeza watumishi wote wa Serikali wale wenye mapenzi mema. Nina imani kabisa tunao watumishi wema, kwa sababu huwa

tunapanga bajeti hapa na tunapeleka pesa huko vijijini. Sisi Wabunge huwa tunabaki hapa kujadili. Kwa hiyo, watumishi wetu wale wanaosimamia kazi na kuhakikisha kwamba pesa zinafanya sawasawa, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninawalaumu wale wachache, maana wamo wachache kidogo tu, hata ukiangalia hii ya Ripoti ya *CAG* pamoja na *LAAC* ambayo inazungumzia kwamba wapo watumishi wengine siyo waaminifu. Hapa sasa niseme kwamba mamlaka zinazohusika, pale linapojitokeza tatizo kwenye *angle* fulani, Mawaziri tumeona hapa huwa mnatoa miongozo, lakini ni 50% tu ambayo inafanyiwa kazi huko mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Mawaziri, ninyi mpo kwa ajili ya kumsaidia Rais, chukueni hatua mapema, tusijekungoja mpaka mtumbwi utoboke, halafu tuanze kuhangaika kutoa maji. Ninyi mnayo mamlaka kutoa maelekezo huko mikoani. Kwa hiyo, mnapotoa miongozo au maelekezo, inaonekana mkoa fulani haufuati na hauzingatii miongozo mliyoitoa chukueni hatua. Kwa sababu ukurasa wa tisa hapa unaeleza, miongozo inayotolewa na Mawaziri ni 50% tu ambayo inatekelezwa. Ina maana 50% hazifanyiwi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawa watendaji walioko mikoani hawafuatilii miradi, hawaangalii na hawakagui, lakini wanalipwa pesa na Serikali na wameaminiwa na Serikali, lakini hawafanya kazi yao ambayo imewakalisha huko mikoani. Kwa hiyo, mimi ninawaomba Mawaziri chukueni hatua mapema tusijekusubiria kuhukumiwa na huu mwaka ni wa uchaguzi. Bora sisi tuhukumiane kwanza huku, halafu baadaye sisi tutahukumiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Endelea kunipa nafasi siku nyingine niweze kuendelea kulisaidia Taifa langu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, ajiandae Naibu Waziri, TAMISEMI.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa moyo wa dhati kabisa ninakipongeza Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuonesha nini maana ya uchaguzi huru na haki na kumpongeza Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa kubeba gharama za demokrasia, kwa kukubali kushindwa na kukubali matokeo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwaambie, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa Mnadhimu wa Kambi, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Chama, ana uwezo wa kukiongoza chama na kutufikisha kwenye demokrasia ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makamu - John Wegesa Heche alikuwa Mwenyekiti wa BAVICHA, alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu zaidi ya miaka kumi, ana uwezo wa kuwa Makamu Mwenyekiti na kumshauri vyema Mwenyekiti na kuhakikisha tunafika kwenye demokrasia ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba nichangie Taarifa ya *LAAC*. Katika vitu ambavyo Mwenyekiti wetu amevisema, moja ni kuhusiana na maazimio ya Bunge kufanyiwa kazi. Mwaka jana tulizungumza hapa ni namna

gani Serikali haiyafanyii kazi maazimio ya Bunge kwa kiwango cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Mwenyekiti anasoma taarifa yake, maazimio yaliyotekelezwa kwa 100% ni 10%; 90% bado hayajatekelezwa. Tunaambiwa yapo kwenye hatua za utekelezaji kwa nafasi mbalimbali; 60%, 38% na kuendelea. Taarifa ambayo imeshapita na wakati zaidi ya mwaka, maazimio ya Bunge yaliyotekelezwa ni 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dharau kwa Bunge, huku ni kufanya kazi kwa mazoea kwamba Taarifa hii ya *LAAC* itakuja itasomwa, tutasikiliza, watu watachangia, tutajibu halafu maisha yanaendelea. Hatuwatendei haki wananchi, hatujitendei haki sisi wenyewe, hatulitendei haki Bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mwenyekiti anasoma taarifa yake amezungumzia baadhi ya taasisi za Serikali kupewa kandarasi na kutotimiza majukumu yao, mbali na kupewa fedha. Hapa tunazungumzia SUMA JKT na tunazungumzia na *TBA*. Ninatolea mfano kwenye Halmashauri ya Mji wa Ifakara. *TBA* imepewa kazi ya kujenga jengo la utawala tangu mwaka 2018, thamani ya jengo ni shilingi bilioni saba, *TBA* imepewa zaidi ya shilingi bilioni 4.7 ikamilishe jengo walau kwa 70%. Jengo liko 47%; limetelekezwa, hayuko *site*, limekuwa gofu. Majengo ambayo halmashauri nyingine zinajenga kwa shilingi bilioni 2.5, shilingi bilioni tatu; shilingi bilioni saba! Zaidi ya mwaka wa saba! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu *TBA* ameshatoroka *site* zaidi ya mara tatu. Cha kushangaza bado anaitwa na anaongezewa shilingi milioni 500, kuna nini? Nani anamlinda? Tuliuliza kwenye Kamati, inakuwaje wewe Mkurugenzi mpya umefika unakubali kumpa tena awamu nyingine ya mradi shilingi milioni 500, ameshatumia zaidi ya shilingi bilioni 4.2, katelekeza mradi zaidi ya mwaka mmoja? Hana majibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *RAS* anaulizwa anasema, ooh, mimi niliona tuwakutanishe pamoja. Umkutanishe pamoja mtu

aliyeshindwa kutimiza wajibu wake? Kala hela za walipakodi shilingi bilioni 4.7, bado unampa aendelea na mradi? Halafu Mkurugenzi yuko salama tu, kinachofanyika anatoka kituo hiki anapelekwa kituo kingine. Haya mambo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuwezi kuyafumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo huyo *TBA*, nenda Kakonko, hii nchi na ni Mkurugenzi tu yupo ofisini. Kwenye mradi anatakiwa kulipwa shilingi milioni 500, kabla ya mradi analipwa zaidi ya shilingi milioni 200 ziada. Mradi una thamani ya shilingi milioni 500, analipwa shilingi milioni 700 na kazi haiendi. Ni Mkurugenzi gani ana mamlaka ya kukiuka taratibu za malipo, kumpa mkandarasi pesa ya ziada shilingi milioni 200, na bado yuko kituoni? Yaani huyu akipewa adhabu anahamishwa anapelekwa anaenda eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo hatuwezi kuyafumbia macho. Kakonko mradi wa shilingi milioni 500, *TBA* anapewa shilingi milioni 700 na kazi haiendi. Nenda Nyasa hapo walikuwa wote wawili, mradi wa shilingi bilioni 1.5, SUMA JKT kafanya yake kaharibu, hakuendelea. Kaja *TBA* hakuendelea, mradi haujakamilika. Kuna nini kwa hawa watu? Wanapewa pesa za walipakodi wakamilishe miradi itakayotoa huduma kwa wananchi na kazi haitendeki, hatuwezi kufumbia macho. Hivi kama mkandarasi *private* (mzawa) angefanya haya angeendelea kupewa pesa? Kwa nini tunalinda uovu? Tumeuliza Kakonko huyu Mkurugenzi yuko wapi? Tunaambiwa ooh alihamishwa akapelekwa TAKUKURU. Ndiyo yale yale Mheshimiwa Mwenyekiti amesema, TAKUKURU inatumika kama kichaka cha kuficha wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ameiba hela za *POS* unampeleka TAKUKURU. Kachukua rushwa au ameiba hela ya halmashauri? TAKUKURU inakaa mwaka mzima. Hatuwezi kufumbia macho mambo ya namna hii ya watu kula pesa za miradi, watu kulinda wezi, watu kufanya makosa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ester. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, ajiandae Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza, ninaomba nianze kwa kuipongeza Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Controller and Auditor General – CAG)*, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaotupatia sisi, wanapotoa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo kimsingi yanalenga kuja kwetu sisi kuboresha utendaji kazi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba nitoe shukrani kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ambaye chini ya uongozi wake yeye anatusimamia sisi pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na wataalamu mbalimbali waliopo huko ambao wanasimamia mamlaka zetu hizi za Serikali za Mitaa. Tunamshukuru sana kwa uongozi wake mahiri ambao unapelekea ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwanza tunapokea maoni ya Kamati na tutaenda kuyafanyia kazi, lakini kuna baadhi ya maeneo naomba niyagusie. Kuhusiana na suala zima la utekelezaji wa miradi na kugharamia miradi ile kutokana na mazingira au jiografia ya eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, tunatambua umuhimu wa kutenga fedha za miradi ambazo zitaenda kutosheleza ukamilishaji wa miradi katika eneo husika na tumefanya mapitio ya gharama ya miradi kwa kuzingatia jiografia na kanda. Katika mwaka wa fedha 2025 tunatarajia kwamba tutaanza kutumia hivi viwango vipya ambavyo vitakuwa

vinalenga kuhakikisha miradi inakamilika kwa ukamilifu wake na zile bajeti zinakuwa zinatosheleza, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika mapitio hayo kwa ujenzi wa madarasa kutokana na gharama za kikanda, kanda zinatofautiana gharama za ujenzi. Kwa hiyo, mathalani kwenye madarasa tunatarajia kiwango kitaanzia shilingi milioni 22 mpaka milioni 25, lakini kwa mfano, katika upande wa afya, kwenye zahanati tunatarajia kwamba viwango hivi vipya vitaanza kutumika, shilingi milioni 284 kwenye baadhi ya kanda, lakini kuna kanda ambazo zinagharama kubwa zaidi ya ujenzi ambapo, zenyewe zitapelekewa shilingi milioni 358.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunatambua hoja ambayo imechangiwa na Kamati. Waheshimiwa Wabunge na wenyewe pia wamegusia eneo hili wakiwa na lengo la kutaka kushauri kwamba miradi iweze kukamilika kwa wakati kwa kupelekewa fedha zinazotosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Ofisi ya Rais - TAMISEMI, suala hilo tumelipokea. Tayari tumeanza kulifanyia kazi na tutaenda kwenye utekelezaji katika mwaka wa bajeti ya 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala zima la tathimini na usimamizi wa miradi; Waheshimiwa Wabunge wamegusia pia katika eneo hili na kutoa msisitizo kwamba miradi yetu inahitaji usimamizi na tathimini ya karibu ili iweze kukamilika kwa wakati na iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, tayari tumeshaweka utaratibu wa viongozi wetu wa mikoa, wa wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa waweze kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi kwenye maeneo yao. Tayari Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imetoa mwongozo huo na tayari umeanza kutekelezwa, tutaendelea kuusimamia ili fedha nyingi ambazo Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anawekeza katika sekta muhimu na nyeti kabisa ziweze kuwa na tija iliyokusudiwa

kwa miradi kuweza kukamilika kwa wakati na kwa viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge pia waligusia kwenye eneo hilo la miradi kuweza kukamilishwa kwa wakati na changamoto mojawapo ikiwa ni mifumo yetu hii ya kimanunuzi *(NeST)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili, sisi kama Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tayari tarehe 12 ya mwezi huu tulikaa kikao na Wakurugenzi wote wa Halmashauri 184, Maafisa Ununuzi, Makatibu Tawala ambao wanasimamia miundombinu katika Sekretarieti zetu za Mikoa pamoja na uwakilishi wa baadhi ya Wabunge hawa, kwa ajili ya kufanya mapitio na mafunzo ya kuwajengea uwezo ili mifumo hii iweze kuwa na tija, isikwamishe utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, pamoja na Wizara ya Fedha tutaendelea kushirikiana kukwamua changamoto za kimifumo hasa mfumo huu wa manunuzi, popote inapotokea tuweze kukwamua ili miradi iweze kutekelezwa na ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kushirikiana na taasisi nyingine, hasa pale miradi inapokuwa imekamilika isikwame na kushindwa kutoa huduma kwa sababu imekosa huduma nyingine za muhimu kama maji, barabara na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ofisi ya Rais - TAMISEMI tunashirikiana na wenzetu na tutaendelea kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta ili miradi yetu inapokuwa imekamilika iweze kuanza kuwahudumia wananchi, isikose maji, isikose huduma muhimu ya barabara na isikose huduma muhimu ya umeme. Hivyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu katika kuhakikisha hilo. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uwekezaji mkubwa sana katika kipindi

hiki cha miaka minne. Ukitazama katika sekta ya afya pekee amefanya uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 1.29 kwa ajili ya kuhakikisha anaboresha miundombinu ya hospitali zetu, zahanati na vituo vya afya. Ananunua vifaa na vifaatiba na kuboresha rasilimali watu kwa ajili ya kwenda kutoa huduma hizi muhimu kabisa za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa elimu, amefanya uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni tatu kuhakikisha anaboresha miundombinu ya kutolea huduma hii muhimu kabisa ya elimu kwa Watanzania ili waweze kupata maeneo mazuri. Watoto wao wapate maeneo mazuri ya kusomea na walimu wapate maeneo mazuri ya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa sekta ya barabara, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya hivyo pia na ndio maana bajeti ya barabara hizi muhimu kabisa za *TARURA* ambazo ni za wilaya, imeongezeka kutoka shilingi bilioni 275 kwa mwaka mpaka sasa ni shilingi bilioni 710. Huu ni uwekezaji mkubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, malizia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili fedha ziweze kupatikana kwa wakati na ziweze kwenda kukamilisha hii miradi muhimu sana na ile dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kufanya uwekezaji na kuleta maendeleo kwa Watanzania iweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha, ajiandae mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Awali ya yote niseme naunga mkono hoja mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yetu ya Bunge ni mapendekezo ambayo Serikali tunakubaliana nayo na tutayafanyia kazi sambamba na maelekezo mengine yanayotolewa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme katika Kumbukumbu za Bunge, hili ni moja ya Bunge ambalo punde linapotoa mapendekezo yake Serikali imekuwa ikiyatekeleza bila kusita kwa sababu mmekuwa mkishauri, sambamba na dira ambayo Serikali tuko nayo. Kuna hoja zimetolewa ambazo ningetamani kuweka kumbukumbu sawa; moja ni hoja ya fedha ambazo zimeongelewa kwamba zinarudi wakati wa kumaliza mwaka wa fedha na pili ni kuna hoja za kupeleka fedha sawasawa na Bunge lilivyotenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mara zote imekuwa ni kupeleka fedha za maendeleo katika maeneo miradi inakotekelezwa. Mheshimiwa Rais ameliongea hili si mara moja, si mara mbili na maelekezo yake yamekuwa sahihi kabisa kwamba tusibaki na fedha benki, tusibaki na fedha zimetulia, fedha zote ziende kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yenyewe inayotekelezwa katika majimbo yetu ni ushahidi wa hiki ambacho Mheshimiwa Rais amekuwa akielekeza. Mimi nina bahati, nimekuwa Mbunge hii awamu ya tatu na nina bahati nimekuwa Serikalini hii awamu ya tatu, nilikuwa Naibu Waziri katika Serikali ya Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne na tena kuna wakati nilikuwa Nakaimu Uwaziri wa Fedha. Nimekuwa Waziri kwenye Serikali ya Awamu ya Tano na sasa nimekuwa Waziri kwenye Serikali ya Awamu ya Sita, tena kwenye Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kipindi tangu nchi hii iitwe Tanzania ambapo majimbo yetu yamepata fedha nyingi za miradi ya maendeleo kama kipindi hiki. Hakuna kipindi fedha zimekwenda kwenye miradi ya maendeleo kama kipindi hiki na

hakuna kipindi nchi yetu imetekeleza miradi mikubwa kwa mkupuo, kwa mara moja na fedha zikaenda kutekeleza miradi, kama kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiongelea Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere peke yake, ni zaidi ya shilingi trilioni 6.5. Kwa nchi nyingine hiyo ndiyo bajeti ya nchi nzima ya kufanya miradi ya maendeleo, lakini ni bwawa peke yake na limekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Reli peke yake mpaka kufika hapa ulipofika ni zaidi ya dola bilioni tano, ni zaidi ya shilingi trilioni 10 na mradi huu umetoka bandarini, umeshafika makao makuu ya nchi na kazi inaendelea, hivi tunavyoongea masuala ya fedha yameshakamilika kwa vipengele vyote. Mradi wa Reli peke yake kwa nchi nyingine ndio bajeti nzima ya shughuli za maendeleo katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hatujaweka miradi ya umwagiliaji, hatujaweka miradi ya huduma za jamii. Nchi yetu hii hii ilikuwa na *CT-Scan* mbili, *MRI* mbili, sijui *Ultra Sound* zilikuwepo tu kwenye mikoa. Sasa hivi tunavyoongea ni mpaka hospitali za halmashauri, manispaa, *MRI* kila ukanda, hamna kusubiri majibu kutoka Dar es Salaam. Hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakaporudi majimboni waambieni wajumbe wenu na anayeongea ndio Waziri wa Fedha, anayepeleka fedha huko kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba katika Ubunge wako, katika kipindi ambacho wewe ni mwakilishi wa wananchi katika jimbo lako, jimbo hilo halijawahi kupata fedha nyingi kama lilivyopata katika awamu hii ya Awamu ya Sita na wewe ukiwa mwakilishi katika jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa hii tunayoijadili ni kweli, kuna maeneo bajeti hatukuitekeleza kwa asilimia mia moja. Ni kweli na wala hatubishani na taarifa iliyosomwa na Mheshimiwa Halima Mdee, wala hatubishani, lakini ni mazingira yaliyojitokeza. Waheshimiwa Wabunge, imetokea katika mwaka wa fedha uliopita, wananchi wetu wamepata maporomoko ya udongo Mkoa wa Manyara, hauwezi ukasema ngoja nimalizie huu mradi

wakati wananchi wengine wakiwa wameporomokewa, hawana makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni katika hali ya ubinadamu tu, tunaheshimu ubinadamu kuliko bajeti, tunaheshimu ubinadamu kuliko hizi kanuni, kwamba wananchi wamefukiwa, hauwezi ukasema tunasimamia bajeti iende tulikoweka badala ya kuwatoa kwanza kwenye janga, halafu ndio miradi iendelee. Tunatekeleza miradi kwa ajili ya binadamu, kwa hiyo, ubinadamu unatangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, pia Kusini huku, mikoa mitatu ilikatika, ilijitenga ikawa kisiwa. Tulilazimika tuwakwamuwe kwanza wenzetu wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambao waliwekwa kama kisiwa baada ya barabara kuwa zimekatika na Bunge lako lilituelekeza hivyo, tuchukue hatua za haraka. Nimetaja tu maeneo machache, Bunge lako pia lilituelekeza tuchukue hatua za haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna maeneo ziliathiri mtiririko wa bajeti yetu, juzi niliongelea kuhusu maeneo ya miradi ambayo tulisema tufunge mikanda na yenyewe tuikamilishe. Ni kweli kuna maeneo hapa na hapa tulifunga mikanda, tulijifinyafinya, iliathiri, lakini nia ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha fedha zote zinakwenda kama Bunge lilivyoelekeza na hicho ndicho ambacho tutaendelea kukifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nawaambia Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo yaliyoletwa na Kamati yetu tuyapitishe. Maelekezo ya Kamati ni samabamba na maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiyatoa na sisi tutaendelea kuwa tunayatekeleza kama yalivyoletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuiongezea Ofisi ya *CAG*. Tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie, kila mwaka tunaongeza fedha kwa *CAG*, kusudi lake ni ili fedha hizi zisimamiwe ipasavyo na *CAG*, ndio jicho lenu Waheshimiwa Wabunge. Tunamwongezea bajeti ili fedha za umma ziweze kutumika ipasavyo na hili tumekuwa tukilifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliongelewa pia kuhusu fedha zinazovuka mwaka. Bajeti yetu ni *cash budget*, tunakusanya ndipo tunatumia. Ni tofauti na nchi ambazo fedha ipo mahali wanapanga kuitumia, sisi tunakusanya ndipo tunatumia. Kwa hiyo, inawezekana hata kwenye taarifa huwa tunasema bajeti ya mwaka huu imetekelezwa kwa 95%, 96%, 97%; tunaendelea kuongeza makusanyo na tunaendelea kuajiri watumishi wa Mamlaka ya Mapato, hii yote ni kwa ajili ya kuongeza ukusanyaji, ili bajeti itimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja niwahakikishie kwa niaba ya Serikali, hakuna mradi wowote utabaki gofu kwa sababu fedha hazikuvuka mwaka, kwa sababu bajeti ya mwaka ule haikutosheleza kwenye mradi ule. Hata maeneo ambayo miradi hiyo ilikutana na changamoto katika vipindi vilivyopita tunaendelea kuongea ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba miradi hiyo inapata fedha ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ambao mna maeneo yenye miradi ya aina hiyo, tutaendelea kuitengea fedha hata kama katika mwaka mmojawapo, labda kwa ajili ya makusanyo, fedha haikutimia ya kuweza kukamilisha mradi huo, tutakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutavuka, kama nilivyosema majuzi, kwenda mpaka na kwenye guvu za wananchi, kwenye miradi ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi. Tutaiwekea fedha kuhakikisha kwamba, inakamilishwa, ili nguvu za wananchi wetu ambao wanajitolea, kwa ajili ya kuijenga nchi yetu zisiende bure.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshasikia kengele ya mwisho. Nilimsikia dada yangu, bibi yangu, Mheshimiwa Ester akisema kwamba Tundu Lissu anaweza na Mnyika anaweza na Heche anaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndivyo na sisi tulikuwa tunaona hivyo, ndivyo na si tulikuwa tunaamini hivyo, ila wao wenyewe wakati wa uchaguzi walituambia mtu yule hatoshi hata kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji, siyo sisi. Sisi tumeshafanya naye kazi hata hapa, tumefanya nao kwenye Kamati, tumefanya nao, ila ni wao wenyewe wakati wa mchakato wametuambia na yeye akashangaa alivyokuwa anaambiwa hivyo, kwa hiyo, tunaomba bibi yangu usitulishe maneno hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba na mimi nihitimishe hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ninawashukuru Wajumbe wote ama Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Kwa sababu ya muda sitawataja, lakini naamini *Hansard* imewachukua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ambayo ilizungumzwa na Mheshimiwa Tarimo ni kuhusiana na Taasisi za Serikali ambazo zinapewa kandarasi. Hii hoja imezungumzwa pia na Mheshimiwa Bulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu wa Januari tumekutana na halmashauri 14/15, hiki kipindi cha wiki mbili tulizokaa. Karibu nusu ya halmashauri zina hii changamoto na ndio maana tumeliomba Bunge likubaliane na azimio letu ambalo litataka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akafanye ukaguzi wa kina kwenye miradi yote ambayo imefanywa na *TBA*. Kwanza kujiridhisha kwamba kuna thamani ya fedha na pili kujiridhisha kwamba imefanywa kama ilivyopaswa kwa sababu inasikitisha pale ambapo chombo cha umma kinahujumu umma wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani chombo cha Serikali kinaihujumu Serikali yenyewe kwa kupewa majukumu ya kufanya kazi, kupewa fedha na kutokutekeleza. Hiyo ni aibu ambayo haiwezi kuzuilika kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba mkaguzi akifanya ukaguzi wa kina kwa mawanda yake *then* itatoa mwelekeo wa hatua ambazo zinatakiwa zichukuliwe kwa kila mmoja ambaye ameshiriki kwenye mchakato huo wa kuhujumu Taifa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusiana na taratibu za malipo. Sisi tumekutana na halmashauri na ninataka hili Mheshimiwa Mwigulu ulichukulie kwa umakini wake. Tunafahamu linapokuja suala la wakandarasi maana yake ni kwamba ni taratibu tofauti na *force account*, haziendani sawa. Sasa kinachotokea hapa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sura mbili; ya kwanza ni *advance payment*. *Advance payment* kwa maelezo ambayo tunayo sisi na tunajua taratibu zinataka ni 15%. Yanatokea mazingira ambayo mkandarasi anapewa *advance payment* 30%. Sasa watu wengi wanaamini kwamba watu wanaomba kazi, halafu inapokuja kwenye *advance payment* ndio sehemu ya watu kulipana, wale waliyopewa kazi. Sasa inaposema 15%, unatoa 30%, hiyo 15% mliidhinisha kwa nini? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mkandarasi anapomaliza kazi ana *raise certificate,* kila siku mnatuambia hapa kuhusiana na *certificate*. *Certificate* inakuwa *raised* pale ambapo amemaliza kazi na mamlaka zote kuanzia halmashauri na wataalamu wake mpaka Mkoa, Ofisi ya *RAS,* wanaandika TAMISEMI, TAMISEMI wanapeleka Hazina, Hazina mnajiridhisha kazi imefanyika, ndio mnalipa. Leo kwenye halmashauri ambazo sisi tumezifanyia kazi, mkisoma taarifa kwa mapana, kuna halmashauri ambazo mkandarasi, achana na *that 15% advance payment,* yaani amelipwa *certificate in advance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haiwezekani ikawa sheria zinasema mambo mengine na utekelezaji unafanya mambo

mengine. Hilo ni la pili, kuhusiana na suala ambalo linagusa Wizara ya Fedha na haya masuala ya taratibu za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, teuzi za Wakurugenzi; Mheshimiwa Mchungahela amezungumza vizuri, nisingependa kurudia maneno yake na sisi tulishazungumza hapa kipindi kilichopita. Tulikuwa tunaishauri Serikali, la kwanza ni kabla hamjamhamisha Mkurugenzi kumpeleka mahali popote mjiridhishe kwamba nyumba yake aliyoiacha iko safi. Ni tatizo ambalo Kamati ya *LAAC* kwa miaka hii miwili ambayo nimeiongoza, pamoja na wenzangu, kama tutakutana na halmashauri 10, 15, wakurugenzi 10 ni wapya, sasa najiuliza, hivi hawa wanacheza karata na sisi? Yaani kwamba wanataka watuletee mtu ambaye anatuambia nimeripoti kituo cha kazi jana au majuzi? Hana majibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sawa kuna *collective responsibility,* lakini mtu amekuja ana wiki mbili, atajibu nini? Amezungukwa hapo na watu ambao ni makonki kwenye halmashauri iliyopita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunataka na tunaelekeza wakurugenzi wote watakaoteuliwa kwa sababu ni mamlaka ya Mheshimiwa Rais, ni masuala ya Kikatiba, sawa ateuwe, ili aende eneo lingine, hakikisheni nyumba yake ipo safi. Kama nyumba ipo chafu muacheni abaki ajibu uchafu wake ili mapendekezo yakitoka asionewe. Kuna wakurugenzi Ifakara huku, hatutaki kuwataja majina kwa sababu wengine ni wenzetu tukonao huku, mambo yameharibika, lakini tuko nao huku na uki-*trace* inawagusa. Sasa kwa nini mnataka tuanze kutajana, kila mtu afanye kazi na awajibishwe kwa wakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na masuala ya *TBA,* nimeshazungumza, watumishi. Nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Tarimo, ninajua kama nchi ni changamoto kuajiri kwa sababu *wage bill* ikiwa kubwa bado uwezo wetu ni mdogo. *I understand that,* lakini ni muhimu kama Serikali, mfanye *audit* ya watumishi mliokuwa nao nchi nzima halafu mjiridhishe kwamba hawa watumishi tuliokuwa nao na kazi ambayo wanatuzalishia na idadi ya watu wanaotuhudumia ina thamani sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, fanyeni *audit*, inawezekana tunasema tuna upungufu wa watumishi kumbe siyo asilimia tunazofikiria, inawezekana watu wanaenda asubuhi wanasoma magazeti, wanaondoka. Nendeni mfanye *audit* nchi nzima kwenye kila kitengo, kila idara, kisha fanyeni msawazo na lazima muwe *strict* kwenye hizi ajira mpya, walizungumza Wabunge hapa kwamba jamani siyo suala la kubaguana ni suala la kuwa halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hakuna mkoa usiokuwa na msomi, sasa hivi hakuna wilaya isiyokuwa na msomi, sasa hivi hakuna jimbo lisilokuwa na msomi. Kwa nini hizi ajira pamoja na mambo mengine tusi-*reflect* watu ambao tumewazalisha kwenye halmashauri zetu? Kwa sababu, leo tutaomba kazi, baada ya miezi miwili nasema, Halima nimeolewa, nataka niende kwa mwenza, aaahh!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Halima, muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Halima muda wako umekwisha, toa hoja tu. Ripoti umeisoma hayo unayoyasema ushayasema, kwa hiyo, *it is already in the…*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini nimeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa kwanza nitoe shukrani tena kwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo mmejadili hoja kwa weledi na ufanisi na tunaendelea kusisitiza kwa mapendekezo na tunashukuru kwamba hayajaletewa mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na ikubali

Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati yaliyotolewa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki. Sasa hii ni taarifa rasmi kwa Serikali ambayo imetoka kwenye Bunge kwenda kufanyiwa kazi na Serikali na tunategemea tu majibu sahihi yataletwa.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Niwashukuru upande wa Kamati kwa kazi nzuri mliyoifanya, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, hasa haya ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa mambo mazuri yaliyofanywa, yanayofanywa na yatakayoendelea kufanywa. *(Makofi)*

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.06 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 14 Februari, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*